

**TAFSIRI ZA METHALI NA MISEMO KATIKA *MSHALE WA MUNGU***

**NA**

**CHRISTINE OYARO**

**Tasnifu hii imetolewa kutosheleza baadhi ya mahitaji ya shahada ya uzamili  
katika idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Nairobi.**

**2019**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijawahi kutolewa katika chuo chochote kile kwa minajili ya shahada.

Sahihi.....

Tarehe.....

**CHRISTINE OYARO**

**C50/76797/2014**

Tasnifu hii imewasilishwa kwa madhumuni ya kutahiniwa kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa na chuo kikuu kupitia idara ya Kiswahili.

Sahihi.....

Tarehe.....

**PROF. RAYYA TIMAMMY**

Sahihi.....

Tarehe.....

**DKT. J. OMBOGA ZAJA**

## **KUTABARUKU**

Naitabaruku tasnifu hii kwa wazazi wangu wapendwa Simeon Oyaro Ogachi na Doris Nyanhoka Oyaro kwa kuniamini na kunifaa kwa hali na mali ili kufikia kiwango cha elimu nilichofikia.

## SHUKRANI

Kwanza kabisa ningependa kumshukuru Mungu kwa uhai, afya niliyo nayo, na kibali chake kwangu. Hakika kila jambo nililofanya liliwezekana tu kwa kuwa alikubali lifanyike. Shukrani za dhati ziwaendee wasimamizi wangu Dkt. J. Omboga Zaja na Prof. Rayya Timammy kwa kunielekeza vyema katika mchakato mzima wa kuandika tasnifu hii. Mungu awabariki kwa kunipa wakati wenu kwa ukarimu mwingi na kujitolea kwa mioyo mikunjufu kunipa msaada wenu kila nilipouhitaji; hasa katika nyakati ambazo ilikuwa vigumu kwenu kupata nafasi ya kutosha kuishughulikia kazi yangu. Shukrani vile vile ziwaendee wahadhiri wote katika Idara ya Isimu na Lugha Chuo Kikuu cha Nairobi; hasa Prof. Iribemwangi miongoni mwa wengine, kwa kunipa mwongozo na maelekezi yaliyonisaidia kufikiria na kutetea maswala ya kiusomi kiusomi, mmenipa mafunzo mengi ambayo yalitokea (na yanaendelea) kuwa msingi mwema katika usomaji wangu wa Kiswahili.

Kwa ndugu zangu wakubwa Gladys, Hellen na Isaac, singefaulu bila msaada mlionipa kila nilipokuwa na hitaji. Mwanangu mpendwa Alpha, na dada zangu wadogo Racheal na Abigael, kila mara nilipowakumbuka nilipata motisha kutia bidii katika usomi ili niwape mfano bora wa kuiga. Asanteni kwa kunivumilia kila wakati nilipochukua muda mrefu mbali nanyi ili kuniwezesha kukamilisha masomo yangu na hasa kuandika tasnifu hii. Wanafunzi wenzangu Veronicah, Mariga, Nina, Jacqueline, Musamali, Okello, miongoni mwa wengine, asanteni kwa kunipa nafasi kusoma pamoja nanyi na kukubali tuisaidiane kupitia kwa mijadala, kutiana moyo na kwa njia yoyote nyingine tuliyochangiana katika masomo yetu, pokea shukurani zangu kwa kuwa marafiki wa kweli.

Wakubwa wangu kazini ambao ni pamoja na: Bi. Naomi Makau, Bi. Virginia Kagendo na Bi. Veronicah Wambua, nashukuru sana kwa kunipa mawaidha mema na nafasi ya kutosha na kufanya shughuli zinazohusiana na kuandika tasnifu hii bila mivutano yoyote. Barikiweni sana. Wapo marafiki wengi ambao, mbali na kunipa masikio kila nilipohutubu kuhusu maswala ya tafsiri yasiyowahusu, walinitia moyo na kunisukuma kukamilisha tasnifu hii. Charles Munene, Esther Ondieki, Samuel Mwenda, Dorcas Muthui, Emily Miriti, Martina Munyao, John Nyamai miongoni mwa wengine ambao sijataja, asanteni sana kwa msaada mlionipa mara kwa mara. Bila mchango wenu kazi hii haingekamilika mola awabariki kwa ukarimu wenu.

## YALIYOMO

<b>UNGAMO</b> .....	ii
<b>KUTABARUKU</b> .....	iii
<b>SHUKRANI</b> .....	iv
<b>UFAFANUZI WA ISTILAHU NA VIFUPISHO</b> .....	viii
<b>IKISIRI</b> .....	ix
<b>SURA YA KWANZA</b> .....	1
1.1 Usuli wa mada.....	1
1.2 Tatizo la utafiti .....	7
1.3 Maswali ya utafiti. ....	7
1.4 Malengo Ya Utafiti .....	8
1.5 Sababu za kuchagua mada hii .....	8
1.6 Upeo na Mipaka.....	10
1.7 Yaliyoandikwa kuhusiana na mada hii .....	11
1.8 Misingi ya Kinadharia.....	17
1.9 Mbinu za utafiti.....	25
<b>SURA YA PILI</b> .....	27
<b>TAFSIRI YA METHALI NA MISEMO KAMA VIWAKILISHI VYA UTAMADUNI KATIKA ARROW OF GOD</b> .....	27
2.0 Utangulizi.....	27
2.1 Tafsiri za methali na misemo kama mfumo wa kimsingi katika wingimifumo ya kazi ya fasihi .....	32
2.2. Vizingiti katika kutafsiri methali na misemo.....	34
2.2.1 Udhaifu wa mtafsiri .....	35
2.2.2 Ufahamu finyu wa utamaduni wa LC.....	35
2.2.3 Tofauti pana za kitamaduni.....	36
2.3. Mikakati ya kutafsiri methali na misemo.....	38
2.3.1 Mkakati wa uhawilishaji .....	38
2.3.2 Mkakati wa utohozi.....	39
2.3.3 Mkakati wa usawazishaji .....	39
2.3.4 Mkakati wa viziada.....	40

2.3.5 Muungano wa mbinu za tafsiri. ....	40
2.3.6 Mkakati wa udondoshaji. ....	40
2.4 Mapendekezo ya wataalamu kuhusu uteuzi wa mikakati ya kutafsiri methali na misemo ....	41
2.5 Hitimisho.....	46
<b>SURA YA TATU.....</b>	<b>47</b>
<b>TAFSIRI ZA METHALI NA MISEMO INAYOWAKILISHA UTAMADUNI WA MAZINGIRA YA KIIKOLOJIA KATIKA ARROW OF GOD, ZINAVYOJITOKEZA KATIKA MSHALE WA MUNGU.....</b>	<b>47</b>
3.0 Utangulizi.....	47
3.1. Tafsiri ya methali zinazohusiana na wanyama .....	48
3.1.1 Methali na misemo inayohusiana na ndege .....	55
3.1.2 Methali na misemo inayohusiana na wadudu. ....	58
3.1.3 Methali na misemo inayohusiana na majira.....	59
3.1.4 Methali na misemo inayohusiana na mimea.....	60
3.1.5 Methali zinazohusiana na maumbile.....	63
3.2 Maswala Ibuka Kutokana na Tafsiri za Methali na Misemo Yenye Ushawishi wa Kiiolojia	64
<b>SURA YA NNE .....</b>	<b>67</b>
<b>TAFSIRI ZA METHALI NA MISEMO ILIYOSHA WISHIWA NA UTAMADUNI WA KIJAMII NA UTAMADUNI WA NYENZO KAMA ZINAVYOJITOKEZA KATIKA MSHALE WA MUNGU.....</b>	<b>67</b>
4.0 Utangulizi.....	67
4.1. Utamaduni wa Nyenzo.....	68
4.1.1 Methali na misemo inayohusiana na Vifaa vya kazi. ....	69
4.1.2 Methali na misemo inayohusiana na vyakula na vinywaji .....	73
4.2. Utamaduni wa kijamii.....	75
4.2.1 Methali na misemo inayohusiana na busara ya jamii .....	76
4.2.2 Methali na misemo inayohusiana na imani za kidini na za kishirikina .....	78
4.2.3 Methali na misemo inayohusiana na shughuli za kazi.....	82
4.2.4 Methali na misemo inayohusiana na desturi za kijamii .....	84
4.2.6 Asasi za Kijamii.....	86
4.3 Hitimisho.....	87

<b>SURA YA TANO .....</b>	<b>89</b>
<b>MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO .....</b>	<b>89</b>
5.0 Utangulizi.....	89
5.1 Matokeo .....	91
5.2 Mapendekezo .....	92
<b>MAREJELEO .....</b>	<b>93</b>

## UFAFANUZI WA ISTILAHU NA VIFUPISHO

Nafasi ya lugha:	Hadhi ya lugha ikilinganishwa na lugha nyingine katika mfumo fulani wa matumizi lugha kuliko na wingi lugha.
Utamaduni lengwa:	Utamaduni ambamo kazi inayotafsiriwa hukitwa na kujibainisha.
Maneno ya kitamaduni:	Maneno ambayo hueleweka katika utamaduni kwa sababu yamefungamana na utamaduni mahususi.
Wingimifumo:	Mfumo ulioundwa na mifumo mingi inayoingiliana na kuchangiana.
Kanuni za tafsiri:	Sheria zinazodhibiti tafsiri kwa mujibu wa Gideon Toury
LC:	Lugha Chanzi
LL:	Lugha Lengwa
MC:	Matini Chanzi
ML:	Matini Lengwa
TY:	Tafsiri Yetu
Utamaduni:	Jumla ya vitu au hali zinazoathiri maisha ya watu wa jamii fulani tangu kuzaliwa hadi kufa.
Methali:	Usemi mzito unaowasilisha ujumbe kwa njia ya fumbo. Katika tasnifu hii methali na misemo imeshughulikiwa kwa pamoja kwa hali ya kubadilishana nafasi kwa kuwa fani hizi huingiliana.
Uk:	Ukurasa
AOG:	Arrow Of God
MWM:	Mshale Wa Mungu.



## IKISIRI

Tafsiri za methali na misemo katika kazi za fasihi, hasa fani hizi zinapotokea kuwa na uamilifu wa kipekee katika kazi husika huhitaji kutafsiriwa kwa njia ambayo itafanikisha dhamira ya mwandishi kuhusiana na matumizi ya fani hizo. Mtafsiri huhitajika kutambua kuwa methali na misemo, mbali na jukumu la kupamba lugha ili kuifanya ivutie na kupitisha ujumbe maalum, wakati mwingine hutumika kama viungo vya kimsingi katika kuchimuza maudhui na kuisukuma mbele hadithi. Hali kama hii inajitokeza katika *Arrow of God* ambapo methali na misemo imetumika kufanikisha dhamira ya mwandishi, Chinua Achebe. Inabainika kwamba methali na misemo miongoni mwa vifani vingine vya fasihi simulizi ya watu wa jamii ya Igbo imetumiwa na Achebe ili kubadilisha lugha ya Kiingereza kuchukua sifa za kitamaduni za jamii ya Igbo. Katika tasnifu hii tafsiri za methali na misemo, kama zilivyofanywa na Hafid Shamte (1974), zimechunguzwa ili kutathmini mbinu alizotumia kutafsiri na kubainisha kama zinatimiza lengo la matumizi ya fani hizi katika *Arrow of God* baada ya kutafsiriwa kwa Kiswahili katika *Mshale wa Mungu*. Inabainika kuwa Shamte anatumia mbinu mbali mbali kutafsiri methali na misemo kutoka *Arrow of God* hadi *Mshale wa Mungu*. Miongoni mwa mbinu hizi, mbinu ya uhawilishaji inajitokeza kwa kiwango kikubwa. Matokeo ya tafsiri zinazotokana na mbinu hizi ni kwamba methali na misemo imejitokeza ama kama kama maelezo tu, au wakati mwingine vipengee vya utamaduni aliokusudia kuwasilisha Achebe vimepotea katika mchakato wa tafsiri. Hali hii inapelekea mapendekezo ya kufanya tafsiri kwa kutumia mbinu ambazo kwa kadri iwezekanavyo, zitadumisha sio tu mtindo wa methali, bali pia ujumbe wa mwandishi kwa njia inayosawazisha tamaduni mbili; utamaduni wa lugha chanzi na ule wa lugha lengwa.

## SURA YA KWANZA

### 1.1 Usuli wa mada

*Mshale wa Mungu* ni tafsiri ya riwaya ya Chinua Achebe iliyochapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 1964 kwa lugha ya Kiingereza ikijulikana kama *Arrow of God*, ambayo ilitolewa upya katika mwaka 1974. Katika riwaya hii mwandishi amejenga taswira ya maisha ya watu wa vijijini baada ya ujio wa Wazungu Afrika. Achebe anamtumia mhusika Ezeulu, kasisi wa mungu wa watu wa Umuaro anayeitwa Ulu, kuonyesha jinsi Waafrika walivyowapokea wazungu waliokuja Afrika kueneza dini ya kikristo na kutawala Waafrika kupitia kwa Watawala wa Wilaya. Ezeulu, kasisi wa Ulu, anatofautiana na watu wa vijiji sita ambao kwa pamoja walikuwa wamemtengeneza huyo mungu aitwaye Ulu na kukabidhi kijiji kimojawapo (Umuaro) ukasisi wa mungu huyo waliyemtengeneza. Ezeulu, ambaye anarithi ukasisi wa Ulu kutoka kwa babake, anatarajiwa kutumia mamlaka yake kama kasisi kuwaongoza watu wa vijiji vyote sita vya Umuaro katika shughuli muhimu katika maisha yao ya kila siku. Miongoni mwa majukumu ya Ezeulu, lipo jukumu la kutangaza siku na nyakati muhimu kama vile mwanzo wa msimu wa uvunaji wa viazi. Msimu wa kuvuna viazi, kwa kawaida ulitangazwa baada ya Ezeulu kula kiazzi cha mwisho miongoni mwa viazi kumi na viwili ambavyo aliwekewa katika ghala maalum. Kasisi huyu alihitajika kula kiazzi kimoja kutoka kwenye ghala hilo kila mwezi.

Ezeulu anatofautiana na baadhi ya watu wa vijiji vya Umuaro wanapomwona kuwa msaliti kwa kusema jambo analoliamini kuwa kweli kuhusu ardhi yenye mzozo kwa mtawala mzungu Winterbottom, ardhi ambapo waliishi yeye na watu wa Umuaro kwa jumla. Ezeulu anadai kuwa, sawa na alivyoambiwa na babake, ardhi hiyo ilikuwa ya watu wa kijiji cha Okperi; anashikilia kuwa madai hayo ni kweli kwa sababu mtu hasemi uongo kwa mwanawe. Winterbottom baadaye anatuma ujumbe kwa Ezeulu akiagiza Ezeulu aende katika makao makuu ya utawala wake (Okperi), kijiji kilicho mbali na Umuaro; jambo hili ni kinyume na baadhi ya taratibu, kaida na masharti ya ukasisi ambayo Ezeulu anatakiwa kuzingatia, kwa mfano, sharti kuwa kasisi wa Ulu asiende mbali na nyumba yake. Ezeulu anawataka ushauri watu wa vijiji vya Umuaro, wengi wao wanaliona hilo kama tatizo la kujitakia na kudai kuwa ni Ezeulu aliyefanya urafiki na mzungu, na hivyo wanaonekana kumtaka alitatu mwenyewe bila kuwataka ushauri. Ezeulu anawakasirikia watu hawa wa Umuaro na katika hali hii anapanga njama kulipiza kisasi.

Baada ya muda mfupi kasisi huyu anaondoka na kuenda Okperi, anakataa kuandamana na mtu yeyote ila mwanaye wa kiume Obika ambaye anampenda sana. Kisdafa anapofika Okperi anagundua kuwa Winterbottom anaugua sana kiasi kuwa hawezi kumuona kwa muda, badala ya Ezeulu kurudi Umuaro kutimiza majukumu yake ya ukasisi, anaamua kukaa Okperi kwa muda mrefu akingoja Winterbottom apone, hili linamfanya akose kutimiza majukumu na mahitaji ya ukasisi ya kula kiasi kimoja kila mwezi maana alikataa pendekezo la mmoja wa wake zake kuja kumpikia Okperi, vivyo hivyo anakataa pendekezo jingine la kuletewa chakula kutoka Umuaro. Wakati wa mavuno ya viazi unapofika, bado ana viazi vitatu ambavyo hajavila. Kulingana na masharti, hawezi kutangaza mwanzo wa msimu wa mavuno ya viazi kabla ale kiasi cha mwisho. Hali inatokea kuwa viazi mashambani viko tayari kwa mavuno, wakati huo huo akiba ya chakula kwenye maghala ya wanavijiji imeisha na watu wana njaa ila hawawezi kuvuna hadi kasisi atangaze mwanzo wa msimu wa uvunaji. Hali hii inasababisha matatizo mengi miongoni mwa watu wa vijiji vyote vya Umuaro kutokana na uhaba wa chakula, ilhali chakula kilikuwa tele mashambani. Wakiwa katika hali hii ya kukata tamaa, watu wa Umuaro, wanapokea habari kutoka kwa wenzao waliokuwa tayari wamekuwa wafuasi wa dini ya Kikristo ambayo ililetwa Umuaro na wazungu, ambapo Wakristo hawa wapya wanawapa ujumbe kuwa wanaweza kuvuna viazi wakati wowote na kutoa sadaka yao ya viazi kwa Mungu wa Wakristo badala ya Ulu ikiwa Ulu hawezi kupokea sadaka yao. Ezeulu anakataa katakata kusikia mashauri ya mtu yeyote aliyejaribu kumshauri kwa sababu ya kiburi na hatimaye watu wengi wanafuata dini ya Kikristo huku mwanawe anayempenda kwa ujasiri wake, Obika, akifa. Matukio haya yanaelekea kuwa kipigo kutoka kwa miungu kwa Ezeulu, kasisi mwenye kiburi.

Achebe anatumia lugha iliyo na wasifu wa kipekee katika riwaya ya *Arrow of God* kusimulia kisa hiki cha kuisimua. Anigbogu na Ahizih (2016), wanasema kuwa lugha ya Achebe katika *Arrow of God* inadhihirisha athari za kitamaduni za utamaduni wa watu wa Igbo, kwamba anatumia Kiingereza kueleza mambo ambayo ni ya kipekee kwa watu wa Igbo, mambo ambayo hutokea miongoni mwa Waigbo tu. Wakimnukuu Palmer (1979), wanasema kuwa wahusika wa Achebe ni wakazi wa vijijini ambao kwa kawaida wangezungumza kwa lugha ya Kiigbo lakini wanafanywa kuzungumza kwa Kiingereza japo Kiingereza hicho wanachokizungumza kimebadilishwa hivi kwamba kinadhihirisha maisha ya jamii ya vijijini na jinsi ambavyo watu hao hufikiria na vilevile kuzungumza.

Lugha hii yenye wasifu wa kipekee katika *Arrow of God* imesheheni methali na misemo mingi, kwa mujibu wa Lawal (2017), ina methali zaidi ya 130 katika kurasa takriban 238. Ukweli huu unachochea wasomi kujiuliza ni kwa nini mwandishi atumie methali na misemo kwa wingi kiasi hicho. Hata hivyo jibu la swali hili linaelekea kupatikana katika kujaribu kueleza umuhimu wa fani hizi—yaani matumizi ya methali na misemo. Abbas (2015), akinukuu Samover na wenzake (2009), anasema kuwa kwa maneno machache tu methali, hueleza amali na imani muhimu za watu wa utamaduni fulani kuhusu utamaduni wao, vilevile zinadhihirisha busara, mielekeo na hata imani za kishirikina za jamii husika. Meider (2004:3) naye anasema;

Methali huwakilisha historia na utamaduni, kipengele muhimu sana cha rangi ya taifa. Jukumu la methali ni jukumu la kitamaduni la kiuuelekezi kwa kuwa methali ina busara, ukweli, maadiliko na mitazamo ya kitamaduni. (TY)

Kulingana na Meider, na Abbas, upo uhusiano wa karibu sana kati ya misemo na methali na utamaduni wa jamii yoyote ile, ni sawa na kusema kuwa methali na misemo ni chombo muhimu katika kubeba historia na utamaduni wa jamii maalum, na kuupitisha utamaduni huo kwa vizazi vya baadaye. Utamaduni huu, anavyosema Abbas, unadhihirika katika amali na imani za watu wa jamii fulani. Miongoni mwa imani hizi kuna; imani za kidini, na pia imani za kishirikina. Methali na misemo vile vile hutumika katika takriban nyanja zote za maisha ya jamii yoyote ile, sifa ambayo inafanikisha jukumu la methali la uelekezi analolitaja Meider.

Methali na misemo ni muhimu sana kama yanavyodhihirisha maoni ya Meider na Abbas, ila mbali na kuelekeza na kubeba utamaduni wa jamii, methali na misemo ilivyotumika katika *Arrow Of God* inadhihirisha jukumu jingine muhimu sana katika fasihi. Lawal (2017), anaeleza kuwa methali zimetumika kiubunifu katika *Arrow of God* kuwezesha kuisukuma mbele hadithi na zaidi, kukifanya Kiingereza kilichotumika kuafikiana na miundo na mifumo ya utambaji hadithi katika miktadha ya Kiafrika, na hasa Kiigbo. Pamoja na hayo, methali hizo zimetumika kuweka kipaumbele na kuchimuza maudhui na dhamira za kimsingi katika riwaya hii yaani, usambaratikaji wa jamii ya Kiigbo kutokana na majilio ya wazungu ama majilio ya tamaduni ngeni hususan Ukristo.

Kuhusu misemo, yapo maoni kuwa methali na misemo ni fani zenye uhusiano wa karibu na huweza kuingiliana mara kwa mara, ingawa ni fani tofauti. Abbas (2015), anaeleza kuwa methali huwa na majina tofauti tofauti, wakati mwingine methali huitwa misemo. Hata hivyo huwa

zimebeba tajriba na ujuzi wa utamaduni fulani uliokusanywa kwa muda mrefu. Maoni haya ya Abbas yanaelekea kuonyesha kuwa misemo ni jina jingine linalotumika kurejelea methali. Mwelekeo wa Abbas utafaa sana utafiti huu, hata kama kuna tofauti baina ya methali na misemo, tofauti hizo hazitapewa kipaumbele katika utafiti huu kwa kuwa ulinganifu baina ya fani hizi na mwingiliano wao ni muhimu zaidi kwa utafiti huu. Fani hizi zitashughulikiwa kwa mkumbo mmoja.

Achebe anafanikisha jukumu la methali la kuubeba utamaduni wa Kiigbo katika *Arrow of God* kwa njia yenye mvuto na hivyo kuupitisha ujumbe kwa wasomaji kwa namna kwamba hawachoshwi na kazi yenyewe na wanaweza kuukumbuka ujumbe huo kwa muda mrefu. Kwa kuwa methali na misemo hupitisha busara ya jamii kwa njia rahisi isiyosahaulika kwa urahisi, kazi ya fasihi inapotafsiriwa, ipo haja ya kutafsiri methali na misemo kwa makini ili kutimiza jukumu hili muhimu. Baadhi ya jamii huwa na utajiri wa misemo na methali, fani ambazo zinadhihirisha utajiri katika ujuzi na busara ya jamii hiyo. Kazi ya fasihi inapoandikwa katika misingi ya tamaduni hizi huwa ni kazi iliyo na manufaa makuu kwa wasomaji wake. Kazi yenye sifa hizi inapotafsiriwa, hadhira yake hupanuka na ujuzi uliomo huwafikia watu wengi na kuwanufaisha. Riwaya ya *Arrow of God*, ni mojawapo ya kazi zenye utajiri huu wa kitamaduni kwa kuwa ni kazi ambayo imesheheni maadili, amali, imani na busara ya jamii ya Waigbo. Kwa sababu hii, ipo haja ya tafsiri bora, hata hivyo tafsiri ya methali hujitokeza kuwa swala changamano na telezi.

Baadhi ya watafiti ambao wamefanya uhakiki wa kazi za fasihi zilizotafsiriwa wamekubaliana kuwa kuna changamoto mbalimbali katika tafsiri za kazi za fasihi, na kutokana na changamoto hizi tafsiri zilizojitokeza zina matatizo. Zaja (1986), akitumia riwaya iliyotafsiriwa ya *Wema Hawajazaliwa* ameonyesha kuwa, japo tafsiri ni muhimu sana katika ukuaji wa fasihi ya Kiswahili, wakati mwingine tafsiri zinazofanywa huwa na makosa mbalimbali ambayo yanaishia kudhoofisha ujumbe ambao mwandishi alikusudia kuwapa wasomaji wake. Mutie (1997:4), anatoa wito kwa watafsiri kuboresha tafsiri ya fasihi ili wasomaji wapate ujumbe aliokusudia mwandishi wa MC kwa njia aliyokusudia huyo mwandishi. Anasema;

Ingawa watafsiri hujitahidi kuepuka matatizo mengi yanayokumba tafsiri, dosari kama vile upotoshi wa maana, sarufi ya lugha pokezi na udhaifu wa fasihi ya lugha hujitokeza kila mara katika fasihi tafsiri. Haya husababisha tafsiri kuwa za kiwango cha chini, hali ambayo inaweza

kurekebisha ili kuziboresha kazi hizo zaidi. Kuboreshwa kwa kazi tafsiri kwa kuzitathmini, kuzikosa na kuzichanganua kutazuia tafsiri duni. Tafsiri huwa na jukumu la kuwasilisha ujumbe wa mtu mwingine kwa hadhira inayotumia lugha tofauti na ile iliyotumiwa na mwandishi asilia. Kazi nyingi nzuri za kifasihi kutoka tamaduni nyingine za ulimwengu zimefika katika Kiswahili zikiwa zimefinywa na kupotoshwa kifani, kimaudhui na kimaana. Sanaa ya kazi yoyote huathirika pale tu, fani inapoathirika.

Matatizo ya tafsiri hutokana na uchangamano wa mchakato mzima wa tafsiri. Kijumla, tafsiri imefafanuliwa kama uhawilishaji wa maana kutoka kwa lugha chanzi hadi kwa lugha lengwa. Uhawilishaji huu huweza kuonekana kuwa sahili kabla ya mtu kuingia katika shughuli yenyewe ya kutafsiri, hata hivyo imedhihirika kuwa kazi ya kutafsiri humpa changamoto mtafsiri katika azma yake ya kuhawilisha maana kutoka kwa MC hadi kwa ML. Newmark (1988:5) anasema kuwa tafsiri;

...ni kutoa maana ya matini katika lugha moja hadi lugha nyingine kwa njia ambayo mwandishi alikusudia matini hiyo,...hili linafaa kuwa jambo rahisi, kwa sababu mtu anafaa kuwa na uwezo wa kusema jambo kwa ufasaha katika lugha moja sawa na katika lugha nyingine. Kwa upande mwingine unaweza kuona hili kuwa changamano, jambo lisilo la kiasilia na la wizi, kwani... unajifanya kuwa mtu usiye. TY

Kama wanavyoeleza wataalamu mbalimbali, uchangamano wa mchakato wa tafsiri unatokana na tofauti nyingi zilizo katika lugha tofauti. Tofauti hizi zinajitokeza katika viwango vyote vya lugha, yaani katika mofolojia, fonolojia na semantiki. Tofauti hizi za lugha pia hujitokeza katika tamaduni zinazofungamana na kila lugha. Baadhi ya wataalamu vilevile wanaelekea kukubaliana kuwa miongoni mwa vipengee vya lugha ambavyo vinampa changamoto kubwa mtafsiri, ni methali na misemo, hali hii inatokana na sifa za misemo na methali, kuwa ni viwakilishi vya utamaduni wa jamii ambamo vimezaliwa anavyosema Meider (2004:3), anasema;

Methali huwakilisha historia na utamaduni, kipengee muhimu sana cha rangi ya taifa... huwa ina busara, ukweli, maadili na mitazamo ya kitamaduni. (TY)

Kila jamii lugha ulimwenguni huwa na utamaduni wake ambao unatofautiana na tamaduni za jamii lugha nyingine kwa kiasi fulani. Upo uwezekano wa baadhi ya tamaduni za jamii lugha tofauti

kulingana, hata hivyo, hakuna jamii lugha mbili zilizo na tamaduni na mitazamo ya maisha inayolingana asilimia mia moja. Kutokana na ufahamu huu, ni sahihi kusema kuwa mtafsiri anapotafsiri methali na semi anakabiliwa na jukumu la kutafsiri sio tu lugha bali utamaduni uliofungamana na methali na misemo hiyo. Ikizingatiwa kuwa tamaduni zinatofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine, inamwia vigumu mtafsiri kupata ulinganifu wa methali na misemo unaodumisha upekee wa kitamaduni na wakati huo huo kudumisha upekee wa mtindo kwa mujibu wa vipengee hivi.

Changamoto nyingine inayomkumba mtafsiri wakati ambapo anatafsiri methali na misemo, inatokana na sifa nyingine ya methali na misemo. Sifa hii ni kuwa misemo na methali ni kauli zisizobadilika. Kulingana na Ghazala (1995:13), “Methali ni vipashio vya kipekee visivyobadilika na ambavyo vina maana zisizobadilika.”(TY) Sifa hii ya methali na semi ya kutobadilika inamfanya mtafsiri kuwa katika hali ya mtanziko wakati wa kutafsiri, mtafsiri huyu anajikuta katika hali inayomtaka atoe, ama tafsiri itakayompa nafasi kufafanua maana inayoeleza utamaduni uliofichama ndani ya semi hizi, au atoe tafsiri ya moja kwa moja itakayodumisha muundo na maneno ya semi zenyewe, mbinu ambayo huenda ikasababisha tafsiri isiwasilishe ujumbe kwa lugha lengwa (LL) jinsi ulivyokusudiwa na mwandishi wa matini katika lugha chanzi (LC).

Wakati mwingine methali katika lugha moja huweza kuwa na methali nyingine zinazolingana kimaana na methali katika lugha nyingine, hata hivyo, ingawa kuna uwezekano wa ulinganifu wa lugha iliyotumika katika methali kuwepo, huwa kuna tofauti za uelewa katika misingi ya tofauti za tamaduni; kwa sababu hii pia, mtafsiri anajikuta katika hali tatizi. Kwa kuzingatia hali hizi changamano ambamo anajikuta mtafsiri wa fasihi ya Kiswahili mara kwa mara, ni wazi kuwa mtafsiri huyu analazimika kuchukua mkondo anaouona kuwa mwafaka zaidi kwa wakati huo na kwa kazi hiyo. Mtazamo wake unaweza kuwa tofauti na mitazamo ya wengine na kwa sababu hii walio na maoni tofauti humkosoa na kudai kuwa tafsiri hiyo ni chapwa. Kwa upande mwingine inawezekana mtafsiri afanye makosa katika kutafsiri kwake na kupotosha ujumbe wa mwandishi au kudhoofisha kazi, hata hivyo, ni jambo la busara kutambua kuwa, ingawa kuna makosa mbalimbali yanayojitokeza katika kazi za fasihi zilizotafsiriwa, kazi hizo zilivyo, zina mchango wake katika ukuaji wa fasihi ya Kiswahili. Sawa na anavyosema Mule (2002), akimrejelea (Zaja 2002), ipo haja ya kuchukua mtazamo mwingine katika utafiti wa tafsiri za fasihi ya Kiswahili, mbali na kujishugulisha kupita kiasi na kukosoa tu watafsiri. Utafiti huu umelenga kutalii tafsiri

ya methali na misemo iliyofanywa na Shamte, kutoka *Arrow of God* hadi *Mshale wa Mungu* ili kuchunguza namna tafsiri hiyo ilifanywa na umuhimu wa tafsiri hiyo katika ukuaji wa fasihi ya Kiswahili.

## **1.2 Tatizo la utafiti**

Utafiti huu ulilenga kuangazia ushawishi wa utamaduni katika tafsiri za kifasihi ikizingatiwa kuwa kuna msambao mkubwa wa matumizi ya methali na misemo katika tungo nyingi za fasihi. Tafsiri za kazi ambazo husheheni methali na misemo mingi na hasa pale ambapo methali hizo zinapokuwa sehemu na wasifu wa kimsingi wa kifani, hukumbana na changamoto nyingi katika miktadha ya kutafsiri, hali ambayo kwa kiasi kikubwa inahusiana na ukweli kwamba tafsiri za methali na misemo ni tafsiri zinazohusu usawazishaji wa mivutano ya kiutamaduni, ikizingatiwa kwamba methali na misemo takriban wakati wote ni mazao ya tamaduni mahususi na kwa hivyo katika kuihari kutafiti msambao wa changamoto zinazojitokeza katika tafsiri za methali hasa methali hizo zinapokuwa sehemu na wasifu wa kimsingi wa kazi ya kiutunzi; na vile vile kuihari kushughulikia kipengele kimoja katika kazi moja patanifu, utafiti huu unatambua kwamba kuna uwezekano wa kuifanyia kazi iliyotafsiriwa “uchanganuzi wa kiuteuzi” (partial analysis) ili kuweza kukishughulikia kipengele kilichoteuliwa kwa undani na kwa ustadi. Ili kuweza kukishughulikia kipengele hiki, utafiti huu umehiari kuchanganua tafsiri za methali na misemo kadri inavyojitokeza katika kazi ya Chinua Achebe *Arrow of God* na kutathmini ulinganifu pamoja na utoshelevu wake katika tafsiri yake ya Kiswahili *Mshale wa Mungu*. Utafiti huu unalenga kuhoji tangu mapema kwamba changamoto za kusawazisha mivutano ya kiutamaduni inayojibainisha katika tafsiri ya methali na misemo, zinahusiana na tofauti za kitamaduni zinazoshawishi kubuniwa na kutungwa kwa methali na misemo katika jamii mahususi. Haya ni mambo ambayo yana athari katika kazi za aina mbalimbali katika usomaji na ufasiri wa matini lengwa.

## **1.3 Maswali ya utafiti.**

- a) Je, ni maswala yapi yanayopelekea methali na misemo kutafsiriwa kwa njia ya ufafanuzi jinsi inavyojitokeza katika *Mshale wa Mungu*?
- b) Methali na misemo kutoka kwa lugha chanzi, inachukua nafasi gani katika fasihi ya Kiswahili?
- c) Mtafsiri anaweza kutumia mbinu zipi ili kusawazisha mivutano ya kitamaduni katika tafsiri?



d) Tafsiri ya methali na misemo ina mchango gani katika ukuaji wa fasihi ya LL?

#### **1.4 Malengo Ya Utafiti**

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza tafsiri ya methali na misemo kama viwakilishi vikuu vya utamaduni wa jamii yoyote ile hasa vinapokuwa kiungo muhimu cha kifani katika kazi ya fasihi. Katika kutimiza lengo hili kuu malengo mahususi yanayotarajiwa kuafikiwa kwanza ni pamoja na:

- a. Kuchunguza jinsi vipengee mbalimbali vya kitamaduni katika matini chanzi ya *Arrow Of God* vinajitokeza katika matini lengwa ya *Mshale wa Mungu* kupitia kwa tafsiri ya methali na misemo.
- b. Kutoa tathmini ya mbinu na mikakati ya tafsiri iliyotumiwa katika kutafsiri methali na misemo kutoka matini chanzi ya Kiingereza ya *Arrow Of God* hadi katika matini lengwa ya Kiswahili *Mshale wa Mungu*.
- c. Kutathmini mchango wa methali na misemo tafsiri katika ukuaji wa fasihi ya Kiswahili.
- d. Kupendekeza njia za kukabiliana na changamoto zinazotokana na tofauti za kitamaduni katika tafsiri.

#### **1.5 Sababu za kuchagua mada hii**

Tulihiari kushughulikia mada hii kwa sababu kadha za kimsingi, sababu hizi zina uhusiano wa karibu na upekee wa matumizi ya methali na misemo katika riwaya ya *Arrow of God*. Sababu mojawapo ni kwamba, watafiti waliotangulia kushughulikia tafsiri ya fani katika kazi za fasihi, wamechukua mwelekeo wa uchunguzi wa tafsiri ya fani katika fasihi katika ujumla wake. Wataalamu hawa kwa hakika wametoa maelezo muhimu kuhusiana na mada hii, hata hivyo, mwelekeo wao wa kushughulikia vipengee vingi vya fani katika mkumbo mmoja humnyima mtafiti nafasi ya kutosha ya kufanya utafiti kwa kina cha kutosha na hivyo kutoa maelezo ya kijumla, ilhali kazi hizo huenda zikahitaji maelezo ya kina. Hali hii hujitokeza pale kipengee fulani cha fani kina uamilifu wa kipekee kama zilivyo methali na misemo katika riwaya ya *Arrow of God*. Uamilifu wa kuendeleza dhamira ya mwandishi kwenye riwaya. Dhamira ya mwandishi ambayo ni kudhihirisha mchango wa utamaduni wa Kiafrika katika upokeaji wa Wazungu barani Afrika kabla ya Ukoloni. Dhamira hii inafanikishwa kupitia kwa njia mbalimbali zikiwemo: usawiri wa wahusika, usimulizi, maudhui na vipengee vingine vya riwaya. Methali na misemo

imechangia kwa kiwango kikubwa katika kufanikisha vipengee hivi na jukumu hili linachangia haja ya kuchunguza kipengee hiki muhimu katika riwaya ya *Arrow of God*.

Jambo lingine ni kwamba, riwaya ya *Arrow of God* ina usimulizi wa kipekee unaofanikishwa na methali na misemo, kwa maana kwamba japo usimulizi huo umejibainisha kwa lugha ya Kiingereza lugha hiyo imesheheni asilimia kubwa ya Uafrika hasa utamaduni wa Kiigbo. Wahusika wa vijijini wanazungumza kwa lugha ambayo, japo ni Kiingereza, mtindo wake unadhihirisha mawazo ya watu wa vijijini na kwa jumla matukio ya vijijini moja kwa moja kama tulivyotangulia kutaja. Ni usimulizi unaodhihirisha kwa uwazi mkubwa utamaduni wa Kiigbo katika kipindi muhimu cha kihistoria; wakati ambapo utamaduni huu unayumbishwa na athari ya utamaduni wa mataifa ya Ulaya, hususan Ukristo na mifumo ya kiutawala ya kimagharibi. Achebe anafaulisha usimulizi wa matukio katika kipindi baada ya majilio ya wazungu kwa namna ambayo inabainisha maudhui makuu katika kazi yake ambayo ni utamaduni, kwa kutumia fani ya methali na misemo. Fani hizi hutumia maneno machache kueleza busara, utamaduni na amali za jamii zinamotoka kwa hivyo zimewezesha usimulizi huu kwa kiwango kikubwa. Hali hii inapelekea matumizi ya kipekee ya methali na misemo, upekee huu unahitaji kudhihirika katika tafsiri ya riwaya hii, la sivyo, ujumbe aliokusudia kuupitisha mwandishi utapotoshwa au kudhoofishwa, au yote mawili.

Mbali na uamilifu wa methali na misemo, wingi pamoja na msambao wa matumizi ya fani hii katika riwaya ya *Arrow of God* umechochea utafiti huu. Ikilinganishwa na fani nyingine zinazojitokeza katika riwaya hii, methali na misemo inajitokeza kwa wingi zaidi katika riwaya ya *Arrow of God*. Katika riwaya nzima ya kurasa takriban mia mbili thelathini na nne, kuna methali na misemo zaidi ya mia moja thelathini. Wingi huu wa fani hii unachochea utafiti huu kwa kuwa, katika kutafsiri riwaya kama *Arrow of God* yenye methali na misemo mingi kiasi hiki, hapana shaka kwamba mtafsiri atachukua sehemu kubwa ya muda wake aliotengea tafsiri ya kazi hiyo kutafsiri methali na misemo na matokeo ya tafsiri hiyo yatakuwa na sehemu kubwa inayotokana na methali na misemo, hivyo ni muhimu kushughulikia swala hili la tafsiri ili kuhakikisha kuwa matini za aina hii zimefanyiwa tafsiri mwafaka. Ikumbukwe kuwa *Mshale wa Mungu* ni riwaya tafsiri inayotumika katika utafiti huu kama kielelezo tu cha riwaya zilizotafsiriwa kutoka Kiingereza hadi Kiswahili ambazo zimesheheni matumizi mengi ya misemo na methali. Matokeo

ya utafiti huu yatafaa watafiti wa tafsiri ya fasihi ya Kiswahili katika uchanganuzi wa kipengee kimoja cha fani hasa kipengee hicho kinapochukua nafasi ya kimsingi katika kazi ya fasihi.

### **1.6 Upeo na Mipaka**

Katika utafiti huu, tumetathmini namna ambavyo Hafid M. Shamte alitafsiri methali na misemo katika riwaya ya Chinua Achebe iliyoandikwa kwa Kiingereza kama *Arrow of God*, hadi matini lengwa ya Kiswahili *Mshale wa Mungu*. Tulivyotangulia kutaja, japo Achebe aliandika riwaya ya *Arrow of God* kwa lugha ya Kiingereza, riwaya hii inadhihirisha matukio katika jamii ya watu wa Igbo, kwa hivyo ‘Kiingereza’ alichokiandikia Achebe, kimesheheheni sifa za Ki-Igbo. Hivyo basi ni muhimu kutambua kuwa methali na misemo inayojitokeza katika riwaya ya Achebe si methali na misemo ya Kiingereza bali ni methali na misemo ya Ki-Igbo ambayo Achebe alitafsiri kwa Kiingereza. Mara kwa mara, tulirejelea utamaduni wa Ki-igbo katika jaribio la kuelewa maana za methali na misemo katika *Arrow of God* ili kutuwezesha kuhakiki tafsiri zilizotolewa na Shamte kwa methali na misemo hiyo.

Maudhui yanayojitokeza zaidi katika *Arrow of God*, yanahusu au yanaangazia utamaduni wa Ki-Igbo hasa unavyoingiliwa na utamaduni wa kidini wa Ulaya katika kipindi na awamu mahususi ya kihistoria. Utafiti huu ulichunguza jinsi tafsiri za methali na misemo zilivyoathiri ujitokezaji wa maudhui haya ya kimsingi katika *Mshale wa Mungu*. Ujitokezaji huo wa kimaudhui ulichunguzwa kwa kushughulikia methali na misemo kwa kuzingatia jinsi zinavyotokana au zinavyoshawishiwa na viungo mbalimbali vya utamaduni. Katika uchunguzi huo tulishughulikia namna Shamte amekabiliana na changamoto ya tofauti za kitamaduni baina ya utamaduni wa Ki-Igbo katika *Arrow of God*, na utamaduni wa Kiswahili katika *Mshale wa Mungu*. Ni kweli kuwa, sawa na fasihi yoyote ile, riwaya ya *Arrow of God*, imesheheni maudhui mengine tofauti na haya tuliyoyashughulikia, vilevile inadhihirisha mbinu nyingine za lugha tofauti na methali na misemo, hata hivyo utafiti huu ulijifunga katika kuchunguza tafsiri za methali na misemo na maudhui ya usambaratikaji wa utamaduni wa Ki-Igbo baada ya kuingiliwa na utamaduni wa ki-Kristo bila kujishughulisha na fani nyingine wala maudhui mengine.

Yapo maswala anuwai yanayohusiana na tafsiri ya kazi za fasihi ambayo yalijitokeza katika mchakato mzima wa utafiti huu, hata hivyo, jukumu la utafiti huu lilikuwa kutoa jaribio katika kudhihirisha umuhimu wa kuchunguza tafsiri ya kipengee kimoja kikuu cha fani katika kazi ya fasihi kwa undani hasa fani hiyo inapokuwa kiungo muhimu katika kutimiza dhamira ya

mwandishi kama zilivyo methali na misemo katika *Arrow of God*. Hivi ni kusema kuwa maswala mengine yote ya tafsiri yalikuwa yamefungiwa nje ya utafiti huu na hayakushughulikiwa ila kwa kiwango kilichofaa utafiti huu.

### **1.7 Yaliyoandikwa kuhusiana na mada hii**

Tafsiri ya methali na misemo kadri zinavyojitokeza katika tungo za kifasihi au katika matumizi ya kawaida ya lugha, ni mada ambayo imeshughulikiwa na watafiti mbali mbali. Watafiti hawa wameshughulikia mada hii kadri ilivyoshughulikiwa katika baadhi ya fasihi na lugha kama vile Kiingereza, Kiajemi, Kichina na Kiarabu. Katika tafiti hizo, wameshughulikia jinsi ya kufanya tafsiri ya methali na misemo kwa kutumia mbinu anuwai na kutoa mapendekezo mbali mbali. Newmark (1988) anadai kwamba kuna tofauti kati ya taratibu za kutafsiri na mbinu za tafsiri. Anaeleza kuwa taratibu za kutafsiri hutumika wakati wa kutafsiri sentensi na vipashio vidogo kuliko sentensi ilhali mbinu za tafsiri zinazohusika na kutafsiri matini nzima. Anapendekeza taratibu zifuatazo za kutafsiri methali;

- a) Uhawilishaji, ambao kimsingi ni sawa na ukopaji
- b) Utohozi ambao kimsingi ni kubadilisha neno katika LC kuchukua sifa za kimofolojia za LL na hivyo kutamkwa kama lugha lengwa,
- c) Kuweka neno la kitamaduni katika LL katika nafasi ya neno la kitamaduni katika LC. Mbinu hii ni sawa na kutumia tamathali katika LL inayofanana kimaana na LC lakini yenye kutofautiana kimuundo,
- d) Maana ya kiuamilifu ambapo mtafsiri anatumia neno lisilofungamana na utamaduni kutoa maana iliyokusudiwa,
- e) Maana elezi au maana fafanuzi ambapo mtafsiri hutoa maelezo linganifu kwa maneno tofauti kubainisha maana. Mbinu hii ni sawa na ya kutoa maelezo,
- f) Tafsiri inayotambulika ambapo mtafsiri hutumia neno linalokubalika zaidi katika kutafsiri,
- g) Tanbihi, viziada na maelezo mafupi: hii inahusisha kuongeza ujumbe wa ziada unaohitajika katika maneno ya kitamaduni, maneno ya kitaaluma na yale ya lugha,
- h) Muungano wa mbinu mbili, muungano wa mbinu tatu na muungano wa mbinu nne (TY) hii hutokea pale mtafsiri anatumia mbinu mbili tatu au nne kwa pamoja.

Mapendekezo haya ya Newmark yanalenga tafsiri ya methali na misemo, sawa na lengo la utafiti huu, hata hivyo Newmark anapendekeza mbinu za kutafsiri methali na misemo katika ujumla

wake, pale fani hii imetumika katika hali za kawaida, na wakati zinatumiwa katika kutimiza jukumu la kupitisha utamaduni. Katika utafiti huu, uchunguzi wa tafsiri ya methali na misemo ulilenga hali ambapo methali na misemo imetumika kama sehemu ya fani katika kuchimuza maudhui na dhamira, kusawiri wahusika na kudhihirisha utamaduni wa jamii fulani katika kazi ya fasihi. Baadhi ya mapendekezo ya Newmark yalikuwa ya manufaa makubwa katika kufaulisha utafiti huu kwa kuwa tuliyatumia kutathmini tafsiri ya methali na misemo iliyofanywa na Shamte kutoka matini chanzi *Arrow of God* hadi kwenye matini lengwa *Mshale wa Mungu*.

Baker (1992) akitumia mifano ya kutafsiri tamathali za usemi kutoka lugha ya Kichina anapendekeza mbinu ambazo zinaweza kuwa za manufaa kwa watafsiri wa methali. Mbinu hizi ni pamoja na;

- a) Kutumia tamathali yenye maana na muundo linganifu ambapo mtafsiri anatumia tamathali katika LL ambayo ina maana na maneno linganifu na LC.
- b) Kutumia tamathali yenye maana sawa ingawa inaweza kuwa na muundo tofauti, yaani maneno tofauti.
- c) Tafsiri kwa njia ya maelezo na anapendekeza kuwa mbinu hii itumike wakati ambapo hakuna tamathali katika LL ambayo inalingana na tamathali katika LC
- d) Tafsiri kwa udondoshaji ambapo mtafsiri anadondosha tamathali kabisa, mtafsiri anajaribu kutoa maelezo ya maana ya tamathali kwa ulinganifu wa karibu iwezekanavyo.

Kuhusiana na swala hili la ulinganifu wa methali kama anavyopendekeza Baker, Vinay na Darbelnet (1995) waliamini kuwa methali linganifu katika lugha lengwa zinafaa kudhihirisha hali sawa na hali asilia kwa kutumia maneno tofauti. Huu mtindo wao unaweza kutumika kuleta athari ya kimtindo ya LC katika LL. Kulingana na wanavyosema, kutumia kisawe ndio mbinu mwafaka zaidi ya mtafsiri kutumia wakati anatafsiri methali na tamathali. Wasomi hawa walipendekeza mbinu hizi kwa fani nyingi. Tofauti na kauli pamoja na mijadala iliyoibuliwa na watafiti hawa, utafiti huu ulijifunga katika kutathmini ufaafu na utoshelevu wa tafsiri za methali na misemo kwa kadri zilivyohawilishwa kutoka lugha na utamaduni mmoja hadi lugha na utamaduni mwingine kwa kutambua kwamba ufanifu wa kutafsiri methali na misemo huwa na athari chanya kwa kazi nzima inayotafsiriwa. Mapendekezo yao yalifaa katika kutathmini iwapo mbinu wanazopendekeza

zilitumika katika kutafsiri methali na misemo katika tafsiri aliyofanya Shamte, na kuchunguza ufaafu wa mbinu hii ikilinganishwa na mbinu nyingine.

Mollanazar (2001) amechangia katika mada hii ya tafsiri ya methali, ambapo katika kazi yake, anapendekeza mbinu mbili za kutafsiri methali; kwanza ni kutumia methali zinazofanana katika maana na pia katika muundo, njia ya pili anayopendekeza ni kutumia methali zenye maana sawa katika muktadha husika ingawa zina tofauti za kimuundo. Mapendekezo haya yalitufaa katika utafiti huu japo kwa kiwango kidogo kwa kuwa si kila methali inaweza kuwa na methali inayolingana kwa njia anazopendekeza Mollanazar katika lugha ambayo mtafsiri atahitajika kutafsiria. Vile vile Mollanazar alishughulikia methali katika matumizi ya kawaida ya lugha ya kimazungumzo, jambo ambalo ni tofauti na kushughulikia methali katika miktadha ya kiubunifu katika kazi mahususi ya kifasihi tulivyofanya.

Gaber (2005), naye anapendekeza mbinu kadhaa za kutafsiri usemi uliofungamana na utamaduni. Mbinu hizi ni pamoja na hizi zifuatazo; ulinganifu wa kitamaduni ambapo maneno yaliyofungamana na utamaduni yanaweza kutafsiriwa hadi LL kwa kutumia maneno katika lugha lengwa yaliyofungamana na utamaduni wa LL. Pili alipendekeza mbinu ya kutafsiri kiuamilifu ambapo katika mbinu hii mtafsiri hutumia neno au kundi la maneno katika LL ambalo lina uamilifu sawa wa neno au kundi la maneno katika LC. Mbinu ya tatu, ni maelezo au ufafanuzi ambapo mtafsiri hufafanua maana ya neno la LC. Nne, maelezo mafupi ambayo ni mbinu ya kutoa maelezo ya ziada kama tanbihi kufafanua kilichotafsiriwa. Tano, ukopaji ambapo neno katika lugha chanzi linakuwa sehemu ya lugha katika LL. Pamoja na kwamba mbinu zinazopendekezwa na Gaber ni muhimu, mbinu hizi ni mbinu za tahadhari kwa maana kwamba zinashauri na kuelekeza mambo yafaayo kufanywa kabla ya kutafsiri, lakini katika utafiti huu kilichongaziwa ni matokeo, yaani kazi ambayo tayari imetafsiriwa. Kwa hivyo ufahamu wa mapendekezo haya una maana kwamba yalitumiwa kama mfumo wa marejeleo katika kutathmini matokeo ya kutafsiriwa kwa kazi ya kifasihi.

Duff (katika Gorjian, 2006) anadokeza kuwa mtafsiri anaweza kutafuta ulinganifu wa tamathali baina ya LC na LL kama ifuatavyo;

- a. Kuibua tafsiri ya moja kwa moja,
- b. Kutumia neno halisi katika alama za mtajo,

- c. Kutumia methali linganifu,
- d. Kutumia tafsiri isiyo ya kitamathali.

Hatimaye, kwa msisitizo anasema kuwa iwapo hakuna methali inayolingana na nyingine kati ya LC na LL mtafsiri asilazimishe methali hiyo isiyolingana kwa tafsiri. Sawa na kazi ya Duff, utafiti huu ulilenga tafsiri za methali na misemo, ila Duff alishughulikia methali na misemo katika mazingira ya kawaida ilhali katika utafiti huu uchanganuzi wa methali na jinsi zilivyotafsiriwa kifasihi ulifanywa kwa kukitwa katika miktadha ya kibunilizi, kwa kuangazia usanifu wa methali na misemo husika, na kwa kuangazia mivutano ya kiutamaduni inayoibushwa na methali wakati zinapohusishwa na upekee wa matumizi katika kazi maalum.

Farahani na Ghasemi (2012), walitathmini kiwango ambacho mbinu mbalimbali za tafsiri za methali zilitumika katika kutafsiri methali kutoka Kiingereza hadi Kiajemi, katika utafiti wao walitumia tafsiri za methali ya Kiingereza hadi katika lugha ya Kiajemi. Waligundua kuwa mbinu ya kutafsiri methali kwa methali nyingine ilitumika ama ingewezekana kwa kiasi kikubwa zaidi, ikifuatwa na mbinu ya kutaja moja kwa moja maana katika mifumo isiyo ya kifani, na kwa mara chache zaidi maneno yaliyofuata kuchukuliwa kama maana ya methali hiyo. Kupitia utafiti huu walidhihirisha kuwa methali zingetafsiriwa kwa lugha ya kitamathali au kwa lugha ya kawaida. Mwelekeo wa Farahani na Ghasemi ni wa kitathmini sawa na wa utafiti huu, wanavyodhihirisha mbinu ya kutafsiri methali kwa methali nyingine ilitumiwa kwa kiwango cha juu zaidi ikilinganishwa na mbinu nyingine. Hali hii inawezekana tu pale ambapo kuna ulinganifu wa methali na misemo baina ya LC na LL. Utafiti huu ulijikita katika kubainisha kiasi cha utoshelevu wa mbinu za tafsiri zilizotumiwa na athari ya mbinu zilizotumiwa katika kuhawilisha maudhui ya utamaduni alivyokusudia mwandishi katika LC inapotokea kuwa ulinganifu wa methali katika LC na LL upo ama haupo.

Tofauti na watangulizi wao, Al-Shawi na Mahadi (2012) walichunguza mbinu ambazo zingesaidia katika kutatua matatizo ya kutafsiri mtindo wa lugha matumizi kutoka Kiingereza hadi Kiarabu na kutoka Kiarabu hadi Kiingereza. Wasomi hawa walitumia mifano ya tamathali katika matangazo ya televisheni, redio, na filamu, mazungumzo ya watu ya kila siku, walitumia vilevile data kutoka kwa maandishi kama magazeti majarida, riwaya vitabu vingine na makamusi ambapo walichanganua data iliyokusanywa ili kutambua matatizo ya kutafsiri na kupendekeza mbinu za

kukabiliana na changamoto hizo. Walidhihirisha kutokana na utafiti huu kuwa zipo mbinu nyingi za kutafsiri tamathali hizi kama vile kutumia tamathali sawia au linganifu katika LL ambazo ina maana sawa katika LC na LL; Kutumia tamathali zisizofanana kimuundo lakini zinazolingana kimaana; kufafanua tamathali; kutoa maelezo mafupi kuhusu tamathali. Methali na misemo hujumuishwa katika lugha ya kimtindo waliyoshughulikia watafiti hawa, ila utafiti huu ulishughulikia kipengee kimoja ambacho ni methali na misemo kama kiungo cha kimsingi katika kazi ya fasihi chenye uamilifu wa kudhihirisha uhalisia wa mandhari ya kitamaduni ambamo mwandishi wa LC anaandikia kupitia kwa namna ya kusema ya wahusika, imani zao, amali zao, mitazamo yao miongoni mwa vipengee vingine vya kitamaduni. Utafiti huu vile vile ulikusudia kuhoji jinsi mbinu anazotumia mtafsiri kukwepa matatizo ya tafsiri huathiri matokeo ya mchakato huo ikilinganishwa na LC.

Nzyoka (2014) naye ameshughulikia mada hii kwa kutathmini tafsiri ya tamathali za usemi katika tamthilia ya *Antigoni* kutoka Kiingereza hadi Kiswahili. Katika kazi yake, sawa na watangulizi wake, anadhihirisha kuwa kuna changamoto mbalimbali zinazomkabili mtafsiri katika kutafsiri tamathali za usemi hasa jazanda, misemo na tashbihi. Anadhihirisha kuwa ingawa tamathali inaweza kukosa ulinganifu wa kimaana unaoakisi uhalisi wa matini chanzi, mtafsiri anaweza kutumia mikakati mbalimbali ili kufanikisha kazi yake. Akirejelea (Newmark 1988), Nzyoka anafafanua mbinu na taratibu za tafsiri zinazoweza kutumiwa katika tafsiri ya tamathali za usemi. Mbali na mbinu na taratibu hizo, anatathmini mikakati ifuatayo ya kutafsiri misemo ilivyotumika katika tamthilia ya *Antigoni*:

- i. Tafsiri ya msemu hadi msemu
- ii. Kutafsiri kwa kufasiri
- iii. Kutafsiri kwa kuondoa msemu
- iv. Tafsiri ya neno kwa neno

Baadhi ya matokeo ya utafiti wa Nzyoka yalikuwa sehemu ya msingi katika utafiti huu kwa sababu, kwanza, sawa na utafiti wa Nzyoka, utafiti huu ulihusu tafsiri za tamathali za lugha hasa methali na misemo. Pili, Nzyoka anasisitiza kuwa tafsiri nzuri ni lazima ifikishe ujumbe wa Mwandishi katika LC kwa wasomaji katika LL kwa usahihi. Mwelekeo huo ni sawa na wa utafiti huu katika kupima kiwango cha kufaulu na kujitosheleza kwa tafsiri ya Shamte katika kufikisha mvutano kitamaduni unaodhihirika katika *Arrow Of God* katika *Mshale Wa Mungu*. Tatu, kazi ya



Nzyoka ni miongoni mwa kazi chache zinazoshughulikia tafsiri ya methali na misemo kutoka Kiingereza hadi Kiswahili sawa na utafiti huu. Ina maana kuwa matatizo ya tafsiri aliyoyashughulikia Nzyoka yana uhusiano wa karibu yale yaliyoshughulikiwa katika utafiti huu

Fakih (2018), kwa upande mwingine ameshughulikia tafsiri ya riwaya kutoka Kiingereza hadi Kiswahili. Anachunguza swala la changamoto anazokumbana nazo mtafsiri wa riwaya. Miongoni mwa changamoto anazoshughulikia ni tofauti za kitamaduni baina ya lugha chanzi na lugha lengwa, kulingana naye, tofauti za kitamaduni zikiwemo tofauti katika dini, mavazi, mila na desturi zinaweza kutatiza mtafsiri wa riwaya katika kazi yake. Fakih hata hivyo, anataja tu kwa ujumla kuwa tofauti za kitamaduni ni changamoto inayomkumba mtafsiri, tofauti na utafiti wa Fakih, utafiti huu uliazimia kuchunguza kwa kina utamaduni katika tafsiri kupitia kwa misemo na methali hasa ikizingatiwa kuwa utamaduni ndio malighafi ya methali na misemo ya jamii husika.

Kutokana na maandishi tuliyopitia, inadhihirika kuwa tafsiri ya fani katika fasihi imeshughulikiwa kwa kiwango kikubwa katika baadhi ya lugha hasa lugha ya Kiingereza miongoni mwa lugha nyingine. Wengi wa wataalamu hawa hata hivyo, wanapendekeza njia ambazo zinaweza kufaulisha tafsiri ya fani za fasihi hasa zile ambazo zimefungamana na utamaduni ikiwemo methali na misemo, ila bado hawajatafiti kwa kina cha kutosha matokeo ya mbinu hizo za tafsiri wanazopendekeza. Hali nyingine inayojitokeza ni kuwa miongoni mwa fani hizi, methali na misemo imeshughulikiwa katika ujumla wake katika matumizi ya lugha ya kawaida na kwa ufupi sana. Tafsiri ya methali na misemo ina upekee fulani inapotumiwa kama kiungo cha kimsingi katika kazi ya fasihi na ambacho kina jukumu maalum kama ilivyo katika *Arrow Of God*. Tafsiri hiyo ni sharti ifanywe kwa makini hivi kwamba jukumu la fani hizo litimizwe. Hali hii inaweka wazi pengo la kiusomi linalohitaji kuzibwa kwa kujenga mawazo zaidi juu ya msingi wa mawazo ya watafiti watangulizi katika mada hii ya tafsiri ya methali na misemo kama kishawishi cha utamaduni. Mapitio haya vilevile yanadhihirisha kuwa ingawa tafsiri ya fasihi ya Kiswahili imetafitiwa kwa kiwango fulani, ni kazi chache mno zimeangazia utafiti wa tafsiri za methali na misemo; na katika kazi hizo hizo, fani hizi zimetaja tu kuwa vipengee vya fani vilivyofungamana na utamaduni na ambavyo huzua changamoto katika tafsiri kwa kuwa kuna tofauti za kitamaduni kati ya LC na LL bila kueleza kwa kina changamoto hizo zinavyozuka au kueleza kikamilifu njia za kukabiliana na changamoto hizo. Utafiti huu ulichunguza mbinu mbali mbali zinazoweza kutumiwa katika kujenga daraja baina ya utamaduni wa LC na LL kwa kutumia riwaya ya *Arrow*

*Of God* na tafsiri yake katika Kiswahili *Mshale Wa Mungu* na kwa njia hii kukabiliana na changamoto za tafsiri kwa ufasaha.

### 1.8 Misingi ya Kinadharia

Katika utafiti huu tulitumia maoni ya Even Zohar (1978) na Gideon Toury (1980) kuhusiana na nadharia ya Wingimifumo (TY). Kwa mujibu wa mwasisi wa nadharia hii Even-Zohar mwaka 1970, istilahi ‘mifumo’ iliasisiwa na Jurij Tynjanov ambaye alizuka na dhana ya ‘mfumo wa fasihi.’ Awali, wanaurasimi walichukulia kazi ya fasihi kama kipengee kilichojisimamia na ambacho kilijitenga na muktadha wake. Hawakuchukulia kazi ya fasihi kama zao la muda wala la mahali fasihi hiyo inamotoka. Tynjanov alipinga msimamo huu kwa kuwa aliuona kuwa mtazamo usio halisi wala sahihi kuhusiana na fasihi, akapendekeza kwamba kazi za fasihi zinafaa kuchunguzwa kama sehemu ya muktadha ambamo zimetoka. Kinyume na maoni ya wanaurasimi walioshikilia dhana ya ‘ufasihi’ wa kazi au sifa za kiubunifu zinazoifanya kazi ya fasihi kuwa ya kipekee, Tynjanov alionelea kuwa mtu hawezi kupima ubunifu katika kazi ya fasihi iwapo hakujua utamaduni ambamo kazi hiyo inatoka. Maoni haya ya Tynjanov, yalipelekea kuzuka kwa dhana ya ‘mfumo.’ Katika kufafanua dhana hii, alieleza kwamba utamaduni wa fasihi, tanzu za fasihi au hata kazi za fasihi zenyewe, huunda mifumo tofauti tofauti ambayo ilitekeleza majukumu yaliyohusiana katika lugha fulani mahususi.

Even-Zohar alipanua mawazo ya Tynjanov na kuifafanua zaidi dhana hii ya mifumo. Aliuita mtandao mzima wa mifumo mingi inayohusiana **Wingimifumo** (TY). Mifumo hii hujumuisha mifumo ya fasihi na ile isiyo ya fasihi. Dhana hii ilitumika kufafanua kazi za fasihi, za kisheria na zile zisizokuwa za kisheria. Ilipoasisiwa dhana ya wingimifumo iliingaliwa kama nadharia ya fasihi iliyokusudiwa kuangazia uchangamano wa kimfumo uliojibainisha katika fasihi, lakini baadaye ilipanuliwa na kuanza kutumika katika nyanja nyingine ukiwemo uwanja wa tafsiri. Nadharia hii inaweza kutumiwa kufafanua nafasi ya fasihi iliyotafsiriwa kama mfumo mmojawapo katika dhana ya wingimifumo inayoweza kudhibitiwa ndani mfumo mpana wa kifasihi. Nadharia hii ya Even-Zohar ilikuwa na uhusiano wa moja kwa moja na kazi yake katika fasihi ya Kihibrania kwa kuwa aliitumia katika kutafitia tafsiri katika fasihi ya Kihibrania. Kihibrania kilikuwa na upungufu wa matini asilia, na fasihi yake iliwiwa sana na kazi zilizotafsiriwa kutoka kwa fasihi ya Kirusi. Hali ya kiusomi ilipotokea kuwa hivi, kazi zilizotafsiriwa zilichukua nafasi ya katikati katika fasihi ya Kihibrania. Jambo hili ndilo lililomfanya Even-Zohar kuwaza kwa undani kuhusu

nafasi za kazi zilizotafsiriwa katika fasihi ya lugha fulani. Even-Zohar alichukulia tafsiri kuwa sehemu ya mtandao wa mifumo mingi ya fasihi. Nafasi ya tafsiri katika mtandao huu mzima ilitofautiana, kulingana na hali ya mfumo wa fasihi inamoingia. Kijumla inaaminika kuwa kazi zilizotafsiriwa huchukua nafasi ya pembeni katika mfumo fulani wa fasihi. Even-Zohar hakukubaliana na maoni haya, aliamini kuwa **kazi iliyotafsiriwa ingechukua nafasi yoyote ile katika mtandao wa wingimifumo; ama ya kati au ya pembeni kutegemea hadhi ya mfumo mkuu ambamo kazi tafsiri hiyo ilitoka.** Huu ndio mhimili mkuu wa kazi yake. Kwa mujibu wa Venuti (2000), kuna hali tatu ambapo kazi iliyotafsiriwa inaweza kuchukua nafasi ya katikati;

- (i) Wakati fasihi ya lugha lengwa ni changa au iko katika hali ya kuundwa,
- (ii) Wakati fasihi ni dhaifu au inachukua nafasi ya pembeni ikilinganishwa na fasihi nyingine katika ujirani wake,
- (iii) Wakati fasihi inapambana na changamoto fulani.

Kulingana na Even-Zohar, katika hali mbili za kwanza tafsiri hutekeleza majukumu muhimu kwa kuwa lugha hiyo haijitoshelezi kueleza matukio anuwai katika ulimwengu wa kisasa.

Kazi zilizotafsiriwa vilevile zinaweza kuzua tanzu mpya za fasihi ambazo hazipo katika fasihi ya lugha lengwa zinamojibainisha. Mara kwa mara tafsiri hizi huonekana kujitenga kutoka kwa kazi zilizozoeleka na kwa njia hii kuwezesha LL kufanya majaribio ya kitanzu. Even-Zohar aliamini hili kuwa kweli kwa tafsiri kwa lugha kama Kihibrania. Hapa kazi zilizotafsiriwa hazikuwa tu vyanzo vya mawazo mapya, bali pia kazi ambazo waandishi wabunifu katika lugha hiyo hujifunza kwayo. Hata hivyo hali huwa tofauti kwa fasihi zilizoendelea kama Kiingereza, japo kwa njia mbali mbali maendeleo hayo yamechangiwa na tafsiri kutoka lugha za kigeni. Kuna wakati ambapo fasihi huonekana kukwama bila chochote kipya kuichangamsha, katika hali kama hizi katika historia ya fasihi, tafsiri inapoingia katika fasihi “zilizokwama” ina uwezo wa kuleta au hata kuibua mtazamo tofauti kabisa katika fasihi husika. Hata hivyo, ni kawaida kwa kazi iliyotafsiriwa kuchukua nafasi ya pembeni katika tamaduni za kifasihi kama Kifaransa, huwa kuna mitindo ya kifasihi imara ya kuandikiwa. Katika hali hii tafsiri huelekea kufuata mitindo iliyopo badala ya kujitungia yao.

Ingawa Even-Zohar aliamini kuwa ni sababu za kifasihi tu zinazofanya kazi kutafsiriwa kutoka lugha moja hadi nyingine, baadaye alipanua mtazamo huu alipoanza kufafanua uchanganuzi wa kidaikronia wa fasihi na kuamini kuwa maswala yaliyo nje ya fasihi pia yalichangia katika kuchagua aina ya matini inayoteuliwa ili kufanyiwa tafsiri. Even-Zohar alishikilia kuwa uchaguzi wa matini inayoteuliwa kufanyiwa tafsiri unategemea hali iliyopo katika mfumo wa LL. Hili kwa upande wake pia lingethiri nafasi ambayo kazi iliyotafsiriwa ingechukua. Nadharia hii kwa njia hii, ilidai kuwa hali ya fasihi ya jamii ya LL ndiyo ilizingatiwa zaidi katika uteuzi wa matini ambayo ingetafsiriwa. Iwapo LL ilipungukiwa katika mitindo fulani au kukosa kuwepo kwa tanzu, tafsiri ya fasihi ingeweza kutumiwa kujaza mapengo hayo. Kulingana na Even-Zohar, hii pia hutofautiana kutegemea na nafasi ya tafsiri hiyo katika utamaduni lengwa. Iwapo tafsiri inachukua nafasi ya kati kati, itatukuzwa kama kazi asilia. Zaidi ya hivyo, alidai kuwa maana ya tafsiri hupanuka kujumlisha dhana nyingine ambazo vinginevyo haziwezi kuchukuliwa kama tafsiri katika hali hii kwa kuwa lengo la tafsiri ni kuleta kitu kipya katika utamaduni lengwa, tafsiri hiyo itadumisha sifa za kazi asilia.

Tafsiri hii itabadilisha mtazamo wa utamaduni pokezi kuhusu kazi ya fasihi. Itokeapo kuwa tafsiri ipo katika nafasi ya pembeni, hali hubadilika hivi kwamba, lengo litakuwa kufanya tafsiri itakayoingia sawasawa katika ruwaza iliyopo wala si kuzua mtindo mpya. Hii ni kwa sababu utamaduni lengwa tayari una tamaduni imara za kifasihi na hautakubali kujitenga ghafla kutoka kwa hali yake ya kawaida. Hali hii haitakubali kufanya majaribio yoyote katika muundo au katika mawazo, bali itatarajiwa kuwa sheria zake zifuatwe. Tafsiri katika hali hii italingana na utamaduni lengwa na wala si utamaduni chanzi. Tafsiri zinazochukua nafsi ya kati zitajaribu kudumisha ladha ya matini asilia na itasisitiza kutimiza uaminifu kwake. Tafsiri ambazo zinaonekana kama zinazochukua nafasi ya pembeni, kwa upande mwingine, zitakuwa zinang'ang'ana kutimiza mahitaji ya utamaduni lengwa na haziwezi kumudu kulingana na kazi asilia. Zinalazimika "kulainishwa" katika jaribio la kuzifanya ziwe sawa na utamaduni lengwa. Kimsingi kazi hizi zimekosa sifa ya kuwa na uaminifu kwa matini asilia.

Nadharia ya Wingimifumo, kwa mujibu Even-Zohar, haikushughulikia miktadha ya kijamii ambayo huzaa fasihi, ila iliweka fasihi katika mifumo iwe imetafsiriwa au isiyotafsiriwa katika ngazi mbalimbali. Hata hivyo kulikuwa na pingamizi kuhusiana na njia ambayo Even-Zohar

alipangilia lugha katika viwango. Wapo wengi ambao walihisi kuwa nadharia hii ilikuwa sahili mno na kuwa viwango hivi vilivyopendekezwa na Even-Zohar vilikuwa na maelezo mengi ya ziada pia. Kwa mfano, ikiwa lugha moja inachukua nafasi ya chini katika ngazi ya lugha anavyopendekeza Even-Zohar, ina maana kuwa lugha hiyo ni duni ikilinganishwa na lugha nyingine? Zingatia lugha kama Kihindi na Kiingereza nchini India. Kihindi hakina hadhi na uwezo wa Kiingereza nchini India. Tafsiri nyingi zinafanywa kutoka kwa lugha za Kihindi hadi Kiingereza. Tukizingatia nadharia ya awali ya Even-Zohar itamaanisha kwamba Kihindi ni lugha ya hadhi ya chini na utamaduni wake ni wa hadhi ya chini pia ambayo ni ngeni ikilinganishwa na Kiingereza, ila ni jambo wazi kuwa hii ni chukulizi ya kijuujuu na kwamba hali halisi ni changamano kutokana na sababu zisizo za kifasihi. Even-Zohar alitambua haya na kufanya jaribio la kuimarisha nadharia yake. Kutokana na jaribio hili nadharia ya Wingimifumo imepiga hatua kutoka hali yake ya mwanzo na inazingatia maswala yasiyo ya kifasihi ambayo yanathibiti tafsiri.

Baada ya Even- Zohar kuasisi nadharia ya Wingimifumo, Gideon Toury (1980), aliipa nadharia hii mtazamo mwingine. Gideon Toury anajulikana kwa kazi yake katika tafsiri ambayo kwa kiwango fulani ni sawa na alioishughulikia Even-Zohar. Kazi yake ambayo ni maarufu sana ni *In Search of a Theory of Translation*, kazi hii ni mkusanyiko wa karatasi ambazo ameziandika kutokana na utafiti wake wa tafsiri nyanjani ambazo zilichapishwa mwaka 1980. Mwanzo kabisa alianza na kushughulikia mradi mpana “The History of Literary Translation into Hebrew” katika kazi hii ambamo alijaribu kuelewa sababu halisi zilizochangia uteuzi wa kazi ambazo zingetafsiriwa, na kuchunguza kama kulikuwa na kanuni au sheria zilizoongoza tafsiri katika Wingimifumo mahususi. Nadharia ya Toury, inapendekeza kuwa sababu za kuchagua kazi maalum ili itafsiriwe zilikuwa zaidi sababu zisizo za kifasihi kuliko zilivyo za kifasihi. Toury aliendelea kusema kuwa uteuzi huu pia uliongozwa na upendeleo wa kibinafsi wa mtafsiri na sababu ya tafsiri. Si ajabu basi kuwa nadharia za tafsiri Toury zinachukuliwa kuwa na mwelekeo wa lugha na utamaduni lengwa. Katika kutoa mchango wake kwa nadharia ya wingimifumo, Toury alipinga nadharia za tafsiri ambazo zina mwegemeo katika chanzo cha kazi. Nadharia za tafsiri katika miaka iliyotangulia zilijaribu kutathmini tafsiri katika mizani ya ulinganifu wa kazi iliyotafsiriwa na matini chanzi. Nadharia ya Toury ilipinga mtazamo huu wa ulinganifu wa ML na MC. Aliamini kuwa tafsiri zilikuwa na nafasi mahali fulani baina ya pande mbili kinzani – upande wa ulinganifu kamili wa kazi iliyotafsiriwa na matini chanzi, na ule upande wa ukubalifu wa kazi

hiyo iliyotafsiriwa katika LL. Alishikilia kuwa hakuna tafsiri ambayo inaweza kukubalika asilimia mia moja katika utamaduni lengwa kwa kuwa itakuwa imesheheni viungo vingi vipya ambavyo haviwezi kukubalika katika LL sawa na kuwa hakuna tafsiri inayoweza kuwa na ulinganifu kamili na LC kwa kuwa tafsiri hiyo itaongozwa na kanuni za kitamaduni ambazo ni tofauti na zile za LC.

Toury alipendekeza kwa usahihi kuwa, kwa kufuata mwelekeo wa LL, swala la ulinganifu katika tafsiri litaleta matokeo halisia. Ni jambo lililopingika kuwa matini iliyotafsiriwa inachukuliwa kuwa wakilisho la LC, akikataa nadharia zote zilizoegemea kwenye ulinganifu wa tafsiri na MC, Toury aliangazia kwenye uhusiano kati ya MC na tafsiri yake. Hakutupilia mbali kabisa vipengee vya lugha na vile vya fasihi vinavyochangia katika tafsiri, ila alipendekeza vipengee vipya. Inadhihirika kuwa lengo la hatima la nadharia ya Toury lilikuwa kutoa mpangilio wa kingazi wa maswala yanayoingiliana na ambayo yanadhibiti tokeo la tafsiri. Kwa ufupi, Toury alitaka nadharia ya tafsiri kuhusisha maswala ya ukweli ya kitamaduni na ya kihistoria. Anapendekeza kuwepo kwa sheria ambazo anaziita “Kanuni za tafsiri.” (TY) Kwa pendekezo hili anakaribiana na Even-Zohar, lakini alipiga hatua zaidi. Anasema kuwa katika jamii yoyote ile kutakuwa na mkusanyiko wa kanuni nyingi katika kipindi maalum cha wakati. Kanuni hizi zinaweza kuhitilafiana, lakini kwa kufanya uchunguzi kwa utaratibu fulani kwa kipindi fulani cha wakati, zitaonyesha ruwaza fulani iliyofichama kwenye hizi kanuni zinazoonekana kutohusiana iwapo zitaangaliwa kijuu juu. Hivi ni kusema kuwa tafsiri tofauti za matini sawa katika nyakati tofauti katika utamaduni sawa zitaonyesha kanuni zilizodhibiti tafsiri ya wakati huo. Toury alipendekeza aina tatu za kanuni katika tafsiri: Kanuni za Matayarisho, Kanuni za Mwanzo na kanuni za Utendaji (TY).

Kanuni za matayarisho ni zile ambazo zinadhibiti mikakati ya kutafsiri na uamuzi kuhusiana na ni kazi gani za kutafsiriwa ili ziingie katika Wingimifumo fulani. Toury anasema kuwa hizi kanuni zinahusiana na kuwepo kwa sheria zinazodhibiti tafsiri, na pia kiwango cha umoja wa tafsiri. Sheria za tafsiri ni jumla ya maswala ambayo hudhibiti uteuzi wa aina za matini; au pia matini zitakazotafsiriwa na hivyo kuingizwa katika utamaduni fulani, au lugha fulani katika wakati kipindi fulani cha wakati. Hii ina maana kuwa maswala mengi yanahitaji kuzingatiwa kabla kazi itafsiriwe hadi utamaduni fulani. Mwegemeo wa kifasihi wa lugha fulani au utamaduni fulani huwa na mchango mkubwa katika kuamua aina za matini na matini hasa zitakazotafsiriwa. Swala

kuu huwa, ni aina gani za tafsiri ambazo utamaduni pokezi utakubali? Kanuni za kimatayarisho katika mchakato wa tafsiri huwa nje ya mapendeleo ya kibinafsi ya mtafsiri.

Kanuni za mwanzo ni maamuzi ya kibinafsi ambayo mtafsiri anapaswa kufanya kuhusiana na mikakati ya tafsiri. Kwa mfano; Je, afanye tafsiri itakayodumisha sifa za lugha chanzi au tafsiri hiyo idumishe sifa za lugha lengwa? Kanuni za utendaji, ambazo ni zile zinazodhibiti tafsiri yenyewe, Toury anazifafanua kama “Maamuzi elekezi yanayofanywa wakati wa tendo la tafsiri lenyewe.” Kanuni hizi zina nafasi katika matini iliyotafsiriwa katika utamaduni lengwa. Nadharia ya Toury inaonekana kuchukua pande mbili za kinadharia zinazokinzana, katika upande mmoja anapinga tafsiri zinazoegemea katika LC. Lakini katika kutumia nadharia zake analazimika kufanya uchanganuzi kiulinganifu wa tafsiri mbalimbali za matini ile ile chanzi. Badala ya kutumia mifano halisia, anatumia mifano ya kufikirika. Anakubali kuwa alihitaji ulinganishi huu usiobadilika ili kufikia pande zake mbili za tafsiri, zilizoegemea LC na zile zilizoegemea LL. Hali hii inaelekeza katika ukwelikiniani wa usawa uliofichika katika tofauti zinazoonekana kijuujuu katika lugha na tamaduni mbalimbali, ambayo ilikinza wazo lake la nadharia halisia ya tafsiri iliyoegemea LL. Hata hivyo, nadharia ya Toury imechangia sana katika utafiti wa tafsiri kwa njia nyingi. Nadharia zake zilisababisha kuchunguzwa kwa maswala ya utamaduni wa jamii katika tafsiri, maswala ambayo yalikuwa yamepuuzwa katika mchakato wa tafsiri.

Gentzler (2001) anadokeza kuwa; Toury ameathiri utafiti wa tafsiri hivi kwamba, wazo la kuwepo kwa ulinganifu kamili wa kazi iliyotafsiriwa katika lugha na pia katika fasihi limetupiliwa mbali, athari ya mitindo ya fasihi ya lugha lengwa katika tafsiri imetambuliwa, wazo la LC kuwa na maana imara kudidimizwa, matini chanzi na matini lengwa kuchukuliwa kama sehemu za mfumo wa kimaana na ambazo zinaingiliana. Inaelekea kuwa faida kubwa zaidi ya nadharia ya Toury ni kwamba ilitambua ukweli kuwa tafsiri ni tukio halisi ambalo hutokea katika ulimwengu halisi na kwamba watafsiri ni watu ambao wanaongozwa na itikadi zao katika tafsiri wazichaguazo. Katika hali hii basi tafsiri huwa kitendo kinachoenea na kukiuka mipaka ya lugha na ya fasihi ambacho kina matokeo yanayoathiri ulimwengu halisi kwa kiwango kikubwa.

Utafiti huu utajikita katika baadhi ya mihimili mikuu ya nadharia hii ya Wingimifumo, mihimili hii ni pamoja na;

- i. Mtazamo kuwa fasihi ni mtandao wa mifumo inayohusiana kwa njia moja au nyingine, fasihi itaangaziwa kama mfumo unaoweza kurejelewa kwa usahihi kama wingimifumo,
- ii. Mfumo huweza kuchukua nafasi ya kati au ya pembeni katika mtandao mzima wa wingimifumo,
- iii. Mwelekeo wa LL katika tafsiri; maoni kuwa mchakato wa tafsiri hudhibitiwa na lugha lengwa,
- iv. Kanuni za tafsiri ndizo hudhibiti tafsiri inayofanywa kwa matini yoyote.

Sawa na maoni ya waasisi wa nadharia ya wingimifumo, utafiti huu ulichukua mwelekeo kuwa fasihi ni mtandao wa mifumo mingi inayoingiliana na kwa sababu hii fasihi ni wingimifumo. Baadhi ya mifumo inayounga wingimifumo ya fasihi ni pamoja na; mfumo wa lugha ambao pia unaungwa na vipengee mbali mbali, upo mfumo wa fani ambazo mtunzi wa kazi ya fasihi hutumia katika kupitisha ujumbe wake au maudhui ya kazi yake, maudhui pia huunga mfumo mwingine katika wingimifumo hii miongoni mwa mifumo mingine. Utamaduni wa jamii ambamo fasihi mahususi huibuka vilevile, ni mfumo ambao huathiri fasihi yoyote ile inayojitokeza, hali hii inatokana na ukweli kuwa mtunzi wa kazi yoyote ya fasihi hutunga kazi yake akitumia mazingira yake kama malighafi ya fasihi itakayoibuka. Sehemu kubwa ya mazingira ya mtunzi kimsingi ni jumla ya utamaduni wa jamii ambamo fasihi hiyo inaibuka. Ina maana kuwa, mfumo wa utamaduni fulani hujitokeza kwa kiwango fulani katika fasihi ya jamii husika. Katika *Arrow of God*, mfumo wa utamaduni wa jamii ya Igbo unajitokeza kwa kiwango kikubwa kupitia kwa methali na misemo ya Kiigbo kwa kuwa utamaduni huu ndio mwandishi alidhamiria kuuangazia hasa jinsi unavyoathiriwa na utamaduni wa dini ya Kikristo. Hivyo basi katika riwaya ya *Arrow of God* mfumo wa utamaduni unavyowasilishwa na methali na misemo umechukua nafasi ya kati kati katika wingimifumo ya riwaya ya *Arrow of God*. Hata hivyo utamaduni kama mfumo unabainishwa katika mfumo wa fani hasa methali na misemo. Sawa na maoni ya Even-Zohar mifumo hii inaingiliana kwa kiasi kwamba bila utamaduni hakuwezi kuwa na methali na misemo, vile vile methali na misemo hurahisisha jukumu la kubainisha utamaduni wa jamii yoyote kwa



kuutaja utamaduni huo kwa maneno machache yenye mvuto na yasiyo rahisi kusahau, tofauti na hali ilivyo utamaduni unapobainishwa kwa kutoa maelezo yanayofanya shughuli hiyo kuwa nzito.

Utafiti huu umejibainisha katika kuchanganua mfumo wa methali na misemo, hasa kwa kuchunguza fani hii inavyojitokeza katika ML na athari ya tafsiri katika utamaduni uliofungamana katika methali na misemo. Mfumo wa methali na misemo huungwa kwa viungo mbali mbali, kwanza; maneno yaliyoteuliwa kwa ufundi mkubwa; pili umbo la kipekee katika jamii husika sawa na anavyosema Barajas (2010) kwamba, “maumbo ya methali ni muhimu katika kuelewa muundo wa kijamii wa maana zao kwa sababu hazijaundwa kwa neno moja na zina miundo maalum inayozitofautisha na vipashio vingine katika lugha hiyo. Hivyo basi watafsiri wanahitaji kufahamu maumbo ya methali.” Tatu, ni utamaduni wa jamii husika ambao utafiti huu unaupa kipaumbele. Litovikina (2014) anadai kuwa methali “zinaweza kubeba maudhui yanayohusiana na wanawake, taaluma na kazi, pesa, mapenzi, ndoa, talaka, urafiki elimu na kujifunza, pombe na mihadarati, watoto na wazazi, kodi Mungu na dini simu magari, tarakilishi ila maudhui niliyopigia msitari methali za Kiigbo katika *Arrow of God* zimesheheni masuala haya kwa hakika”

Methali na misemo ni fani ambazo zimechukua nafasi kubwa sana kwa kuwa, sawa na tulivyotaja awali takriban kila ukurasa una methali na misemo, wakati mwingine inatokea kwamba kuna methali na misemo zaidi ya mmoja katika ukurasa mmoja. Kwa mujibu wa Meider (2004) methali na misemo ni viwakilishi vya utamaduni na historia ya jamii husika, kwa kuzingatia hili, itakuwa sahihi kutaja kuwa fani hizi zimeungwa kwa kujumuisha vipengee mbali mbali vya utamaduni wa jamii ya Igbo, vikiwemo imani ya kidini, mielekeo ya Waigbo kuhusu maisha (mapenzi, kazi, ushirikiano, ndoa, kifo, mazishi miongoni mwa mengine), imani za kishirikina, mazingira, amali za jamii almradi chochote kinachohusu maisha. Hivyo, kwa kuchanganua fani hizi tulichunguza namna viungo vya utamaduni vinajitokeza katika tafsiri kwa jumla.

Tafsiri katika kazi za fasihi vilevile huchangia katika fasihi ya jamii lugha fulani ambayo inatambuliwa kwa utamaduni wake maalum, katika mchakato wa kufanya tafsiri ya kazi ya fasihi kutoka kwa LC hadi LL, maamuzi muhimu hufanywa ili kufikisha ujumbe wa mwandishi katika mfumo wa LL ambayo ina mfumo wa kitamaduni ulio tofauti na mfumo wa LC. Anavyosema Toury akipendekeza mwelekeo wa LL katika tafsiri, maamuzi hufanywa ili tafsiri inayofanywa ya

kazi ya fasihi kutoka kwa LC ikubalike katika utamaduni wa LL. Maamuzi haya huelekea kusawazisha tofauti za kitamaduni baina ya tamaduni mbili; utamaduni wa LC na ule wa LL na mwelekeo wa maamuzi haya hutegemea sheria za tafsiri pamoja na maswala yaliyo nje ya tafsiri. Kwa mfano, sheria za matayarisho hudhibiti maamuzi ya kazi itakayotafsiriwa na kubainisha dhamira ya tafsiri hiyo inayokusudiwa kufanywa. Katika kiwango hiki jukumu la tafsiri hubainishwa, na baada ya kuelewa jukumu la tafsiri, mtafsiri huwa ana mwelekeo wa jinsi atatafsiri kazi aliyo nayo. Katika kiwango hiki vilevile mtafsiri huamua mkondo wa tafsiri atakaouchukua; ama atafsiri kwa kutumia mbinu itakayodumisha muundo wa kazi anayotafsiri bila kuzingatia ujumbe au kujishughulisha katika kutafsiri ujumbe kwa ulinganifu iwezekanavyo, ingawa kwa kufanya hivyo huenda akapoteza muundo wa MC na katika hali hiyo kupoteza ujumi wa kazi yenyewe na usanii wa mtunzi wa kazi hiyo. Kutokana na nadharia ya Wingimifumo, tuliangazia methali na misemo kama mfumo katika mfumo wa fani ulio katika mfumo mkuu wa fasihi na unaotokana na mfumo wa utamaduni. Tulichunguza namna tafsiri za methali na misemo huthibitiwa na mfumo wa utamaduni ambao ndio unaangaziwa

### **1.9 Mbinu za utafiti.**

Utafiti huu ulikuwa wa maktabani. Tulichagua riwaya ya *Mshale wa Mungu* makusudi kwa kuwa mwandishi (Achebe) katika Kiingereza ametumia methali na misemo mingi. Tulisoma riwaya ya *Arrow of God* kama ilivyoandikwa na Achebe, na tafsiri yake katika Kiswahili *Mshale wa Mungu* kama ilivyotafsiriwa na Shamte ili kupata data ya kimsingi tuliyotumia katika utafiti huu. Data hii ilitokana na ukusanyaji wa methali na misemo kadri inavyojitokeza na ilivyotumiwa katika kazi chanzi, *Arrow of God*. Methali na misemo iliyotafsiriwa vilevile ilikusanywa kutoka kwa tafsiri ya matini chanzi kwa Kiswahili *Mshale wa Mungu* kwa kadri ilivyohitajika. Baada ya kupata data hii ya kimsingi kutoka kwa MC na ML, tuliiweka katika matapo. Utabakishaji huu ulifanywa kwa kuzingatia vipengee vya kitamaduni vinavyojitokeza katika methali na misemo vikiwemo: imani za kitamaduni, desturi za jamii husika, amali za jamii, utamaduni wa kidini, mazingira ya kitamaduni, na mfumo wa kitawala unaodhihirika katika jamii husika, kazi na shughuli za starehe za watu wa utamaduni husika miongoni mwa vipengee vingine. Tulisoma kwa makini riwaya ya Kiingereza *Arrow Of God* ilivyoandikwa na Achebe, kisha tukasoma tafsiri ya Kiswahili ya Shamte na kulinganisha maana na matumizi ya misemo na methali katika Kiingereza na maana na matumizi ya methali na misemo hiyo ilivyotafsiriwa katika Kiswahili. Ulinganishi huu ulitufaa katika kuhoji kiwango cha ulinganifu wa uamilifu wa fani hizi na kiwango ambacho vipengee

mbalimbali vya kitamaduni vilivyojitokeza kwa Kiingereza katika *Arrow of God* vimejitokeza katika Kiswahili katika *Mshale wa Mungu*. Tulizamia mada hii zaidi kwa kusoma vitabu, majarida, tasnifu, machapisho, makamusi ya tafsiri na makala mbalimbali yaliyochapishwa na kwenye mtandao kama chanzo cha data ya ziada. Zaidi tutapata data ya ziada kwa kufanya mijadala na wataalamu mbalimbali katika uwanja huu ili kupata maoni ya wataalamu mbalimbali katika uwanja wa tafsiri ambao ulitusaidia katika uelewa wa maswala muhimu katika utafiti huu na kutupa ushahidi tuliohitaji ili kutoa misimamo muhimu kuhusiana na utafiti huu.

## SURA YA PILI

### TAFSIRI YA METHALI NA MISEMO KAMA VIWAKILISHI VYA UTAMADUNI KATIKA *ARROW OF GOD*

#### 2.0 Utangulizi.

Kwa mujibu wa Lloyd (1972), kazi za kibunifu za Achebe zinadhihirisha kujishughulisha kwake kwa kiwango kikubwa na lugha, sio tu kama chombo cha mawasiliano, bali pia kama wasilisho la tajriba kamili ya utamaduni. Katika kiwango hiki, lugha inatumika sio tu kama nyenzo, bali pia kama dhihirisho la kiwango cha kustaarabika kwa jamii na inawakilisha mikondo ya uelewa na muonoulimwengu wa watu katika kundi la kitamaduni. Mwingiliano wa kisanii baina ya muundo na ujumbe katika riwaya za Achebe, ikiwemo riwaya ya *Arrow of God* unatoa mchango mkubwa katika uelewa wa utamaduni wa Ki-Igbo kwa wasomaji katika misingi ya kimaadili na ya kiuajumi. Kulingana na utamaduni wa Ki-Igbo msemaji mzuri ni yule ambaye anatumia methali zinazoakisi utamaduni wake kwa ujuzi na busara. Methali huwakilisha msembo wenye busara unaoeleweka miongoni mwa watu wa utamaduni fulani. Awa na Ngele (2014) wakimnukuu Amadiume (1995:3) wanasema kuwa, “katika riwaya yake ya kwanza kabisa *Things Fall Apart*, Chinua Achebe anafafanua methali kama mawese ambayo kwayo maneno huliwa” (TY). Kulinganishwa kwa methali na mawese kunaonyesha kuwa methali ni kiungo ambacho hufanya usemi kuvutia. Mawese hutumika kulia viazi vikuu kwa kuwa huvifanya viwe vitamu zaidi, sawa na vile methali huongeza ladha katika usemi na kusisitiza mambo muhimu. Methali pia inaweza kutumiwa na watu wa jamii lugha fulani wanapokuwa miongoni mwa wageni kuficha maana. Kulingana na kamusi ya Webster (2000) uwezo huu wa methali unatokana na hali kuwa umejikita kabisa katika utamaduni wa jamii mahususi, yaani ujumla wa tabia ya binadamu na matokeo ya tabia hizi, ambayo hujitokeza katika mawazo, usemi, au vitendo na mtu hupata utamaduni huu kupitia kwa kujifunza, kupata elimu na pia kupitia kwenye tajriba yake.

Kwa mujibu wa Gogoi (2017), Achebe anafaulu kubadilisha lugha ya Kiingereza kwa kuiongezea methali, vitendawili, visa vya kimaadili na hadithi mbalimbali za Ki-Igbo kwa wingi. Hata hivyo, jukumu la Achebe halipaswi kuchukuliwa kama ambalo lilikuwa mchakato wa kunyunyizia kazi yake methali chache na hadithi mbali mbali hapa na pale tu; lilikuwa jukumu changamano. Kupitia kwa lugha yake Achebe anatoa jaribio katika kuwasilisha muundo mzima wa kimawazo wa watu wa Afrika; anajaribu kupenya katika enzi zilizopita na kuwapa wasomaji wake nafasi kuionja

tajriba ya utamaduni mkamilifu. Akimnukuu Gikandi (1991) kuhusu jinsi Achebe anavyotumia lugha, Gogoi (2017) anaendelea kusema kuwa ingawa tunasoma ulimwengu wa Igbo katika Kiingereza, Achebe anajitolea kwa kiwango kikubwa kutumia fani mbalimbali za lugha. Miongoni mwa fani hizi anazotumia Achebe, zinazojitokeza zaidi ni methali na misemo na huwapa wasomaji wake uelewa wa jinsi utamaduni huu ulivyojikwawakilisha na unavyojidhihirisha ili kupinga lugha ya mkoloni (Kiingereza) iliyo banifu kimuundo na dumifu kwa jumla. Hivyo basi, Achebe anajaribu kushughulikia chanzo cha nguvu ya watu wake, hisia zao, matamano yao, ukamilifu wa kanuni zao za maisha na mitanziko ya maisha yao kwa kuibadilisha lugha hiyo ya mkoloni na kuifanya iseme hadithi ya Kiafrika kutoka kwa mwono wa Kiafrika. Katika kudhihirisha kuwa Wa-Igbo wa Umofia kabla ya ukoloni walikuwa na mipangilio ya kijamii, kitamaduni, kielimu, kiutawala, na mipangilio ya kimahakama, Achebe anatumia methali, hadithi na ngano kama ghala na hazina ya amana na tamaduni. Anawasilisha falsafa ya ulimwengu wa Igbo kupitia kwa methali na hadithi. Anadhihirisha kuwa jamii huweza kuwa na umoja kwa kushikilia amali na ukamilifu wa kimaadili ulio katika methali.

Kwa mintarafu ya kauli hizi za ufunguzi, lengo la sura hii ni kutalii nafasi ya utamaduni katika kutafsiri methali na misemo. Ni muhimu kutambua kwamba, katika sura hii na utafiti huu kwa jumla, neno *utamaduni* linatumika kwa maana mahususi. Dare (2008) amefafanua istilahi hii ya utamaduni kwa upana sana, anasema kuwa utamaduni ni ruwaza ya tabia na mawazo ambayo kundi mahususi la kijamii hujifunza, kuumba, na vile vile kushiriki. Pia utamaduni ni kibainishi na kitambulisho cha lugha, utambulisho wa watu, utaifa wao, uchumi wao, na kadhalika. Anachukulia utamaduni wa watu kuwa jumla ya maisha yao, michakato ya kuishi kwao na kufa kwao hasa kwa kuzingatia kiwango cha ukuaji na ustawi wa jamii na pia kiwango chake cha ustaarabu; katika hali kuwa utamaduni hudhibiti itikadi, desturi, imani, maadili na amali za jamii kwa kuwa umesheheni, sanaa, dini, falsafa, ruwaza za tabia na mawazo ambayo watu wanaoishi katika kundi mahususi jamii wanaumba na kujifunza. Anasisitiza kuwa utamaduni ni maisha, kuishi na kufa kwa kundi la watu-kusema kwao, kuonekana kwao, chakula chao, kuzaliwa kwao na kuzikwa kwao, ndoa zao na afya yao; almradi kila kitu kinachounga kuishi na kufa.

Sera ya utamaduni ya taifa la Nigeria ya mwaka 1988 inaupangilia utamaduni katika matapo kadha wa kadha na inaeleza kuwa, utamaduni umejumlisha vipengee vinne vifuatavyo: kipengee cha nyenzo, kipengee cha taasisi, kipengee cha falsafa, na kipengee cha ubunifu. Kipengee cha nyenzo kinahusiana na zana na vifaa vya kijamii katika upana wake (nyumba vyombo, chakula, dawa, mavazi na kadhalika); kipengee cha taasisi hujishughulisha na miundo ya kijamii, miundo ya kisiasa, miundo ya kisheria na ile ya kiuchumi iliyowekwa ili kufikia malengo sio tu ya nyenzo bali pia ya kiroho; huku kile kipengee cha kifalsafa kikijishughulisha na mawazo, imani na amali; kipengee cha ubunifu huhusu fasihi ya watu (fasihi simulizi au fasihi andishi) na vilevile sanaa za maonyesho na utendaji ambazo kwa kawaida hufinyangwa na vilevile kusaidia kufinyanga vipengee vingine vya utamaduni.

Katika utafiti huu utamaduni ulichukuliwa kwa misingi inayolingana na maoni ya Dare (2008) kuwa, ujumla wa maisha ya watu wa jamii mahususi, kila kitu au hali inayochangia au kuathiri kwa namna yoyote ile, kuzaliwa, kuishi na kufa kwa watu wa jamii fulani. Kwa mujibu wa utafiti huu utamaduni vile vile umeainishwa katika makundi makuu kwa kuwa utamaduni ni mfumo mzima unaojitokeza katika wingimifumo ya *Arrow of God*. Newmark (1988) aliainisha utamaduni katika kategoria tano tofauti, kategoria hizi ni pamoja na: Ikolojia, utamaduni nyenzo, taasisi za jamii, utamaduni wa kijamii, desturi na mawazo na ishara na tabia. (TY) Newmark alifafanua kategoria hizi ifuatavyo: Kategoria ya ikolojia ambayo hujumuisha wanyama, mimea, upepo unaovuma katika eneo fulani, milima, nchi tambarare miongoni mwa vitu vingine. Dhana kama vyakula, mavazi, maskani, njia za usafiri na mawasiliano huanishwa katika utamaduni nyenzo. Kategoria nyingine ni ya utamaduni wa kijamii ambao unarejelea, kwa mfano, kazi na starehe za watu wa jamii fulani. Mipangilio ya kisiasa, kijamii, kisheria, kidini na usanii wa watu wa jamii husika hujadiliwa katika kategoria ya utamaduni wa taasisi, desturi na mawazo. Kategoria ya ishara na tabia hurejelea tabia za watu wa tamaduni tofauti tofauti katika hali tofauti tofauti.

Tofauti na Newmark, Mgbemere (2014) anadai kwamba kuna aina mbili za tamaduni: utamaduni nyenzo (vifaa vya kijamii) na utamaduni usio wa nyenzo. Utamaduni wa nyenzo hurejelea vitu vinavyoonekana, raslimali na nafasi ambazo watu hutumia kufafanua utamaduni wao. Hivi ni pamoja na makazi (maskani na mastakimu), ujirani, miji, shule, makanisa, masinagogi, mahekalu, misikiti, maafisi, viwanda, vifaa, mbinu za uzalishaji bidhaa na mazao, maghala na kadhalika.

Utamaduni usio wa nyenzo kwa upande mwingine unarejelea mawazo yasiyo dhahiri waliyo nayo watu kuhusu utamaduni wao zikiwemo; imani, amali, sheria, kanuni, lugha, mashirika na asasi. Kwa mfano, dhana ya utamaduni usio wa nyenzo hujumuisha mawazo na imani kuhusu Mungu, ibada, maadili, na adabu. Kwa kuzingatia migao hii ya Newmark na Mgbemere, utafiti huu umeainisha utamaduni katika kategoria tatu kuu ambazo zitaainishwa zaidi kadri vipengee hivi vya utamaduni vitakavyojitokeza katika *Arrow of God*. Kategoria hizi za utamaduni ni utamaduni wa mazingira ya kiikolojia, utamaduni wa kijamii na utamaduni wa nyenzo (vifaa vya kijamii).

Kategoria ya utamaduni wa mazingira ya kiikolojia sawa na kategoria ya ikolojia ya Newmark, imejumlisha maumbile ambayo yanamzunguka binadamu na binadamu ana mchango mdogo sana (kama anao) katika kuwepo kwake. Mazingira haya husheheni, wanyama, ndege, wadudu, mimea na maumbile mengine yanayomzunguka binadamu na kumwathiri ambayo hakuchangia katika kuwepo kwake kama vile, ardhi, upepo, mvua miongoni mwa maumbile mengine. Utamaduni wa nyenzo kwa mujibu wa utafiti huu, unarejelea vitu vyote anavyotumia binadamu katika shughuli zake za kila siku; kimsingi ni raslimali na nafasi ambazo watu huunda na kutumia katika kufafanua utamaduni wao. Hivi ni kusema kwamba utamaduni nyenzo hujumuisha makazi (maskani na mastakimu), ujirani, miji, shule, makanisa, masinagogi, mahekalu, misikiti, maafisi, viwanda, vifaa, maghala na kadhalika. Utamaduni wa kijamii kwa upande mwingine unarejelea mawazo yasiyo dhahiri waliyo nayo watu kuhusu utamaduni wao zikiwemo; imani, desturi, amali na busara, sheria, kanuni, lugha, mashirika na asasi za jamii. Kwa mfano, dhana ya utamaduni wa kijamii hujumuisha mawazo na imani kuhusu Mungu au miungu, ibada, maadili, na adabu miongoni mwa maswala mengine.

Kama tulivyotangulia kutaja, riwaya ya *Arrow of God* imeandikwa kwa lugha ya kipekee ili kuweka wazi utamaduni wa Wa-Igbo. Utamaduni huu wa Igbo basi, kulingana na ufafanuzi uliotolewa awali, husheheni kila kipengee cha maisha ya Wa-Igbo, tangu kuzaliwa, kukua kufa na hata kuzikwa kwao. Vipengee hivi vya kitamaduni vinaunda kitovu cha ufinyanzi wa methali na vimejibainisha katika methali na misemo inayojitokeza katika *Arrow of God* kwa kuwa ndivyo malighafi ya vipengee hivi vya fani. Kwa misingi ya mantiki hii, azma ya utafiti huu kwa jumla ni kutathmini ujitokezaji wa utamaduni unaojitokeza kwenye lugha chanzi katika lugha lengwa kupitia kwa tafsiri ya methali na misemo. Hata hivyo katika sura hii utamaduni wa jamii ya Igbo

haujabainishwa kwa kina ila maswala ya jumla yataangaziwa katika kubainisha namna utamaduni huathiri tafsiri za methali na misemo kutoka katika LC hadi LL. Maoni ya wataalamu mbalimbali yamehusishwa ili kuweka misingi thabiti, iliyo muhimu katika uchunguzi wa tafsiri za methali na misemo kama viwakilishi vya utamaduni. Misingi hii ilifaa sana katika kufanya tathmini ya tafsiri ya Methali na misemo sio tu kama ilivyofanywa na Shamte, katika *Mshale wa Mungu*, bali pia katika tafsiri nyingine kama hizo zilizofanywa tayari au zitakazofanywa.

Mgbemere (2014) anasema kwamba, kwa kuangazia vigezo vyote vya kutambua utamaduni, *Arrow of God*, ni usimulizi wa kitamaduni kuhusu ulimwengu wa Igbo, katika enzi za ukoloni. Riwaya hii imegusia vipengee vyote vya maisha ya hawa watu, ushirikiano wao, tofauti zao, maisha yao, ruwaza za kuishi na kufa kwao na zaidi ya yote tabia fulani za kitamaduni mahususi kwa utamaduni wa Igbo ambazo hazina njia nyingine ya kuwasilishwa ila kwa kutumia vidokezi ambavyo vikichunguzwa hudhihirisha maana iliyojificha kwenye kipengee kinachokusudiwa cha utamaduni.

Sawa na tulivyotaja katika sura ya kwanza, Litovikina (2014) anadai kuwa methali zinaweza kubeba maudhui yanayohusiana na wanawake, taaluma na kazi, pesa, mapenzi, ndoa, talaka, urafiki, elimu na kujifunza, pombe na **mihadharati**, watoto na wazazi, kodi, Mungu na dini **simu magari, tarakilishi**, anaendelea kusema kwa usahihi kuwa maudhui haya yanajitokeza katika methali na misemo iliyo katika *Arrow of God*, isipokuwa maudhui yaliyokolezwa wino, yaani mihadharati, simu, magari na tarakilishi, haya kwa kweli hayamo katika riwaya hii. Maudhui hayo mengine yote yanajitokeza katika methali na misemo ya Ki-Igbo kwa njia anuwai katika *Arrow of God*. Maudhui haya anayotaja Litovikina, kimsingi yanaathiri binadamu kwa njia moja au nyingine, na kulingana na maelezo tuliyotangulia kutoa hapo juu, chochote kinachohusu kuishi na kufa kwa binadamu ni sehemu ya utamaduni wake. Ikumbukwe pia kuwa tamaduni za jamii tofauti huweza kulingana kwa kiasi fulani, kwa mfano, katika desturi zao, mazingira yao au hata imani na shughuli zao za kikazi, lakini hakuna utamaduni ulio sawa na mwingine kwa asilimia mia moja. Hivyo basi, kila jamii ina utamaduni wake wa kipekee ambao hujitokeza katika maisha ya wanajamii husika. Sawa na utamaduni wa jamii yoyote ile, utamaduni wa Ki-Igbo kama unavyobainika katika methali na misemo, unaweza kuainishwa katika matapo matatu makuu ambayo tulitangulia kutaja, yaani utamaduni wa mazingira ya kiikolojia, utamaduni wa nyenzo



(vifaa) na utamaduni wa kijamii. Kwa kuwa utamaduni unaweza kuanishwa, vile vile methali na misemo inaweza kuainishwa katika matapo mbali mbali kulingana vipengee vya utamaduni ambavyo methali hizo zinawakilisha.

Ni muhimu kutambua kuwa utamaduni haujielezwa wala kufafanuliwa kwa ukamilifu katika methali na misemo husika, bali baadhi ya dhana za kitamaduni zimetajwa au kurejelewa kwenye methali na misemo. Dhana hizi zinazotokana na utamaduni wa Ki-Igbo zinapochunguzwa kwa kina hubainisha kuwa, vipengee vya utamaduni zinazowakilisha vimechangia katika kuwepo kwa methali au misemo hiyo, ama kwa kuchochea kubuniwa kwa methali na misemo hiyo au kuhusika katika kubuniwa kwa fani hizi.

### **2.1 Tafsiri za methali na misemo kama mfumo wa kimsingi katika wingimifumo ya kazi ya fasihi**

Kwa mujibu wa nadharia ya wingimifumo kama inavyofafanuliwa na Toury (1980), tafsiri huhusisha maswala yaliyo nje ya lugha. Hivyo basi katika kuchunguza ulinganifu wa tafsiri ni muhimu kuzingatia sio tu ulinganifu wa kileksika, bali pia viwango vingine vya ulinganifu vilivyo nje ya lugha. Kulingana na madai ya nadharia hii ya wingimifumo yaliyotangulia kujadiliwa, kazi yoyote ya fasihi ni wingimifumo iliyofumwa na mifumo mbalimbali ambayo imechukua nafasi ama ya katikati au ya pembeni katika mfumo mkuu. Mfumo huchukua nafasi katika wingimifumo kwa kutegemea jukumu la mfumo huo katika kufaulisha lengo kuu la wingimifumo husika. Utafiti huu ukiongozwa na nadharia ya wingimifumo unapendekeza kuwa, katika shughuli ya kutafsiri mtafsiri awe makini sana; badala ya kuangazia na kutafsiri wingimifumo husika kwa jumla ni bora mtafsiri huyo afanye tafsiri huku akizingatia mifumo iliyomo kwenye wingimifumo hiyo na nafasi ya mifumo hiyo inayojitokeza katika wingimifumo. Baada ya kutaja hivi, utafiti huu unasisitiza kuwa mtafsiri akizingatia kiuchanganuzi mifumo inayounga wingimifumo husika na kuitafsiri kwa usahihi anaweza kufikia lengo la jumla la tafsiri-linganifu. Mtafsiri basi, anafaa kuzingatia nafasi za mifumo katika wingimifumo anayotafsiri ili kuhakikisha kuwa matokeo ya tafsiri yake yanatimiza azma ya tafsiri ambayo ni kuufikisha ujumbe wa mwandishi wa LC kwa wasomaji katika LL kama alivyokusudia mwandishi.

Baada ya kutaja haya, ni muhimu kutambua kuwa methali na misemo ni mfumo ambao unachukua nafasi ya katikati katika riwaya ya *Arrow of God*. Madai haya ni kwa mujibu wa Gogoi (2017)

kuhusu jukumu la methali na misemo katika usimulizi mzima; anadai kuwa, Achebe ana azma ya kutambulisha utamaduni wa Ki-Afrika hususan Ki-Igbo, kwa wasomaji wake. Achebe anatumia lugha ya Kiingereza ambacho kimesheheni miongoni mwa fani nyingine, methali na misemo ya Ki-Igbo fani zilizo na uamilifu mkubwa sana; zinamsaidia kubadilisha lugha ya Kiingereza na kuifanya iseme hadithi ya Ki-Afrika kupitia kwa mwonoulimwengu wa Mwafrika. Swala hili linadhihirisha busara ya kutafsiri riwaya kama *Arrow of God* kwa kutilia maanani methali na misemo, viungo ambavyo kimsingi ni viwakilishi vya utamaduni na ambavyo vimejitokeza kwa wingi. Isisahaulike kuwa katika kuwakilisha utamaduni wa jamii husika, methali na misemo hudhihirisha mvuto wa kisanii wa jamii husika na hivyo kuleta athari ya kiujumi ya kazi ya fasihi. Hivi ni kusema kwamba, methali na misemo ya Ki-Ibo ina uzuri wa kiujumi unaotokana na usanii wa kifasihi wa Wa-Igbo ambao unahitaji kutafsiriwa pamoja na ujumbe kutoka kwa *Arrow of God* hadi kwa LL ambayo katika muktadha huu ni Kiswahili.

Katika mwanga wa nadharia ya wingimifumo, mhakiki wa tafsiri ya methali na misemo ana haja ya kujiuliza maswali ya kimsingi kabla ya kufanya tathmini ya tafsiri yoyote ile iliyofanywa na maswali haya ni pamoja na: Ni nini jukumu la mtafsiri wa kazi yenye methali na misemo kama kiungo cha kimsingi? Je, ufasaha wa tafsiri ya methali na misemo hutegemea nini? Katika kujibu maswali haya muhimu, mhakiki anaweza kufanya maamuzi mazuri kuhusu tafsiri yoyote ya methali na misemo iliyofanyika. Ikumbukwe kuwa kutafsiri matini zilizo na msambao mkubwa wa vipengee vya kitamaduni si kazi rahisi kwa kuwa katika kufanya tafsiri mtafsiri huitoa sehemu ya mfumo wa utamaduni katika wingimifumo yake asilia na kujaribu kuingiza mfumo huu kwa wingimifumo tofauti. Hivyo basi, ili mtafsiri afaulu katika azma yake hii, anafaa kufahamu vyema mfumo wa utamaduni wa jamii lugha ambamo kazi anayotafsiri inatoka, na vile vile mfumo wa utamaduni wa jamii lugha ambamo kazi anayotafsiri inamoingia.

## **2.2. Vizingiti katika kutafsiri methali na misemo**

Methali na misemo kama viwakilishi vya utamaduni ni miongoni mwa fani changamano kutafsiri kwa sababu, zaidi ya kutafsiri methali na misemo katika misingi ya maana za maneno yanayoiunda, kuna haja ya kutafsiri pia utamaduni uliojikita humo. Kwa kuzingatia kauli zilizotolewa na Abbas (2015) kwamba vipengee vingi vinavyojitokeza katika kazi za kiubunifu kama vile ujitokezaji wa utamaduni na desturi za kitamaduni ni masuala magumu sana kushughulikia katika michakato ya kutafsiri kutoka lugha moja hadi nyingine, hasa iwapo tunataka kudumisha umbo na muonjo wa methali asilia. Ugumu huu wa kutafsiri unatokana na sababu kwamba imani za kidini, mazoea na desturi, visasili na utamaduni hutofautiana kutoka jamii tumizi-lugha moja hadi nyingine. Kufahamu usuli wa kitamaduni na mahusiko yake katika ukuaji na matumizi ya lugha, kunaweza kutusaidia kutambua maana za kitamaduni za methali na misemo ili kuzitafsiri ipasavyo. Methali kama kifani kilichosheheni vipengee hivi vya kitamaduni, haziwezi kutafsiriwa kwa njia ya moja kwa moja kwa sababu zitapoteza uamilifu wao, ni lazima kutumia methali linganifu kutoka kwa LL inayotimiza wazo la methali katika LC ili kuingia katika nafasi ya methali katika LC.

Kuchagua methali mwafaka katika ML ya kutumia kama tafsiri ya methali katika MC ni mchakato changamano kwa sababu ni shughuli inayohusu kuchagua ni lipi la kupewa nafasi zaidi miongoni mwa mambo mbalimbali yanayohusika katika kufanya uteuzi huu. Kwa mujibu wa Dabaghi na wenzake (2010), kila methali huwasilisha maana mahususi katika muktadha mahususi, kwa sababu hii methali inafaa kutafsiriwa kwa makini ili kuhawilisha hali za kitamaduni kama zilivyo katika methali asilia, hadi kwenye methali iliyotafsiriwa. Sio jambo la busara kutafsiri methali kwa kuzingatia maana za maneno yake kama yalivyo katika kamusi. Ina maana kuwa katika kutafsiri mfumo wa methali na misemo, ni lazima mtafsiri atafsiri mfumo wa utamaduni pia. Kwa kuwa tamaduni za jamii tofauti huwa tofauti, mara kwa mara mtafsiri atajikuta katika hali inayomhitaji kufanya kazi iliyo zaidi ya tafsiri kwa maana yake ya kimsingi; kutafsiri LC na kufasiri utamaduni wa LC, dhamira ambayo huenda ikamwia mtafsiri ngumu kuafikia kwa asilimia mia moja kwa sababu ya tofauti hizi za kitamaduni. Mtafsiri huenda akapata changamoto katika shughuli yake ya kutafsiri kwa sababu ya vizingiti vifuatavyo:

### 2.2.1 Udhaifu wa mtafsiri

Vizingiti vya tafsiri ya methali na misemo huweza kutokana na ujuzi finyu wa mtafsiri katika tafsiri kama vile: mtafsiri kutokuwa na uwezo wa kutafsiri maneno au kauli zilizofungamana na utamaduni vizuri. Hali hii inasababisha kutoa kisawe katika lugha lengwa kisicho sahihi; kutoa maana isiyofaa na kufanya makosa katika ufafanuzi; kutumia tafsiri ya moja kwa moja na matumizi mabaya ya maneno mwafaka ya kileksika; kufanya makosa ya lugha, makosa ya mtindo na ya sarufi; na kutofahamu mikakati na mbinu za tafsiri. Kulingana na Newmark (1988), kuna matatizo mengi ya lugha ambayo mtafsiri hukabiliana nayo wakati anapotafsiri kama vile: kufanya makosa yanayotokana na mtafsiri kukosa kuwa na uwezo katika kuandika vizuri, matumizi mabaya ya makamusi, kutumia tafsiri ya moja kwa moja ya methali au kukosa uwezo wa kufanya maamuzi mwafaka kuhusiana na tafsiri. Vilevile haya matatizo ya lugha yanaweza kutokana na ujuzi finyu wa sarufi, mtindo, maneno ya kileksika, nahau au tamathali. Makosa kama haya yanayotajwa na Newmark yanajitokeza katika tafsiri ya riwaya ya *Arrow of God* hasa katika baadhi ya methali zilizotafsiriwa na Shamte kwa mfano methali *The man who has never submitted to anything will soon submit to the burial mat*, katika *Arrow of God* ukurasa 11 imetafsiriwa kuwa *Mtu ambaye hajapata kuitikia chochote, ghafla huitikia mkeka wa kuzikiwa katika Mshale wa Mungu* ukurasa 10 Tafsiri ya methali hii inapochunguzwa, neno “soon” katika *Arrow of God*, limetafsiriwa kuwa “ghafla”. Neno hili “soon” lina maana ya “karibuni au hatimaye” katika muktadha wa methali hii. Maana hii inapaswa kujitokeza katika tafsiri inayofanywa ya neno hilo katika methali, ila mtafsiri anatumia neno “ghafla” ambalo kimsingi linaleta dhana ya “bila kutarajiwa.” Kwa kufanya hivi, maana ya methali ambayo inafaa kuwa mtu shujaa, ambaye hashindwi na yeyote hatimaye hushindwa na mauti, imejitokeza kuwa na maana kuwa mtu ambaye hashindwi na yeyote hufa bila kutarajia. Maana hii inavyojitokeza ni tofauti na kusudio la mwandishi na inatokana na mtafsiri kutoa kisawe cha neno la LC kwa LL kisicho sahihi.

### 2.2.2 Ufahamu finyu wa utamaduni wa LC.

Kulingana na Awa & Ngele (2014) fasihi ya Kiafrika ambayo imeandikwa kwa lugha za Kizungu kama vile *Arrow of God*, tayari ni aina ya tafsiri kwa sababu, ingawa mwandishi bila shaka hufikiria kwa lugha yake ya kwanza, huiandika fasihi hiyo kwa lugha ya kigeni kupitia kwa michakato ya kitafsiri. Hivyo basi, mtafsiri anafaa kuwa makini sana kuhakikisha ana ufahamu wa kina wa utamaduni na historia ya jamii ambayo kwayo kazi hiyo ya fasihi imekitwa; la sivyo atafanya makosa katika tafsiri. Zaidi ya hali hii, inawezekana mwandishi anapoandika akatumia

maneno au kauli katika lugha anayoitumia, kwa mfano Kiingereza, ambazo zinatoa maana isiyokusudiwa kwa kukosa ulinganifu mwafaka kutokana na tofauti za kitamaduni baina ya utamaduni wa mwandishi na utamaduni wa lugha anayoitumia kuwasilisha kazi hiyo ya fasihi. Hali inapotokea hivi basi mtafsiri wa kazi hii huwa na changamoto kubwa kwa kuwa inamwia vigumu sana kufikisha ujumbe huo kwa usahihi kwa kuwa huwa umedhoofishwa au kupotoshwa hata kabla ya tafsiri yenyewe.

### **2.2.3 Tofauti pana za kitamaduni.**

Vizingiti vya tafsiri vile vile vinaweza kutokana na tofauti pana za kitamaduni ambazo ni ngumu kupunguza. Tofauti hizi baina ya tamaduni husababisha vizingiti kwa watafsiri wanapotafsiri matini kama vile tamathali, methali, nahau na nyingine kama hizo. Maswala ya kitamaduni ambayo yanaweza kuathiri tafsiri yamejadiliwa na watafiti wengi kama vile Baker (1992) na Newmark (1988) na yamefanyiwa mukhtasari ifuatavyo; Utamaduni wa mazingira, kwa kuwa Kiingereza na lugha nyingi za Kiafrika zina istilahi tofauti zinazohusiana na wanyama, hali ya anga au mimea — hili ni dhahiri katika methali za Ki-Igbo ambazo zimekopa sana kutoka kwa mazingira yake kuhusiana na wanyama na mimea; utamaduni wa kidini—methali zinazorejelea desturi za kidini na utamaduni wa Ki-Igbo. Hili lina mchango katika kuathiri methali zinazohitaji kutafsiriwa kwa Kiswahili; hivyo basi dini ina athari za kimsingi katika kutafsiri methali za Ki-Igbo hadi Kiswahili. Utamaduni wa kijamii wa jamii ya Wa-Igbo huathiri kuundwa kwa methali kwa kuwa katika methali hisia za watu kuhusiana na mambo kama mapenzi, ndoa, miongoni mwa maswala mengine hujitokeza. Na hali hii hakika ni tofauti na ilivyo katika Kiswahili. Utamaduni wa nyenzo wa Wa-Igbo pia unajitokeza katika methali nyingi na hivyo methali ya Ki-Igbo kama kiwakilishi cha methali za Afrika Magharibi hutofautiana katika dhana zao na wanatumia aina tofauti za vyakula, maleba, samani, mapambo na hata njia za usafiri miongoni mwa mengine.

Tofauti za kitamaduni baina ya LC na LL hujitokeza katika dhana za kipekee katika jamii lugha mahususi. Baker (1992) anataja kuwa utamaduni huzusha changamoto zinazozua matatizo kwa watafsiri wanapotafsiri matini zilizo na kauli za kitamaduni, methali, jazanda, nahau na istilahi za kidini. Kuna dhana za lugha chanzi ambazo hazijulikani katika lugha lengwa; dhana hizi zinaweza kuwa ni dhana kuhusiana na imani za kidini, desturi za kijamii au aina ya chakula. Kwa mfano— *He who will swallow udala seeds must consider the size of his anus (Arrow of God: uk.226).* Methali hii imetafsiriwa kuwa *Mtu atakayemeza kokwa za udala lazima afikiri kiasi chake cha*

*mkundu (Mshale wa Mungu: uk.203)* neno *udala* linatumiwa kurejelea aina fulani ya matunda, yanayopatikana katika utamaduni wa Ki-Igbo. Dhana hii inaweza kuzua changamoto katika tafsiri kwa sababu ni dhana ngeni katika utamaduni wa Kiswahili ambapo tunda hili halifahamiki wala halina kisawe katika Kiswahili. Hivyo basi, jukumu la mtafsiri sio tu kutafsiri maana bali pia kutafsiri utamaduni kwa kufasiri dhana hizi ambazo vinginevyo hazieleweki nje ya jamii lugha husika la sivyo ML haitakuwa na maana kwa wasomaji kwa kuwa haitaeleweka kikamilifu. Dhana za kipekee katika *Arrow of God* ni pamoja na dhana za mazingira ya kiikolojia, mazingira ya kijamii, istilahi za kidini za dini ya kitamaduni ya watu wa Igbo, istilahi za vifaa vya kazi na taaluma za Ki-Igbo. Mbali na methali na misemo kutaja dhana za kipekee mingoni mwa jamii lugha mahususi, kwa kiwango kikubwa methali na misemo huundwa kwa kutumia jazanda. Kulingana na Shastri (2012:101), “Methali na tamathali zimefungamana na utamaduni mahususi, zinatumika kijazanda na huwasilisha dhana nzima kwa sentensi moja. Zinabeba jazanda maalum na dhana inayohitaji kutafsiriwa. Haziwezi kutafsiriwa moja kwa moja. Wakati mwingine hupata dhana zenye ulinganifu kamili katika LL ambazo zinaweza kuchukua nafasi yake kwa urahisi. Hata hivyo Iwapo ulinganifu wa aina hii haupatikani, nafsi yake inaweza kuchukuliwa na tamathali au methali yenye maana sawa katika LL” (TY)

Classe (2000) anachukulia kuwa tofauti baina ya utamaduni chanzi na utamaduni lengwa unaweza kusababisha kupotea kwa maana ya ndani ya methali au msemu kwa sababu kuna vipengee vya kimuktadha ambavyo vina sifa zinazohusiana na utamaduni wa LC pekee wala vipengele hivyo havipatikani katika utamaduni wa LL. Sifa hizi ni tabia na mitindo ya maisha yasiyo ya kawaida ambayo ni ya watu mahususi ambayo hayatokei katika LL, kwa mfano, *The thing that beats the drum for ngwesi is inside the ground (Arrow of God, 225)* ambayo imetafsiriwa kuwa *Kitu ambacho hupiga ngoma kwa ajili ya ngwesi kimo ndani ya ardhi (Mshale wa Mungu, 202.)* Inadhihirika kuwa methali hii inarejelea upigaji wa ngoma usio wa kawaida ila unaweza kueleweka katika muktadha wa mtindo wa maisha wa Wa-Igbo. Kwa kujikita katika mkondo huu wa changamoto za kutafsiri mambo yanayofungamana na utamaduni, Emery (1997) anadai kuwa kinachompa changamoto mtafsiri wakati wa kutafsiri methali ni hali yao kuwa zimefungamana na utamaduni. Hii inabainisha kuwa mtafsiri anawajibikia tamaduni zinazohusika kwa kuwa michakato ya kutafsiri inamjukumisha kuwa mpatanishi kati ya utamaduni chanzi na utamaduni

lengwa na anafaa kutoa maana ya moja kwa moja na maana ya kijazanda ya methali na pia athari yao ya kimawasiliano.

Mtafsiri wa *Arrow of God*, bila shaka anakumbana na changamoto hizi katika shughuli ya kutafsiri methali na misemo; kwa upande mmoja anahitajika kutafsiri methali kwa njia ya moja kwa moja itakayodumisha muundo wa methali na misemo ya mwandishi na kwa njia hiyo kutarajia kudumisha mvuto wa kazi asilia, ila miundo ya methali na misemo ya Kiswahili si sawa na ya Ki-Igbo. Kwa hivyo, kudumisha miundo ya methali na misemo ya *Arrow of God* kunatokea kuwa misemo na methali hizi hazijibainishi kama methali wala misemo katika Kiswahili. Kwa upande mwingine, mtafsiri anahitaji kufafanua ujumbe katika methali na misemo ambao una uhusiano wa karibu na utamaduni ila hapa pia mara kwa mara anakumbana na changamoto nyingine ambayo ni ukosefu wa maneno au kauli linganifu katika Kiswahili hivi kwamba analazimika kutumia maneno au kauli zinazokaribiana zaidi na zile za Ki-Igbo.

### **2.3. Mikakati ya kutafsiri methali na misemo**

Kulingana na Firoozkoohi (2010) mtafsiri wa kazi ya fasihi anahitaji kusuluhisha mvutano baina ya usahihi na uzuri wa kazi tafsiri kwa kulinganisha mtindo wa kibinafsi wa lugha ya mwandishi wa LC na matumizi ya kawaida ya vipengee husika vya lugha katika LL. Kutokana na maswala haya yaliyotajwa ipo haja ya kutambua mikakati mbalimbali ya tafsiri inayotumiwa katika tafsiri ya methali na misemo. Mapendekezo mbali mbali yametolewa kuhusiana na swala zima la kutafsiri methali na vile vile kutafsiri vipengee vilivyofungamana na utamaduni. Mapendekezo ya Newmark (1988) ni msingi muhimu sana katika kusuluhisha tatizo la ukosefu wa ulinganifu wa methali na misemo katika LL. Tafsiri ya methali na misemo katika *Arrow of God* iliyofanywa na Shamte inadhihirisha matumizi ya mikakati hii kwa njia mbalimbali inavyodhihirika katika mifano ifuatayo:

#### **2.3.1 Mikakati wa uhawilishaji**

Hii ni mbinu ambayo kimsingi ni sawa na ukopaji, hutumika pale neno au kundi la maneno kutoka LC huchukuliwa bila kubadilishwa kwa njia yoyote ile na kuingizwa katika LL. Mikakati huu pia umetambuliwa na wataalamu wengine ambao wametumia istilahi tofauti kuurejelea, kwa mfano, Pedersen (2005: 4) anauita mikakati huu, “ubakizaji” huku, Petrulione (2012: 45) anataja “udumishaji” na urudiaji” kama baadhi ya majina yanayotumika kurejelea mikakati huu. Kulingana

na Newmark, mkakati huu ni mwafaka kwa majina halisi ya watu, mahali, majina ya anwani za kazi zisizotafsiriwa miongoni mwa maneno mengine, kwa mfano neno *nte* katika methali *An animal more powerful than nte was caught by nte's trap* Katika *Arrow of God* (kuanzia hapa na kuendelea tutatumia AOG) ukurasa (kuanzia hapa kuendelea tutatumia kifupisho uk.) 144 limetafsiriwa kwa mbinu hii. *Mnyama mwenye nguvu zaidi ya nte alinaswa na mtego wa nte katika Mshale wa Mungu* (kuanzia hapa na kuendelea-MWM) uk. 126.

### 2.3.2 Mkakati wa utohozi

Mkakati mwingine kulingana na Newmark (1988) ni utohozi ambao kimsingi ni kukopa neno kisha kulibadilisha neno hilo la LC lililokopwa na kulifanya lichukue sifa za kimofolojia za LL na hivyo kutamkwa kama neno la lugha lengwa. Mbinu hii imetumika katika msemu *The king's Kolanut returns to his hands* katika AOG (uk.97) ambapo neno kolanut limetoholewa na kuwa, Kola katika tafsiri *Kola ya mfalme hurudi mikononi mwake* (MWM uk.84.)

### 2.3.3 Mkakati wa usawazishaji

Mkakati huu umekusudiwa kuziba pengo linalotokea pale ukosefu wa ulinganifu unapotokea, baadhi ya mbinu huweza kutumiwa kuleta usawazishaji huu; mbinu hizi ni pamoja na kuweka neno la kitamaduni katika LL katika nafasi ya neno la kitamaduni katika LC. Katika mbinu hii mtafsiri anaweza kutumia methali au msemu wa LL unaofanana kimaana na methali au msemu katika LC ila fani hizi zinatofautiana kimuundo. Kwa mfano, Akuakalia akiwa njiani kuelekea Okperi na wenzake anawaambia kuwa watakapofika Okperi wakumbuke “...*kufunga midomo*” (MWM uk.18) yao na kumwachia azungumze na wenyeji wa Okperi kwa sababu ni watu wagumu kusemezwa. Msemu huu ni tafsiri ya kauli, “...*to hold your tongues in your hand*” (AOG uk. 21). Katika kufanya hivi mtafsiri amefaulu kutafsiri msemu huu kwa njia kwamba mbali na kudumisha mtindo, amefaulu kutafsiri ujumbe kwa ufasaha. Usawazishaji vilevile unaweza kuafikiwa kupitia kwa mtafsiri kutafsiri methali na misemo kutumia maana ya kiuamilifu ambapo neno lisilofungamana na utamaduni hutumiwa ili kutoa maana iliyokusudiwa. Mbinu hii inajitokeza katika methali *If a man says yes, his chi also says yes* (AOG uk.29). Katika tafsiri ya methali hii neno la kitamaduni *chi*, limetafsiriwa kuwa *mungu* inavyojitokeza katika tafsiri ya methali hii, *Mtu akisema ndiyo, mungu wake husema ndiyo vilevile* (MWM uk.25)



#### **2.3.4 Mkakati wa viziada.**

Katika mkakati huu, maneno ya ziada huongezewa katika methali au misemo husika ili kuweka wazi maana. Tafsiri ya aina hii hufanywa kwa njia zifuatazo; kwa kutoa maana elezi au maana fafanuzi ambapo mtafsiri hutoa maelezo linganifu kwa maneno tofauti kubainisha maana au kwa kutoa tanbihi, viziada na maelezo mafupi. Mbinu hii inahusisha kuongeza ujumbe wa ziada unaohitajika katika maneno ya kitamaduni, maneno ya kitaaluma na yale ya lugha. Baadhi ya Methali katika AOG zimetafsiriwa kwa kutumia mbinu hii.

#### **2.3.5 Muungano wa mbinu za tafsiri.**

Mkakati wa muungano wa mbinu, huhusiana na hali ambapo mtafsiri hutumia zaidi ya mbinu moja kutafsiri methali au msembo mmoja. Newmark (1988) anapendekeza kuwa mtafsiri anaweza kutumia mbinu mbili, tatu au hata nne kutafsiri kipengee kimoja, mbinu hizi huitwa: muungano wa mbinu mbili, muungano wa mbinu tatu na muungano wa mbinu nne (TY). Mfano wa mkakati huu unajitokeza katika tafsiri ya methali inayorejelewa katika usemi, *...like the lizard who fell down from the **high Iroko tree** he felt entitled to praise himself if nobody else did.* (AOG uk. 118) Methali hii imetafsiriwa kuwa *...alihisi anastahili kujisifu kama mjusi aliyeanguka kutoka kwenye **mti mkubwa** bila ya kuvunja mfupa wowote.* (MWM uk. 103) Katika tafsiri hii mtafsiri ametumia mbinu mbili ambazo ni: mbinu ya viziada na mbinu ya udondoshaji. Shamte ametoa ufafanuzi wa methali kwa kuongezea maneno “...bila kuvunja mfupa wowote,” pengine kueleza sababu inayoweza kumfanya mjusi ahisi anastahili kujigamba. Zaidi udondoshaji wa neno “Iroko unadhihirika kwa sababu neno hili lipo katika MC ila katika tafsiri limeondolewa.

#### **2.3.6 Mkakati wa udondoshaji.**

Kutafsiri kwa udondoshaji huhusiana na hali ambapo mtafsiri anadondosha tamathali au methali husika kabisa. Mtafsiri anajaribu kutoa maelezo ya maana ya tamathali kwa ulinganifu wa karibu iwezekanavyo (Baker 1992). *A man does not summon Umuaro and not set before them even a pot of palm wine* (AOG uk.145) Katika mfano huu, Ezeulu anaomba msamaha kwa kosa la kuwaita watu wa Umuaro katika mkutano bila kuwapa mvinyo kama ilivyo desturi yao, anasisitiza kosa lake kwa kutoa msembo huu. Sehemu hii inapotafsiriwa katika MWM uk. , Ezeulu anaomba msamaha vile vile ila msembo huo anaoutoa katika AOG kama njia ya kusisitiza makosa hayo yake umedondolewa, haupo.

## **2.4 Mapendekezo ya wataalamu kuhusu uteuzi wa mikakati ya kutafsiri methali na misemo**

Kwa mujibu wa mikakati iliyopendekezwa ya kutafsiri kazi za fasihi, hasa kazi zenye vipengee vya utamaduni, mtafsiri ana nafasi kubwa ya kufanya uteuzi wa mikakati atakayoitumia kutafsiri kazi anayokusudia kutafsiri Imedhihirika katika miaka ya karibuni kuwa mtafsiri ni zaidi ya fundi ambaye huhamisha maana ya matini kutoka kwa lugha moja hadi kwa nyingine kisahili, kinyume na hivyo kwa kila uchaguzi anaofanya katika tafsiri, mtafsiri ni chombo cha mabadiliko. Naude na Naude (2010) wakimrejelea Marais (2008) wanaeleza kuwa, tafsiri huhusisha mtafsiri ambaye ana mchango mkubwa katika mchakato wa tafsiri baina ya tamaduni mbili kwa sababu lugha siku zote, imefungamana na mfumo, utamaduni na mawazo ya watu wa utamaduni fulani. Kwa sababu hii basi, tafsiri haiwezi kusafiri kuelekea kwa mazingira mapya bila kubadilika kulingana na mahitaji ya mazingira hayo inamoingia, kwa upande mwingine, tafsiri itaathiri mazingira yake mapya.

Watafsiri basi ni lazima wafahamu mchango wao mkubwa katika kutimiza mabadiliko kupitia kwa uchaguzi, unaoongozwa na maswala yaliyo nje ya lugha, wanaoufanya katika mchakato mzima wa tafsiri. Kulingana na Naude na Naude (2010), Marais (2008) anaangazia zaidi mbinu mbili ambazo mtafsiri anaweza kutumia mojawapo katika kutafsiri umbo la matini. Katika mbinu moja umbo la matini hutafsiriwa jinsi lilivyo bila kufanyiwa mabadiliko yoyote, hivi kwamba matokeo huwa ni matini inayoonekana ya kigeni. Mbinu hii ndiyo inayojitokeza katika tafsiri ya methali na misemo aliyoifanya Shamte. Njia ya pili umbo la matini halitafsiriwi na badala ya kutafsiri umbo, kauli za kitamaduni za LL zinazolingana na kauli za kitamaduni za LC hutumika katika nafasi ya kauli za LC.

Kulingana na Xizhi ZHANG (2014) akirejelea mawazo ya Toury kuhusiana na nadharia ya wingimifumo ambayo hudai kuwa tafsiri hudhibitiwa na kanuni za tafsiri anasema kuwa, kama waendeshaji wakuu wa shughuli ya tafsiri, watafsiri wanaweza kutumia mikakati mbali mbali katika kazi ile ile inayohitaji kutafsiriwa. Xizhi ZHANG akimrejelea Toury anasema kuwa, mtafsiri si lazima afuate mpangilio uliopo kwa ukamilifu; maamuzi yake yanaweza kumfanya kuufuatilia mpangilio uliopo kulingana na kanuni au kukosa kufanya hivyo. Sababu za mtafsiri kufanya hivyo hutofautiana kulingana na ama kiwango ambacho mtafsiri anathamini ujumi wa kazi anayoitafsiri au mahitaji ya kipekee katika usomaji wa kazi hiyo. Kwa kuzingatia swala hili

la mitazamo ya kihisia na kimionjo katika tafsiri Xizhi ZHANG anasema kwamba Toury anaweka tafsiri katikati ya maswala mawili; kwa upande mmoja, kuna uzingatiaji wa kanuni na katika upande ule mwingine kuna maswala ya upekee na unafsi wa mwandishi wa MC au mtafsiri. Athari ya kanuni katika hali hii hutegemea nafasi yao katika hali hii ya mvutano baina yake na upekee na unafsi wa mwandishi wa MC. Jambo lingine la kuzingatia katika maamuzi ya tafsiri ni jukumu ambalo tafsiri inakusudiwa kufanya. Watafsiri wa kazi za fasihi, hutafsiri kazi ambazo zimeteuliwa kutafsiriwa na kuzifanya ziwepo katika fasihi ya Kiswahili. Maamuzi ya uteuzi wa kazi za kutafsiriwa hufanywa kulingana na kanuni za matayarisho, kwa mujibu wa Toury (1980), ambazo hudhibiti maamuzi hayo ya ni kazi gani itakayotafsiriwa kwa kuzingatia sababu ya kufanyia kazi fulani tafsiri. Kwa kuwa katika kutafsiri kazi za fasihi, watafsiri hawatafsiri lugha tu bali pia utamaduni uliofungamana na lugha; hasa katika kazi zenye methali na misemo kama kiungo cha kimsingi. Ipo haja ya watafsiri hao kufanya tafsiri kwa makini ili kutimiza lengo la tafsiri. Azma ya tafsiri, kulingana na Landers (2001) ni uchapishaji, anasema:

Tafsiri kwa ajili ya kujifurahisha au kama zoezi la kiakili ni nzuri, lakini mtafsiri aliyejitolea hulenga katika kuwafikishia wasomaji wa LL matokeo ya tafsiri, wasomaji ambao bila tafsiri kamwe hawangewahi kuipata kazi hiyo.  
(TY)

Landers (2001) anavyodai ni sahihi kabisa kwani tafsiri hufanywa kwa azma moja kuu, kuwafikishia wasomaji wa LL kazi husika ya fasihi katika LC. Kazi ambayo haiwezi kuwafikia pasipo na tafsiri. Basi ikiwa sababu ya tafsiri ni kufikisha ujumbe wa mwandishi wa MC, ipo haja ujumbe huo umfikie msomaji wa LL kwa usahihi na ukamilifu iwezekanavyo; la sivyo, tafsiri haina maana wala haihitajiki. Tulitangulia kutaja kwamba, dhamira ya mwandishi wa *Arrow of God*, ni kueleza utamaduni wa Ki-Igbo katika kipindi fulani cha kihistoria; ujumbe huu utamfikia msomaji kwa usahihi tafsiri ikifanywa kwa makini. Newmark (1998) anasema kuwa lugha ya kifasihi ni sharti ibaki ikivutia kiujumi na lazima daima kuwepo na mvutano baina ya majukumu mawili ya lugha, jukumu la kufahamisha na lile la kiujumi. Kadri matini ilivyo nyeti, kimaadili na kiujumi, ndivyo inavyohitaji kutafsiriwa kwa usahihi na iktisadi, ili kudhihirisha mawazo, mtindo na misisitizo ya kazi asilia kwa kadri iwezekanavyo. Anaendelea kusema kuwa, tahadhari inafaa kufanywa katika kutafsiri maneno na kauli zenye maana zaidi ya moja ili kubainisha maana zao na kudumisha maneno yaliyorudiwarudiwa ambayo kwa kawaida ni maneno msingi katika kauli

husika. Wakati mwingine hutokea haja ya kutohoa jazanda za kitamaduni, wakati mwingine pia kunatokea haja ya kubadilisha majina halisi ya kibunifu ili maana zao ziwe zimetafsiriwa na muundo wa LC udumishwe kwa tendo hili.

Larson (1984) anasema kuwa, maana kwa ujumla wake imefungamana na utamaduni, na kwa sababu hii kila jamii huelewa ujumbe kwa muktadha wa utamaduni wao. Hadhira lengwa hufasiri tafsiri kulingana na utamaduni na tajriba yao na wala sio kulingana na tajriba na utamaduni wa mwandishi wa matini chanzi. Mtafsiri basi lazima asaidie hadhira lengwa kuelewa ujumbe na lengo la MC kwa kutafsiri akizingatia tamaduni zote mbili. Mtazamo huu wa kutafsiri kwa kuzingatia utamaduni wa LL na wa LC umerejelewa na baadhi ya waandishi kama, tafsiri ya kitamaduni. Kwa mfano, Shuttleworth & Cowie (1997) wanadai kuwa, tafsiri ya kitamaduni hujali maswala ya kitamaduni na ya lugha na huchukua maumbo mbalimbali kama vile kuwasilisha ML kwa hali ambayo inawafahamisha wasomaji kuhusu vipengee vya utamaduni chanzi, au kutafuta maneno au kauli katika LL ambazo inaaminika zina ulinganifu wa kitamaduni na maneno au kauli zinazotafsiriwa kutoka kwa LC.

Kulingana na Nida & Taber (1969) tafsiri ya kitamaduni ni tafsiri ambayo inapofanywa, ujumbe unabadilishwa na kufanywa ulingane na utamaduni lengwa kwa njia fulani na katika tafsiri hii huenda ujumbe ukaongezewa ambao haujitokezi katika lugha kwenye MC; Katika muktadha wa tafsiri ya Biblia Nida & Taber (1969) wanataja kuwa tafsiri ya kitamaduni ni ile ambayo inapofanywa nyongeza hufanywa ambazo hazibainiki katika maneno ya MC, hizi nyongeza huwa ni mawazo ambayo kitamaduni ni mageni kwa MC au nyongeza tu za kutoa maelezo ambayo hufafanua ujumbe usio wazi. Mtafsiri ambaye anatumia mtazamo wa kitamaduni anatambua kwamba kila lugha imesheheni vipengee ambavyo vimetokana na utamaduni wake, kwamba kila matini imekitwa katika utamaduni mahususi. Ufahamu huu, huifanya rahisi kutambua kuwa tafsiri ni mchakato unaotokea baina ya tamaduni bali sio tu baina ya lugha. Yapo maneno ambayo ni ya kipekee, kwamba ni viwakilishi vya utamaduni fulani. Maneno haya yalirejelewa na Newmark (1988) kama maneno ya kitamaduni. Mengi ya maneno haya ya kitamaduni, kulingana na Newmark ni rahisi kuyatambua kwa kuwa yanahusishwa na lugha maalum na hayawezi kutafsiriwa kwa njia ya moja kwa moja. Hata hivyo, desturi nyingi za kitamaduni huelezwa kwa

lugha ya kawaida ambapo tafsiri ya moja kwa moja huweza kupotosha maana. Hivyo basi tafsiri inaweza kuwa na maelezo amilifu na mwafaka yenye ulinganifu.

Newmark anaendelea kueleza kuwa, mambo machache ya jumla huhusika katika kudhibiti tafsiri ya maneno ya kitamaduni. Jambo la kwanza na la muhimu zaidi linafaa kuwa kutambua hatua za kitamaduni zilizofikiwa na jamii ambazo zimerejelewa katika matini ya LC na heshima iliyotolewa kwa nchi zote za kigeni na tamaduni zao katika kazi hiyo ya fasihi iliyosheheni maswala ya kitamaduni kwa kiwango kikubwa. Jambo la pili ni kuwa kwa kawaida mikakati miwili ya tafsiri ambayo inakinzana huwepo; uhawilishaji, ambao kwa kawaida huwasilisha rangi na mguso wa mazingira ya nyumbani mwa MC. Hata hivyo, uhawilishaji, kwa ufupi wake hufungia uelewa wa msomaji, badala yake husisitiza utamaduni na kufungia nje ujumbe, na kwa njia hii huzuia mawasiliano. Kwa upande mwingine kuna uchanganuzi wa vipengee ambao ni mkakati mwafaka zaidi wa kutafsiri ambao hufungia nje utamaduni na kubainisha ujumbe. Uchanganuzi wa vipengee, umejikita katika kipengee ambacho kinalingana baina ya LC na LL ambacho kinaweza kuongezewa viziada vinavyoonyesha tofauti za kimuktadha. Udhaifu wa mbinu hii ni kuwa inahusisha kutumia maneno mengi na hupoteza athari ya kazi asilia.

Hivyo basi mtafsiri wa neno la kitamaduni ambalo kwa kawaida huwa halijafungamana na muktadha kama ilivyo lugha ya kawaida, anafaa kuzingatia motisha ya uandishi, kiwango cha kudhihirisha utamaduni na kiwango cha usomekaji wa kazi tafsiri. La muhimu kuzingatia katika kutafsiri hatua kwa hatua, ni kuwa kwa kila kipindi cha wakati, kiwango cha uaminifu katika uelewekaji na tafsiri ya matini za fasihi hutofautiana katika sehemu tatu; ya mwandishi, msomaji, na matini yenyewe. Hivyo basi mtafsiri wa kazi ya fasihi anafaa kuelewa mbinu muhimu za tafsiri na maswala yanayojitokeza kutokana na mbinu hizo.

Usomi wa tafsiri katika miaka ya karibuni unaonyesha kwamba kuna msisitizo katika muungano wa kudhibiti na kuupa sura mpya ufahamu wa kitamaduni. Naude na Naude (2010), akimrejelea Connolly (2008) anadhihirisha kuwa mwelekeo wa kitaaluma wa magharibi unapunguza na kupotosha utamaduni simulizi wa ujuzi asilia wa Ki-Afrika kwa kiasi kwamba utamaduni wa kiafrika unapoteza thamani yake asilia na halisi. Kuachwa nje kwa vipengee vya utamaduni simulizi vinavyojitokeza katika MC kunawasilisha ufahamu wa utamaduni ulioegemea upande

mmoja. Nel (2008) anaonyesha kuwa lugha na utendaji, hasa tafsiri ina nafasi kuvunja zile nguvu banifu za tamaduni za kizungu ili kuhudumia jamii ya Kiafrika. Methali za kitamaduni ni akiba muhimu ya ujuzi wa kitamaduni. Tafsiri ya methali basi lazima zizingatie ujuzi wa kitamaduni wa utamaduni chanzi na vilevile utamaduni lengwa. Ili kuelewa methali vyema, aina tatu za maana zinazolingiliana zinahitaji kushughulikiwa. Aina ya kwanza ya maana inahusu maana ya kileksika. Hii ni maana ya kimsingi kabisa. Kiwango cha pili cha maana kinahusisha msingi wa kitamaduni na umaanisho wa methali hiyo.

Kiwango cha tatu cha maana kinahusu umuhimu na uamilifu wa kipragmatiki wa methali, yaani kile ambacho methali inajaribu kutimiza katika jamii. Tafsiri ya neno kwa neno kutumia mbinu ya kufanya matini iwe ngeni inaweza kuwa mwafaka kwa kitabu cha kiakademia ambapo kuwakilisha umbo maalum la methali ni muhimu. Ili kuelewa maana na uamilifu wa methali. Hata hivyo ili kuelewa maana na uamilifu wa methali itahitaji kuongezewa aya ndefu ambayo itadhihirisha viwango vyake mbalimbali vya maana ya lugha na kitamaduni. Mkakati unaozua ugeni kwa tafsiri hata hivyo hautakuwa wa msaada iwapo mtu angetaka mzungumzaji wake kuelewa maana ya kipragmatiki ya methali au hata kutambua methali kama methali. Ingawa mbinu hii ya matumizi ya kauli ambazo ni maelezo ni muhimu katika kuunganisha utamaduni chanzi na utamaduni lengwa hakuna moja kati ya kauli hizi inajitokeza kama methali katika LL na hakuna moja kati yao inayoweza kukufanya kazi kama methali. Methali za Kiswahili kwa kawaida huwa fupi zilizojitosheleza, na huwa na muundo maalum unaosheheni sifa za kishairi kama vile ruwaza sawa za sauti, takriri na mahadhi. Ingawa maelezo kama hayo hubainisha viwango vya kitamaduni na vya kipragmatiki katika methali, matokeo yenyewe si methali-methali ni lazima iwe toshelevu na iwe na mfumo wa mahadhi na sauti sawa. Kutafsiri methali ya lugha chanzi kwa njia inayokubalia methali iliyotafsiriwa kutumika kama methali ni lazima methali hiyo ichukue umbo la methali ya lugha lengwa, ni lazima ifanywe kuwa na sifa za LL. Njia ya tatu basi ya kutafsiri huhusisha ubadilishaji wa methali hiyo kuchukua sifa za LL kiasi kwamba inachukua umbo la methali ya utamaduni wa LL huku ikidumisha sehemu za maana za ya methali asilia.

Mbinu nyingine ya kufanya methali iwe na sifa za LL inahusu kutumia methali ya LL inayopitisha maana ya kipragmatiki inayokaribia maana ya LC. Ingawa katika kufanya hivi muundo na jazanda za methali asilia hupotea pamoja na ladha ya kitamaduni ya utamaduni wa LC, uelewa wa msomaji

wa ML huwa umeboreshwa kwa kuwa atakuwa anasoma ML yenye utamaduni anaouelewa. Swala la ulinganifu wa tafsiri litokeapo, na mtafiti akauliza kama kwa kufanya tafsiri ambayo itasababisha MC ichukue sifa za lugha na utamaduni wa ML na kupoteza sifa za lugha na za utamaduni wa LC; nadharia ya wingimifumo itakuwepo kuondoa utata kwa kufafanua kuwa katika hali kama hiyo, tafsiri imepewa nafasi ya pembeni na utamaduni na LL zikachukua nafasi ya katikati. Kutokana na maelezo haya, tafsiri haina makosa ila imeegemea kwenye LL zaidi ya kwenye LC. Ila tafsiri inapoegemea katika utamaduni na lugha ya MC, tatizo hutokea kwa kuwa tafsiri kama hiyo hudunisha utamaduni na lugha ya matini lengwa na hivyo kubana ujitokezaji wa uhalisia wa kitamaduni wa utamaduni wa LL.

Maoni haya ya wataalamu yanapelekea utafiti huu kuchukua mwelekeo muhimu kwa kazi hii, kwamba katika kutafsiri methali na misemo katika AOG, mtafsiri alihitajika kufanya tafsiri ambayo ingedumisha jukumu muhimu la methali na misemo ambalo ni kubainisha utamaduni wa Ki-Igbo ambao unajitokeza katika MC ambayo ni AOG.

## **2.5 Hitimisho**

Achebe ni mwandishi ambaye amefaulu sana katika kuwasilisha utamaduni wa Ki-Afrika kupitia kwa fani mbali mbali hasa kupitia kwa methali na misemo katika riwaya ya *Arrow of God*. Utamaduni ni jumla ya hali na vitu vyote anavyotagusana navyo mwanajamii yeyote katika maisha yake tangu kuzaliwa, kuishi, kufa hata kuzikwa kwake. Utamaduni unaweza kuainishwa katika kategoria tatu, utamaduni wa mazingira ya kiikolojia, utamaduni wa kijamii na utamaduni wa nyenzo. Methali na misemo mbalimbali katika *Arrow of God* zimesheheni kategoria hizi za utamaduni. Mtafsiri wa kazi za fasihi zenye methali na misemo kama viwakilishi vya utamaduni hukumbana na vizingiti mbalimbali vikiwemo, uelewa finyu wake kama mtafsiri kwa kazi yake, mtafsiri kutoelewa utamaduni wa LC na LL vyema na tofauti kubwa za kitamaduni baina ya LC na LL. Ipo mikakati mbalimbali inayoweza kutumiwa katika kusawazisha tofauti za kitamaduni katika tafsir. Mikakati hii ni pamoja na, uhawilishaji, utohozi, tafsiri iliyokubalika, usawazishaji, udondoshaji, mungano wa mbinu, utohozi na viziada. Hata hivyo mtafsiri sharti achukue mtazamo wa tafsiri ya kitamaduni kulingana na lengo la tafsiri ili kufaulisha kazi yake na kumfikishia msomaji ujumbe jinsi ulivyokusudiwa na mwandishi wa MC. Tafsiri hata hivyo huweza kutofautiana, kwa sababu kuna tofauti baina ya matini zinazotafsiriwa, tofauti katika sababu za kutafsiri, tofauti za wasomaji wanaolengwa na zile za mapendeleo ya watafsiri.

## SURA YA TATU

### TAFSIRI ZA METHALI NA MISEMO INAYOWAKILISHA UTAMADUNI WA MAZINGIRA YA KIIKOLOJIA KATIKA *ARROW OF GOD*, ZINAVYOJITOKEZA KATIKA *MSHALE WA MUNGU*.

#### 3.0 Utangulizi

Vipengee vya utamaduni wa mazingira ya kiikolojia vinajitokeza katika lugha inayohusiana na dhana za kiikolojia. Dhana hizi zinajumuisha: wanyama, ndege, wadudu, majira, mimea pamoja na maumbile kama vile: mawe, mvua na kitu chochote kile kinachotokea katika maeneo ambapo binadamu anaishi, na binadamu ana athari au mchango mdogo sana katika kuwepo kwake. Mazingira huwa na mchango mkubwa katika utamaduni wa watu wa jamii fulani kwa kuwa kazi wanazofanya hutegemea mazingira yao, maskani na mastakimu yao na hata vyakula vyao hutokana na haya mazingira. Misemo na methali mbalimbali zinazotaja vipengee hivi vya utamaduni zinaashiria jinsi binadamu anavyokabiliana na kuhusiana na mazingira yake kwa mapana na marefu yake na kwa njia ya kibunifu hutumiwa ili kueleza mawazo au falsafa zinazowaongoza wanajamii. Katika kuwazia kwa undani vipengee vya mazingira ya kiikolojia vinavyojitokeza katika methali na misemo, busara iyojificha humo hudhihirika na kutimiza lengo la mtumizi wa fani hizo. Lengo la mtumizi huyu linaweza kuwa, kusisitiza ujumbe fulani ili kukumbusha mtu kuhusu jambo fulani, kusuta au hata kumtia motisha katika mwelekeo fulani. Mazingira ya kiikolojia yamejitokeza katika viwango mbalimbali katika *Arrow of God* kukiwemo na methali na misemo inayoangazia wanyama, ndege, wadudu na maumbile ya nchi.

Mara nyingi, sehemu ya maumbo ya methali na misemo huwa ni dhana zilizoelzewa kwa mafumbo yanayotokana na jazanda zinazotumika ili kurejelea tabia au hali fulani za binadamu katika jamii. Jazanda kwa kawaida hutokana na sifa za kipekee za istilahi zinazotumiwa kijazanda, hivyo basi, dhana nyingi ambazo ni majina ya wanyama, ndege, majira, wadudu, mimea, na maumbile mengine zinatumiwa kwa sababu ya sifa fulani zinazoangaziwa katika kubuni methali au misemo mahususi. Dutta (2010) anasema kuwa, usimulizi katika riwaya ya *Arrow of God* unashirikisha ishara za kuvutia, jazanda na tashbihi, baadhi zinazodhihirisha mandhari ya Kiafrika. Anaendelea kusema kuwa, baadhi ya maelezo yanavyojitokeza katika usimulizi huo yanadhihirisha kwa uwazi kabisa mimea inayomea katika eneo la ki-jiografia ambapo wanaishi Wa-Igbo. Dhana hizi zinajitokeza pia katika methali, kwa mfano, *whoever sent his son up the palm to gather nuts*



*and then took an axe and felled the tree?* (AOG uk. 233) ambayo imetafsiriwa kuwa, *nani anaweza kumtuma mwanawe akaangue nazi kisha akachukua shoka na kuukata ule mti?* (MWM uk. 205) Methali hii inataja mimea kama vile *palm* ambao ni *mtende* (ingawa Shamte ameutafsiri kuwa *nazi*) ambao kimsingi ni kiwakilishi cha mazingira ya kiikolojia. Katika msemu, *I shall slap okro seeds out of your mouth* (AOG uk.156) uliotafsiriwa na Shamte kuwa, *nitakutoa mbegu za okro kutoka mdomoni mwako* (MWM uk.136) unadhihirisha mmea ambao una matunda yenye mbegu zinazofanana na meno yaliyovunjika. Kwa kutumia misemo kama hii pamoja na methali zinazohusisha dhana za kimazingira mwandishi anawasilisha taswira ya mazingira ya kiikolojia ya Wa-Igbo na zaidi kupitisha maswala ya kifalsafa ya jamii husika. Maswala haya ya kifalsafa huwa ndio ujumbe unaosisitizwa katika methali au misemo na hujitokeza katika kufafanua sifa za dhana za kimazingira zilizotumiwa kijazanda katika muktadha wa matumizi ya fani husika.

### 3.1. Tafsiri ya methali zinazohusiana na wanyama

Jedwali lifuatalo lina orodha ya baadhi ya methali na misemo tutaliyojadili na ambayo kwa njia moja au nyingine inahusiana na wanyama kama sehemu ya mazingira ya kiikolojia katika *Arrow of God* pamoja na tafsiri zake kama zinavyojitokeza katika *Mshale wa Mungu*.

	Methali na misemo inayohusiana na wanyama kama inavyojitokeza katika <i>Arrow of God</i> .	Tafsiri ya methali na misemo kama inavyojitokeza katika <i>Mshale wa Mungu</i> .
1	<i>A toad does not run in the day unless something is after it. (uk.21)</i>	<b>Chura</b> hakimbii mchana mpaka awe anafuatwa na kitu. (uk.18)
2	<i>Did you expect what the leopard sires to be different from leopard? (uk.76)</i>	Ulitaraji alichozaa <b>chui</b> kitofautiane na chui (uk. 65)
3	<i>When an adult is in the house, the she-goat is not left to suffer the pains of parturition on its tether. (uk.18)</i>	Mtu mzima akiwa ndani ya nyumba hamwachi <b>mbuzi jike</b> asembuliwe na tumbo la uzazi huku amefungwa (uk.16)
4	<i>He whose name is called again and again by those trying in vain to catch a wild bull has something he alone can do to bulls. ( uk.228)</i>	Yeye ambaye jina lake huitwa tena na tena na wale wanaojaribu bila ya kufanikiwa kumkamata <b>fahali</b> , basi ana kitu ambacho yeye pekee anaweza <b>kumfanyia fahali</b> (uk.201)

5	<i>If the lizard of the homestead should neglect to do the things for which its kind is known, it will be mistaken for the <b>lizard of the farmland.</b> (uk.18)</i>	<i>Ikiwa <b>mjusi wa nyumbani</b> ataghafilika asifanye mambo yampasayo afanye, atadhaniwa ni <b>mjusi wa shamba.</b> (uk.15)</i>
6	<i>The person who sends a child to catch a <b>shrew</b> will also give him water to wash his hand (uk. 212)</i>	<i>Mtu amtumae mtoto akamkamate <b>panya mdogo</b>, lazima pia amtafutie maji ya kuoshea harufu mbaya kwenye mikono yake (uk.186)</i>
7	<i>An animal more powerful than <b>nte</b> was caught by <b>nte's</b> trap (uk.144)</i>	<i>Mnyama mwenye nguvu zaidi ya <b>nte</b> alinaswa na mtego wa <b>nte</b> (uk.126)</i>

Kuna methali na misemo mingi katika *Arrow of God* inayohusiana na wanyama mbali mbali wa mwituni na vilevile wanyama wa kufugwa wakiwemo: *chura, chui, mbuzi fahali, panya, mjusi, ng'ombe, panya buku, kobe, nyani* miongoni mwa wanyama wengine ambao wamerejelewa katika methali na misemo katika riwaya hii. Baadhi ya wanyama hawa walioorodheshwa, wanapatikana katika tamaduni nyingine mbali na ule wa Igbo, ukiwemo utamaduni wa Kiswahili, kwa hivyo ni kipengee cha utamaduni kilicho na ulinganifu kwa kiasi kikubwa na tamaduni nyingine. Wanyama wanaorejelewa, au kutajwa katika methali na misemo ya jamii yoyote ile, wana sifa za kipekee ambazo zimechochea kubuniwa kwa methali na misemo hii na wametumiwa kijazanda ili kuwakilisha tabia na sifa za binadamu. Kwa mfano, tukiangazia methali, *a toad does not run in the day unless something is after it. (AOG.uk. 21)*, methali hii imetafsiriwa na Shamte kuwa, *chura hakimbii mchana mpaka awe anafuatwa na kitu (MWM uk.18)*. Bila shaka methali hii inatokana na sifa za chura, kwamba yeye ni mnyama ambaye hutoka mafichoni kutafuta chakula usiku na kulala mchana ila kunapotokea hatari, au chura anapokuwa anafukuzwa na kitu fulani ndipo tu anaweza kuonekana akikimbia mchana. Kulingana na Awa na Ngele (2014), maana asilia ya methali hii ni kuwa hakuna kitu kinachotokea bila sababu. Methali hii imetumiwa na Uduezue mzee mmoja katika kijiji cha Okperi ambaye pia ni mjomba wa Akuakalia. Akuakalia na vijana wenzake wawili walikuwa wametumwa na wazee kutoka Umuaro waende Okperi kuwataka watu wa Okperi kuchagua kati ya vita au amani baina yao na Umuaro. Jamii hizi mbili zilikuwa na mzozo wa ardhi na watu wa Umuaro hawakuwa tayari kuachilia ardhi ile kwa watu wa Okperi ingawa, kulingana na Ezeulu, ardhi ilikuwa ya Okperi na wala si Umuaro. Akuakalia na wenzake wanapofika kwa Aduezue ambaye alichukuliwa kama mjomba wa Akuakalia, anatumia methali

hii anapowaona, kwa kuwa walikuwa wamefika Okperi mapema mno; na nyuso zao zilivyoonekana zilimtia wasiwasi. Kwa kutumia methali hii Aduezue ana maana kuwa kulikuwa na jambo lisilo la kawaida na kama inavyojitokeza kwenye muktadha Aduezue hakutarajia wageni kutoka Umuaro na hasa mtoto wa dadake (anavyomwita Akuakalia) kuwatembelea asubuhi na mapema kiasi hicho. Katika muktadha huu, Aduezue anaendelea kusema kuwa, mamake Akuakalia (dadake Aduezue) angekuwa hai, angejua kwamba jambo baya limempata; ila dadake alikuwa tayari ameaga dunia kabla, kwa hivyo Aduezue ana wasiwasi kutaka kujua kilichomleta mwana huyo wa dadake kwake mapema hivyo.

Tafsiri ya methali hii imefanywa kwa njia ya moja kwa moja. Ingawa ujumbe wa mwandishi unaweza kueleweka kwa kuwa wasomaji wa Kiswahili wanaelewa na wanawafahamu vyura na sifa zao kwa kuwa wanawaona katika mazingira yao mara kwa mara na hivyo kufahamu tabia na sifa zao. Tafsiri hii imepoteza mtindo kwa kuwa tafsiri inajitokeza kama maelezo, methali imepotea. Pengine, mbinu nyingine ambayo angetumia mtafsiri ni kutumia methali ya Kiswahili yenye maana linganifu na methali hiyo ya Ki-Igbo, kwa mfano angetumia methali *pafukapo moshi pana moto* au hata *dalili ya mvua ni mawingu*. Kwa kutumia methali linganifu mtafsiri angefaulu katika kudumisha ujumbe wa methali katika MC kwenye ML na pia kudumisha sifa za kimuundo za MC, ila kuna kiungo muhimu ambacho kingepotea, nacho ni taswira ya kitamaduni inayotokana na istilahi za kitamaduni za lugha ya MC zinazoachwa nje na kwa nafasi zao, huingia istilahi za kitamaduni za lugha ya ML. Ili kudumisha kipengee husika cha kitamaduni, pengine Shamte angefinyanga tu tafsiri aliyoitoa kwamethali hii, lakini aifinyange tafsiri hiyo ili ichukue muundo wa methali ya Kiswahili. Kwa mfano angetafsiri methali hii kwa kusema, *ukiona chura anakimbia mchana jua anafuatwa na kitu*.

Hali sawa na hii iliyojadiliwa vile vile inajitokeza katika methali nyingine ambayo ni *did you expect what the leopard sires to be different from leopard?* (uk.76) ambayo imetafsiriwa kuwa *ulitaraji alichozaa chui kitofautiane na chui* (MWM uk. 65). Methali hii imetumiwa na Ugoye mmoja wa wake wa Ezeulu (mamake Oduche) kumrejelea bintiye wa kambo anayelitwa Adeze. Kwa kutumia methali hii Ugoye anadai kwamba, Adeze ni katili kama babake (Ezeulu). Haya yanatokana na Adeze kumuuliza Ugoye swali la kejeli, kwamba alikuwa (Adeze) amesikia kuwa mamake huyo wa kambo anawafundisha wanawe kuua na kula chatu. Adeze alikuwa anarejelea

tendo la Oduche kumfungia chatu wa Idemili (mungu mmojawapo wa Ki-Igbo) kwenye sanduku akijaribu kumuua sawa na alivyohimizwa katika kanisa la Wakristo. Ili kudumisha mtindo wa kazi ya fasihi, Shamte angetumia methali ya Kiswahili, *mwana wa nyoka ni nyoka* kulingana na mapendekezo ya wataalamu mbalimbali wa tafsiri ya fasihi. Kwa kutumia methali ya Kiswahili kama hii yenye ulinganifu wa maana; mtafsiri hufaulu sio tu kuwasilisha maana bali kudumisha mtindo kwa kuwa methali hii haiwezi kupotea kama ilivyopotea pale alipotumia tafsiri ya moja kwa moja iliyofanya methali ipoteze mtindo wake na kutokea tu kama maelezo ya kawaida. Ingawa mbinu hii ya tafsiri ingefaa katika miktadha mingine, haifai katika muktadha wa kutafsiri methali na misemo katika AOG. Madai haya yanatokana na hali kuwa tafsiri ya aina hii inasababisha kupotea kwa taswira ya kitamaduni inayowasilishwa na jazanda ya nyoka katika methali ya Ki-Igbo. Hivyo basi kuna haja ya kutafsiri kwa kutumia mbinu ambayo mbali na kupitisha ujumbe wa methali hii, pia itadumisha maudhui makuu ya utamaduni. Mbinu hii inaweza kuwa tafsiri ya maana za kileksika iliyopewa umbo la methali na misemo ya Kiswahili. Pengine mtafsiri angetafsiri methali hii kuwa, *chui huzaa chui*, ili kujaribu kutimiza mahitaji ya tafsiri ya methali hii katika muktadha wa matumizi na uamilifu wake.

Mnyama mwingine ambaye anajitokeza katika methali ni *Mbuzi (she goat)*. Mbuzi ni mnyama wa kufugwa ambaye muda mwingi huwa amefungwa kwa kamba ili kumdhibiti asije akafanya uharibifu wa mimea fulani mashambani au hata nafaka. Mbuzi hukua na kukomaa na akishakomaa hutarajiwa kuzaa wanambuzi wakati fulani katika maisha yake. Mbuzi anapokuwa katika uchungu wa uzazi, na hali hii itokee wakati ambapo kuna mtu mzima karibu, mtu huyo humfungua mbuzi ili kumpa nafasi nzuri kukamilisha shughuli hiyo ya uzazi. Mambo huwa tofauti inapotokea kuwa walio karibu na mbuzi mwenye uchungu wa uzazi ni watoto kwa sababu inawezekana hata wasitambue tatizo la mbuzi huyo na hivyo wanamwacha katika matatizo maradufu. Ukweli huu wa kitamaduni umechangia katika kubuniwa kwa methali hii. *When an adult is in the house, the she-goat is not left to suffer the pains of parturition on its tether (AOG uk.18)*, ambayo imetafsiriwa kuwa, *mtu mzima akiwa ndani ya nyumba hamwachi mbuzi jike asembuliwe na tumbo la uzazi huku amefungwa (MWM uk.16)*. Ezeulu anajaribu kuwashauri wazee wa Umuaro kwamba msimamo wao kuhusu ardhi yenye mzozo utaleta taabu na hivyo watumie busara yao ili kuzuia vita na watu wa Okperi. Methali hii ni wito kwa wazee wa Umuaro kwenye kikao kutumia busara yao ili kuzuia vita na wenzao wa Okperi. Kulingana na Ezeulu, iwapo vita vingetokea watu wa

Umuaro wangeshindwa na kuumizwa sana kwa sababu hawangepata msaada wa Ulu (mungu wao) ambaye hawezi kushiriki vita vyenye ila kama hivyo. Umuhimu wa busara ya wazee ni imani ya kitamaduni iliyo na ulinganifu katika Kiswahili na kuna methali na misemo ya Kiswahili ambayo ingetumika katika tafsiri, kwa mfano, *palipo na wazee, hapaharibiki neno*. Hata hivyo mtafsiri kwa mara nyingine tena ametafsiri kiufafanuzi na kupoteza ladha ambayo ingedumishwa iwapo angetumia methali ya Kiswahili badala ya maelezo katika kutafsiri. Lakini, kama tulivyotangulia kutaja, kutumia methali linganifu ya Kiswahili katika nafasi ya methali ya Ki-Igbo kutapoteza jazanda muhimu zinazotokana na wanyama waliotajwa kwenye methali za Ki-Igbo na hivyo kupoteza mandhari ya kitamaduni yanayowasilishwa na wanyama hao. Hivyo basi inabidi mtafsiri kuwa mbunifu zaidi na kutafsiri kwa kutumia mbinu ambayo itadumisha mandhari hayo bila kuathiri mvuto unaotokana na methali au msemu kwa kufinyanga maelezo na kuyapa sifa za methali na misemo ya Kiswahili. Kwa mfano anaweza kutafsiri methali hii kuwa *mtu mzima akiwa nyumbani, mbuzi hasumbuliwi na tumbo la uzazi kifungoni*.

Methali *he whose name is called again and again by those trying in vain to catch a wild bull has something he alone can do to bulls* (uk. 228) imetumiwa na Aneto akijaribu kumshawishi Obika kusaidia kufanya shughuli ya kitamaduni maarufu miongoni mwa Wa-Igbo kama *Ogbazulobodo* kwa ajili ya babake Aneto (Amalu) aliyekuwa amekufa. Shughuli hii hufanyika wakati ambapo mtu ameaga dunia na mtu mwenye tajriba katika shughuli hii (kama aliyokuwa nayo Obika) hukimbia huku akilumba ulumbi ambao kimsingi ni muungano wa methali na misemo mingi ya Ki-Igbo. Obika anajaribu kukataa jukumu hili kwa sababu anajihisi mgonjwa na kupendekeza mtu mwingine afanye kazi hiyo. Aneto anamjibu kwa msemu huu na Obika anakubali kukikimbia *Ogbazulobodo* akiwa mgonjwa, shughuli inayosababisha kifo chake. Ujumbe unaosisitizwa na methali hii ni kwamba mambo yasiyo ya kawaida hutokea kwa sababu fulani maalum na yanahitaji kuchukuliwa kwa uzito yanayostahili. Msemu huu umetafsiriwa na Shamte kuwa *yeye ambaye jina lake huitwa tena na tena na wale wanaojaribu bila ya kufanikiwa kumkamata fahali, basi ana kitu ambacho yeye pekee anaweza kumfanyia fahali* (uk.201). Tafsiri hii aliyoitoe Shamte haiwasilishi ujumbe kwa ukamilifu kama unavyojitokeza katika msemu asilia. Kwanza kabisa ametafsiri istilahi “*wild bull*”, kuwa, “*fahali*”. Tafsiri hii imepoteza kipengee kuwa si fahali yeyote tu anayezungumziwa, bali *fahali mkali asiyesikika kwa urahisi*. Jambo la pili, ni kwamba ametafsiri sehemu *...has something he only can do to bulls* kuwa *...ana kitu ambacho yeye pekee*

*anaweza kumfanyia fahali.* Tafsiri hii imepoteza ,kwa kiasi fulani,msisitizo muhimu kuhusu, kwanza uwezo wa kipekee wa mtu huyo anaeyeitwa na wenzake kuhusiana na shughuli anayoitiwa, na pili, kwa kusema “*kumfanyia fahali,*” mtafsiri ameondoa dhana ya wingi ambayo ni muhimu kwa kuwa inaonyesha kuwa sio kuwa ana uwezo kwa huyo fahali anayezungumziwa pekee bali fahali wote. Pengine tafsiri mwafaka ya moja kwa moja ingekuwa *Yeye ambaye jina lake huitwa tena na tena na wale wanaojaribu bila mafanikio kumkamata fahali mkali ana kitu fulani ambacho ni yeye tu anaweza kuwafanyia fahali.*

*Mijusi (lizards)* nao ni wanyama ambao hupatikana katika maeneo mengi ulimwenguni, na kuna mijusi wa aina mbali mbali ambao huishi katika mazingira tofauti kulingana na maumbile yao, bila shaka sifa hii imechochea kubuniwa kwa methali; *if the lizard of the homestead should neglect to do the things for which its kind is known, it will be mistaken for the lizard of the farmland (uk.18).* Ezeulu anapotumia methali hii kwa wazee wa Umuaro anajaribu kuwaeleza kwamba wamepuuza wajibu wao kama wazee. Wazee wanatarajiwa kutoa mashauri ya busara, na katika muktadha huu, Ezeulu alitarajia kuwa wazee wangemuunga mkono na kupinga wazo la kuanza vita dhidi ya wenzao wa Okperi ila walionekana kutojali. Anatoa methali hii akiwasilisha kutoridhika na busara yao kama wazee; alikusudia kuwachochea kubadilisha msimamo wao. Shamte ametafsiri methali hii kuwa, *ikiwa mjusi wa nyumbani ataghafilika asifanye mambo yampasayo afanye, atadhaniwa ni mjusi wa shamba* (uk.15). Tafsiri hii ni potovu kwa sababu imewasilisha ujumbe visivyo kwa kuwa ametafsiri neno *neglect* ambalo lina maana ya *kupuuza* kuwa *kughafilika*. Neno ‘kughafilika’ kama ilivyotumika na Shamte, limeleta dhana ya kusahau ama kufanya jambo bila kukusudia. Kwa kufanya hivi methali hii imemfikia msomaji wa Kiswahili ikiwa na maana kuwa wazee hawa walisahau kufanya wajibu wao, badala ya kueleweka aliyokusudia mwandishi kuwa walikataa kufanya walivyotarajiwa kwa mapuuza. Mtafsiri angetumia tafsiri kama *ikiwa mjusi wa nyumbani atatelekeza kufanya mambo ambayo mijusi wa nyumbani hujulikana kufanya, atachukuliwa kimakosa kuwa mjusi wa shamba.*

Anichebe Uzeodo, ni mmoja wa wazee wa Umuaro wanaofika kwa Ezeulu, kumwomba ale viazi vyote vilivyosalia, na ambavyo vilimzuia kutangaza mwanzo wa msimu wa kuvuna viazi, katika hiyo siku moja ili atangaze mwanzo wa msimu huo. Kwa sababu Ezeulu alikuwa amechelewa kutangaza mwanzo wa msimu wa kuvuna, viazi vilikuwa tayari mashambani lakini watu walikuwa na njaa kwa sababu hawakuwa na ruhusa kuvuna mpaka Ezeulu atangaze kwamba wana ruhusa

ya kufanya hivyo. Hali hii inamfanya Anichebe kutoa pendekezo la kutafuta njia ya mkato kwa jambo hili. Ezeulu anamkumbusha kuwa ni makosa kwake (Ezeulu) kufanya hivyo na akijaribu wanaweza kuadhibiwa na Ulu. Anichebe anamjibu kwa msemu, *the person who sends a child to catch a shrew will also give him water to wash his hand (uk. 212)*. Anachokusudia kusema Anichebe ni kwamba yeye na wazee wenzake wanaomtuma Ezeulu kula viazi vyote kinyume na masharti, watachukua lawama na adhabu yoyote itakayotokana na kosa hilo. Methali hii inasisitiza kuwa mtu anapofanya jambo, lazima awe tayari kwa matokeo ya jambo hilo analolifanya. “Shrew” ni mnyama mdogo kama panya ila ana mdomo mrefu, na kama njia ya kujisalimisha kutoka kwa maadui zake, mnyama huyu hutoa harufu kali ya uvundo kutoka tumboni mwake ili kujikinga dhidi ya maadui zake. Ni muhimu kutambua kuwa huyu panya anayezungumziwa si panya wa kawaida. Shamte anatafsiri methali hii kuwa *mtu amtumae mtoto akamkamate panya mdogo, lazima pia amtafutie maji ya kuoshea harufu mbaya kwenye mikono yake (uk.186)* Katika tafsiri hii msomaji wa Kiswahili hawezi kuelewa harufu inayozungumziwa kwa sababu panya wa kawaida awe mdogo au mkubwa hawezi kuachia mtoto amshikaye harufu mikononi, hivyo basi kuna haja ya kutoa maelezo kamili ambayo yatamfanya msomaji huyu kuelewa maana ya methali hii kwa usahihi. Kwa mfano angesema, *mtu amtumaye mtoto akamkamate panya mdogo mwenye harufu mbi, lazima pia amtafutie maji ya kuoshea harufu mbi kwenye mikono.*

Mbali na wanyama hawa waliojadiliwa kuna mnyama ambaye amerejelewa kwa Ki-Igbo bila kutafsiriwa kwa Kiingereza, mnyama anayeitwa **nte** katika msemu, *an animal more powerful than nte was caught by nte’s trap (AOG uk.144)* ambayo imetafsiriwa kuwa *mnyama mwenye nguvu zaidi ya nte alinaswa na mtego wa nte (MWM uk.126)*. Methali hii imetumiwa na Akuebue, kurejelea hali ya Ezeulu baada ya kushindwa kutangaza msimu wa kuvuna viazi, kwao wanajamii wengine wa Umuaro, hali hii ilikuwa juhudi za Ezeulu kuwaadhibu. Tofauti na wanajamii wenzake, kwa Akuebue hali hii ilikuwa sawa na mnyama mkubwa kuliko **nte** kukamatwa kwa mtego wa **nte**, kwa maana kwamba jambo kubwa kushinda lililotarajiwa lilikuwa limetokea na Ezeulu hajui namna ya kulisuluhisha; jambo aliloliona kuwa dogo sasa limekuwa kubwa kupita kiasi. Kabla ya kujikuta katika hali hii Ezeulu alihisi kuwa uwezo wake kama kasisi wa Ulu ni mkubwa sana akataka kutumia nafasi yake kuadhibu watu wa Umuaro, baadaye anajiona kuwa kama mshale tu katika uta wa miungu ambao hauna uwezo wowote ila kwenda popote utakapoelekezwa. Tafsiri ya methali hii imefanywa kwa ufafanuzi ila neno la Ki-Igbo ‘**nte**,’

ambalo limesumishwa katika tafsiri. Sawa na tafsiri zilizojadiliwa awali methali hii imepoteza muundo wake na ikaishia kuwa maelezo tu ambayo yanawasilisha kwa kiasi fulani utamaduni wa LC. Mbinu hii ya tafsiri ingekuwa mwafaka zaidi iwapo mtafsiri angetoa tanbihi kueleza maana ya neno **n**te ili kuwezesha uelewa sahihi wa msemu huo kwa msomaji wa Kiswahili.

### 3.1.1 Methali na misemo inayohusiana na ndege

Jedwali hili ni orodha ya methali na misemo inayohusiana na ndege pamoja na tafsiri zake kulingana na Shamte katika *Mshale wa Mungu*;

<i>Methali na misemo inayohusiana na ndege kama inavyojitokeza katika Arrow of God.</i>		<i>Tafsiri ya methali na misemo kama inavyojitokeza katika Mshale wa Mungu</i>
1	<i>Do you blame a <b>vulture</b> for perching over a carcass? (uk.9)</i>	<i>Unamlaumu <b>tai</b> kwa kutua juu ya mzoga (uk. 8)</i>
2	<i>The offspring of a <b>hawk</b> cannot fail to devour <b>chicks</b> (uk. 130)</i>	<i>Mtoto wa <b>kipanga</b> hawezi kushindwa kukamata <b>vifaranga</b> (uk. 114)</i>
3	<i>Men of today have learnt to shoot without missing and so I have learnt <b>to fly without perching</b>. (uk.47)</i>	<i>Wanaume wa siku hizi wamejifunza namna ya kulenga shabaha bila ya kukosea, na mimi nimejifunza <b>kuruka bila ya kupumzika</b> (uk.40)</i>
4	<i>The mighty tree falls and <b>the little birds</b> scatter in the bush (uk.231)</i>	<i>Mti mkubwa unaanguka na <b>ndege wadogo</b> hutawanyika kwenye kichaka (uk.203)</i>

Methali katika *Arrow of God* imehusisha vile vile ndege, kwa mfano, katika methali *Do you blame a vulture for perching over a carcass? (uk.9)*. Methali hii inataja ‘Vulture’, ndege mla nyama ambaye ni *tai* katika Kiswahili. Methali hii imetafsiriwa na Shamte kuwa, *unamlaumu tai kwa kutua juu ya mzoga (uk.8)*. Tai ni mnyama ambaye hula nyama, hivyo akiona mzoga wa mnyama atatua juu yake kuula. Kwake Tai kutua juu ya mzoga ni kawaida na ni jambo ambalo yeye hulifanya kila mara, kwa sababu hiyo hawezi kulaumiwa kwa kufanya ambacho yeye hufanya kila wakati kujilisha. Matefi mke wa pili wa Ezeulu, anatumia methali hii kurejelea tabia ya Nwafu mtoto wa mke mwenzake, Ugoye, ya kulamba sahani baada ya kula chakula kilichopikwa na Matefi. Kulingana na madai ya Matefi, ugoye hapiki samaki kwake hivyo Nwafu hupata windo



akipata sehemu ya chakula cha babake kilichopikwa na Matefi na chenye samaki. Katika muktadha huu methali inatumiwa kueleza kuwa mtu akipata kitu akipendacho hukifurahia sana wala hakuna haja ya kumshangaa mtu huyo. Tafsiri aliyofanya Shamte kwa msemu huu inafikisha ujumbe kwa kuwa tai ni ndege ambaye hupatikana katika mazingira ya watumizi wa lugha ya Kiswahili, hivyo kwa kutafsiri kwa njia ya moja kwa moja, mtafsiri tayari amefikisha ujumbe kwa muktadha wa kitamaduni kwa kuwa msomaji wa tafsiri ya Kiswahili anajua tai na sifa zake. Pengine tokeo la tafsiri hii haliwezi kuchukuliwa kama methali, lakini mabadiliko kidogo yakifanywa, tafsiri hii inaweza kuwa na mvuto na ladha sawa na methali au misemo ya Kiswahili. Kwa mfano anaweza kusema, *tai halaumiwi kwa kutua juu ya mzoga*. Kwa kutafsiri msemu huu hivi, Shamte atadumisha sio tu ladha ya msemu huu katika Kiswahili, bali pia atakuwa amedumisha ‘tai’ na ‘mzoga’, kama viwakilishi vya utamaduni.

Oyilidie mwanamke aliyeumwa na Ojiugo bintiye Ezeulu wakati ambapo alijaribu kuwatenganisha Ojiugo na kakake wa kambo Oduche walipokuwa wanapigana, anatomia methali *the offspring of a hawk cannot fail to devour chicks* (uk.130). Kwa kusema hivi Oyilidie analinganisha Ojiugo na mamake Matefi katika masuala ya utukutu. Bila shaka methali hii imeshawishiwa na sifa za kipanga ambaye hula vifaranga. Inatarajiwa kuwa mwana wa kipanga vile vile atakula vifaranga. Methali hii imetafsiriwa kuwa *mtoto wa kipanga hawezi kushindwa kukamata vifaranga* (uk. 114). Kwa mara nyingine tena, ujumbe kuwa kinachozaliwa na kitu, huchukua sifa za mzazi wake unadhihirika. Katika tafsiri hii, japo ni ya moja kwa moja, methali imedumishwa kwa kuwa muundo wa methali hii ni sawa na muundo wa methali za Kiswahili. Hata hivyo, ujumbe umepotoshwa kwa kiwango fulani pale ambapo mtafsiri ametafsiri “cannot fail to devour chicks”, kuwa, “hawezi kushindwa kukamata vifaranga”. Maana hapa inakuwa tofauti na iliyokusudiwa. Tafsiri mwafaka kwa maneno haya inaweza kuwa, *hakosi kuwala vifaranga*. Kwa hivyo tafsiri ya methali nzima inaweza kuwa, *mtoto wa kipanga hakosi kuwala vifaranga*.

Ndege mmoja ambaye anaitwa *Eneke-nti-oba* anarejelewa katika methali *Men of today have learnt to shoot without missing and so I have learnt to fly without perching* (uk.47), ambayo imetafsiriwa kuwa *wanaume wa siku hizi wamejifunza namna ya kulenga shabaha bila ya kukosea, na mimi nimejifunza kuruka bila ya kupumzika* (uk.40). Kulingana na Achebe, katika *Arrow of God* (uk. 47), ndege anayeitwa *Eneke-nti-oba* ndiye anasema maneno haya hata hivyo methali hii

imerejelewa tu katika maelezo wala haijatajwa kikamilifu, vinginevyo methali hii huwa, *Eneke the bird said, men of today have learnt to shoot without missing and so I have learnt to fly without perching*. Ezeulu anajilinganisha na Eneke kwa kumtuma mwanawe Oduche kujifunza dini mpya ya Kikristo. Methali hii inasisitiza kuwa mtu awe na busara katika kutenda mambo ili asijikute kwa matatizo. Labda methali hii inaweza kutafsiriwa kwa maelezo yaliyo katika muundo wa methali za Kiswahili kwa mfano, *ndege Eneke alisema kwamba, kwa kuwa wanaume wa kisasa wamejifunza kulenga shabaha bila kukosa, nami nimejifunza kuruka bila kutua*. Kisha tanbihi itolewe kufafanua sifa za ndege Eneke-nti-Oba kwa msomaji wa Kiswahili ambaye vinginevyo hawezi kujua sifa za ndege huyu.

Mbali na ndege hawa ambao wametajwa kwa majina yao, wapo wengine ambao wametajwa tu, kwa mfano *little birds (ndege wadogo)* katika methali *the mighty tree falls and the little birds scatter in the bush (uk. 231)* ambayo inatajwa na pepo wa usiku wakati wa Ogbazulobodo Methali hii imetafsiriwa kwa njia ya moja kwa moja kuwa *mti mkuu huanguka na ndege wadogo hutawanyika vichakani (uk 203)*. Methali hii inatokana na hali kuwa mti mkuu kwa kawaida huwa ndio masikani ya ndege wengi wadogo ambao hujenga viota vyao katika majani ya mti ule. Mti huu unapoanguka ndege hawa hupoteza makao yao na hivyo kutawanyika. Methali hii ina methali linganifu katika maneno na maana ambayo inaweza kutumiwa katika kutafsiri badala ya tafsiri ya Shamte ambayo imejitokeza kama maelezo tu methali hii ni *mti mkuu ukianguka, ndege huwa mashakani*.

### 3.1.2 Methali na misemo inayohusiana na wadudu.

<i>Methali na misemo inayohusiana na wadudu kama inavyojitokeza katika <b>Arrow of God</b>.</i>		<i>Tafsiri ya methali na misemo kama inavyojitokeza katika <b>Mshale wa Mungu</b></i>
1	<i><b>White ant</b> chews Igbegulu because it is lying on the ground; let him climb the palm tree and chew (uk.230)</i>	<i><b>Siafu mweupe</b> anatafuna Igbegulu kwa sababu ipo njiani, mwache apande juu ya mnazi na autafune (uk.203)</i>
2	<i>The <b>fly</b> that has no one to advise it follows the corpse into the grave. (27).</i>	<i><b>Inzi</b> asiyekuwa na wa kumshauri hufuata maiti kaburini (uk 23)</i>

Methali na misemo ya Ki-Igbo, haijaacha nyuma wadudu katika maumbo yao, baadhi ya wadudu ambao wametajwa ni kama, *siafu mweupe (white ant)* katika methali *White ant chews Igbegulu because it is lying on the ground; let him climb the palm tree and chew (AOG. uk.230)*. Methali hii imeshawishiwa na sifa za *siafu mweupe* anayeishi mchangani na anaweza kuharibu chochote kilicho karibu na mchanga kwenye ardhi lakini hawezi kupanda miti mirefu kama mnazi kuitafuna. *Igbegulu* ni shina la mnazi katika Igbo, na *siafu mweupe* ambaye hutambaa chini hutafuna shina la mnazi hasa linapokuwa limekatwa na kulala chini kwa sababu ni rahisi kulifikia. Methali hii imetumiwa na Obika wakati wa *Ogbazulobodo* ambaye ni pepo wa usiku; anaghani methali nyingi zenye mafunzo huku akikimbia katika njia mahususi kijijini. Methali hii inakejeli watu wanaowadharau wenzao wanapokuwa miongoni mwao bila kujua wao ni nani hasa na kwa kutowajua wana wadharau watu ambao ni wenye uwezo mkubwa kuwashinda wao wenyewe. Tafsiri ya methali hii imejitokeza kuwa, *siafu mweupe anatafuna Igbegulu kwa sababu ipo njiani, mwache apande juu ya mnazi na autafune (MWM uk. 203)*. Mtafsiri ametumia tafsiri ya neno kwa neno, hata hivyo, anapofikia neno *Igbegulu*, amelihawilisha. Neno hili ni geni kwa msomaji wa Kiswahili. Mbali na kufanya hivyo neno *ground* limetafsiriwa kuwa *njiani*, jambo ambalo limepotosha maana. Kutafsiri kwa mbinu hii kumeifanya methali hii, sio tu kupoteza sifa zake kama methali bali hata ujumbe haumfikii msomaji ambaye kwanza hatatambua *Igbegulu* na zaidi ameelekezwa vibaya kuwa *Igbegulu* imelala *njiani* na wala sio *ardhini*. Ingekuwa bora kujaribu mbinu ya tafsiri ambayo itapunguza athari mbaya zilizotokea katika tafsiri hii pengine angetumia methali ya Kiswahili, yenye maana linganifu kwa mfano *usione wembamba wa reli, gari moshi hupita*. Lakini kutumia methali hii ya Kiswahili kutapoteza utamaduni uliowasilishwa kwenye

methali katika LC, na kwa sababu hii, ni bora kutumia tafsiri ya moja kwa moja; na maelezo yatakayojitokeza, yabadilishwe ili kuondoa sifa za methali za kigeni, yaani sifa za Ki-Igbo. Badala yake maelezo haya yatolewe kwa njia itakayoyafanya kujitokeza kama methali ya Kiswahili. Ili kupunguza tofauti za kitamaduni, mtafsiri anaweza kutoa tanbihi yenye maana ya istilahi ya Ki-Igbo, *Igbegulu* baada ya tafsiri.

Nzi (fly) ambaye ni mdudu anayependa mazingira yenye uchafu, uozo na uvundo, kwa mfano, palipo na maiti aliyeoza na kuwa na uvundo; amerejelewa katika methali *The fly that has no one to advise it follows the corpse into the grave (AOG uk.27)*. Methali hii imetumiwa kubainisha umuhimu wa washauri katika jamii kwa kuwa wanaweza kumuokoa mtu ambaye yupo kwenye hatari asiyoitambua, sawa na nzi kwenye maiti asiye na habari kwamba maiti huyo anaelekea kuzikwa. Hali hii ya nzi huenda ikamsababishia kuzikwa pamoja na maiti jambo linaloweza kusababisha kifo chake. Methali hii imetafsiriwa kuwa, *Inzi asiye na wa kumshauri hufuata maiti kaburini (MWM uk.23)*. Tafsiri hii inadhahirisha muundo sawa na wa methali za Kiswahili na hivyo inaweza kukubalika kama tafsiri mwafaka, ila masahihisho ya neno ‘nzi’ ambalo limeendelezwa kuwa ‘inzi’ yafanywe.

### 3.1.3 Methali na misemo inayohusiana na majira

	<i>Methali na misemo inayohusiana na majira kama inavyojitokeza katika <b>Arrow of God</b>.</i>	<i>Tafsiri ya methali na misemo kama inavyojitokeza katika <b>Mshale wa Mungu</b>.</i>
1	<i>Greeting in the <b>cold harmattan</b> is taken from the fireside. (uk.116)</i>	<i>Kumsalimu mtu <b>wakati wa baridi</b> kunakuwa karibu ya moto (uk.101).</i>

Majira hayajajitokeza kwa wingi katika methali na misemo katika *Arrow of God*, hata hivyo katika methali *Greeting in the cold harmattan is taken from the fireside (uk.116)* dhana ‘harmattan’ imejitokeza ambayo kimsingi ni upepo uvumao katika maeneo ya Afrika Magharibi katika kipindi mahususi cha mwaka. Upepo huu wa ‘harmattan’ huleta baridi kali katika eneo hili ambapo Wa-Igbo huishi na hivyo kuwaathiri kwa kuwasababishia baridi kali, ndiposa methali hii ambayo imetafsiriwa kuwa *Kumsalimu mtu wakati wa baridi kunakuwa karibu ya moto (uk.101)*. Wakati wa baridi itokanayo na ‘Harmattan’, watu huketi karibu na moto kuuota ili kukabiliana na baridi na hawapedi kutoka karibu na moto hata kupokea salamu, ila anayewasalimu hulazimika kusonga karibu na moto ule ili kuwapa salamu zake. Akuebue anamwambia Ezeulu methali hii huku akirudi

katika kazi yake ya kutayarisha mbegu za viazi, baada ya kuviacha ili akamwamkue rafikiye Ezeulu. Alichomaanisha Akuebue ni kwamba, itabidi Ezeulu aseme naye akiwa anaendelea na kazi yake. Mtafsiri kwa mara nyingine ametoa maelezo kwa Kiswahili, na katika kufanya hivyo ameondoa kipengee muhimu cha utamaduni wa kiikolojia, *Harmattan*. Ingekuwa bora kama mtafsiri angetafsiri alivyofanya ila atumie neno la kitamaduni la utamaduni wa Kiswahili ili kuufikisha ujumbe kwa ufasaha. Kwa mfano angetafsiri kuwa *Salamu wakati wa kipupwe, hupokelewa karibu na moto*. Tafsiri ya aina hii inaufikisha ujumbe kwa ufasaha. Hii ni kwa sababu maana iliyokusudiwa kupitishwa ni zaidi ya maana ya kileksika, ni funzo kwenye methali na linamfikia msomaji wa Kiswahili kwa njia iliyo rahisi kuelewa na sio hivyo tu, pia inadumisha mtindo kwa kuchukua umbo la methali ya Kiswahili .

### 3.1.4 Methali na misemo inayohusiana na mimea

<i>Methali na misemo inayohusiana na mimea kama inavyojitokeza katika <b>Arrow of God</b>.</i>		<i>Tafsiri ya methali na misemo kama inavyojitokeza katika <b>Mshale wa Mungu</b></i>
1	<i>Like the lizard who fell down from the <b>high Iroko tree</b> felt entitled to praise himself if nobody else did. (uk.118)</i>	<i>Alihisi anastahili kujisifu kama mjusi aliyeanguka kutoka kwenye <b>mti mkubwa</b> bila ya kuvunja mfupa wowote. (uk. 103)</i>
2	<i>A ripe <b>maize</b> can be told by merely looking at it. (uk.129)</i>	<i><b>Hindi</b> lililokomaa linajulikana kwa kulitazama tu.(uk. 113)</i>
3	<i>When mother-cow is cropping <b>giant grass</b> her calves watch her mouth.(uk.176)</i>	<i>Mama n'gombe akitafuna <b>majani makubwa</b> ndama wake huutazama mdomo wake(uk.155)</i>

Katika mazingira ya watu wa Igbo kuna mimea ambayo baadhi ni maarufu katika maeneo wanamoishi, kwa mfano, mti unaoitwa *Iroko*. Mti huu wa *Iroko* una sifa za kipekee. Kwanza ni mti unaokua na kuwa mrefu sana na humea wenyewe bila kupandwa na mtu. Kulingana na Gogoi (2017) mti huu haupandwi na yeyote na hata mtu akapanda mbegu zake, hazitamea kwa sababu ni mti uchaguao pa kumea, sawa na ulivyo ukuu miongoni mwa watu. Ingawa Wa-Igbo wanathamini umoja na ushirikiano wa kijamii vilevile wanathamini umuhimu wa kufaulu kwa mtu binafsi kama inavyodhihirika katika methali *The lizard that jumped from the high iroko tree to the ground said he would praise himself if no one else did*. Achebe anarejelea methali hii katika *Arrow of God* anapoeleza jinsi Obika alijionea fahari kwa kuwa mmoja wa vijana wachache tu ambao

hawakufanya kosa la kujuana kimwili na wapenzi wao kabla ya ndoa. Mwandishi anasema –*like the lizard who fell down from the **high Iroko tree** felt entitled to praise himself if nobody else did (uk.118)*. Bila shaka katika muktadha huu, methali hii imejikita katika sifa ya mti wa Iroko ya kuwa mti mrefu sana na mjusi aliyeruka kutoka juu yake hadi chini alijionea fahari kwa kufaulu kufanya jambo gumu kama hilo. Obika anapomwoa mkewe hatimaye, bila kujamiiana naye kabla, anahisi fahari naye mwandishi analinganisha fahari hii na ile ya mjusi aliyefaulu kuruka kutoka kwa mti mkuu wa Iroko. Ila kuna maswala kadha yanayojitokeza katika tafsiri ya Shamte kwa methali hii. Katika *Mshale wa Mungu* methali hii imetafsiriwa kuwa *alihisi anastahili kujisifu kama mjusi aliyeanguka kutoka kwenye **mti mkubwa** bila ya kuvunja mfupa wowote na akasema kuwa ikiwa hakuna mtu aliyefikiri sana kuhusu tendo hili kubwa, yeye mwenyewe alifikiri (uk. 103)*. Katika tafsiri hii, Shamte alifanya ufafanuzi wa ujumbe ulio kwenye methali kwa kiasi kikubwa sana mpaka akaiptoteza methali kabisa, hivi kwamba ni vigumu kutambua kama kuna methali inayorejelewa. Jambo la pili ni kuwa ameongeza maelezo ya ziada, ambayo ni *...bila kuvunjika mfupa wowote*. Msingi wa maelezo haya haueleweki kwa uwazi, kwa sababu maelezo haya hayapo kwenye MC wala dhana hiyo ya kuvunjika mfupa, haijitokezi kwenye methali ya LC. Kwa kuongeza maelezo yasiyo na msingi bainifu anapotosha msomaji. Jambo jingine ni kwamba ameondoa jina la mti unaorejelewa (Iroko), kwa kutaja tu mti mkubwa. Mwandishi alilitumia neno Iroko kutoa taswira ya mazingira ya kitamaduni, mti huu ni wa kipekee miongoni mwa Wa-Igbo kwa kuwa una sifa za kipekee Gogoi (2017) akirejelea Achebe (1958) katika *Things Fall Apart* anasema kuwa hakuna anayeweza kupanda mbegu za mti wa Iroko zikamea, kwa kuwa ni mti unaochagua pa kumea na kuwa mkubwa sana. Kwa kuliondoa neno hili, mtafsiri ameondoa picha hii muhimu ambayo Achebe alikusudia kuibainisha. Kwa kuwa methali hii inasisitiza umuhimu wa uvumilivu, bidii na kujitolea mhanga ili kufaulu katika maisha, labda mtafsiri angetoa tafsiri inayoweza kuchukua umbo la methali za Kiswahili. Vile vile angedumisha taswira kwa kulitafsiri neno Iroko kwa Kiswahili maana ni mmea unaopatikana katika maeneo ya uswahilini na unafahamika kama mvule. Pengine angetafsiri methali hiyo kuwa, *mjusi aangukaye kutoka juu mvule mrefu huhisi kujisifu asiposifiwa na yeyote*.

Mbali na mmea huo uliotajwa, upo mmea mwingine, *maize (mhindi)* ambao umerejelewa katika methali *A ripe maize can be told by merely looking at it (uk. 129)*. Methali hii imetumiwa na Akuebue akirejelea Edogo, mtoto wa kwanza wa kiume wa Ezeulu. Edogo anataka kuwa Kasisi

wa Ulu baada ya babake, ila anaona kuwa babake hana mipango kama hiyo. Edogo anakwenda kumtaka ushauri Akuebue, ila Akuebue anahisi kuwa Edogo hawezi kuwa kasisi wa Ulu kwa sababu ni mwoga, hata hawezi kusimama kama mwanamume aseme anachotaka kwa uwazi. Kwa kutaja methali hii Akuebue anadhihirisha kuwa mtu anayestahiki cheo fulani hujulikana kwa urahisi. Methali hii imetafsiriwa na Shamte kuwa *Hindi lililokomaa linajulikana kwa kulitazama tu (uk.113)*. Tafsiri hii ni mwafaka kwa kuwa imechukua umbo la methali za Kiswahili na vile vile inawasilisha maneno ambayo msomaji wa Kiswahili anaweza kujihusisha nayo kwa urahisi na hivyo kuyaelewa.

Baadhi ya mimea ni chakula cha wanyama kama vile ng'ombe. Mimea hii ni kama *grass (nyasi)* ambayo imejitokeza katika methali *When mother-cow is cropping giant grass her calves watch her mouth (uk.176)*. Methali hii inatokana na ukweli kuwa ndama wa ng'ombe hujifunza mambo mbali mbali kutoka kwa mama yao yakiwemo kula nyasi hasa zile kubwa kwa kumtazama kisha kumuiga. Akuebue anataja methali hii akieleza kuwa bintiye, Udenkwo, ameiga tabia mbaya ya utukutu kutoka kwa mamake. Tafsiri ya methali hii imejitokeza kuwa *Mama ng'ombe akitafuna majani makubwa ndama wake huutazama mdomo wake (uk155)*. Tafsiri hii, mbali na kupoteza methali kwa kuwa imejitokeza kama maelezo, pia inapotosha maana kwa kuwa majani sio tafsiri sahihi ya neno *grass*. Kwa kuwa kuna methali linganifu kimaana katika Kiswahili, tafsiri linganifu kimaana kwa methali hii inaweza kuwa *mtoto akibebwa hutazama kisogo cha nina*. Hata hivyo katika muktadha huu, tafsiri hii haitakuwa mwafaka kwa sababu kuna haja ya kudumisha utamaduni wa kiikolojia wa Ki-Igbo. Hivyo basi tafsiri mwafaka kulingana na muktadha huu inaweza kuwa *Mama ng'ombe anapokata nyasi, ndama wake hutazama mdomo wake*. Tafsiri ya aina hii inawezesha kuwasilisha utamaduni aliokuwa anauwasilisha Achebe katika *MWM*.

### 3.1.5 Methali zinazohusiana na maumbile.

<i>Methali na misemo inayohusiana na maumbile kama inavyojitokeza katika <b>Arrow of God.</b></i>		<i>Tafsiri ya methali na misemo kama inavyojitokeza katika <b>Mshale wa Mungu</b></i>
1	<i>Our eye sees something; we take a <b>stone</b> and aim at it. But the <b>stone</b> rarely succeeds like the eye in hitting the mark. (174)</i>	<i>Macho yanaona kitu, tunachukua jiwe na kukitunga kile kitu. Lakini lile <b>jiwe</b> si aghalabu kufanikiwi kama jicho kupiga ile alama.(uk.152)</i>
2	<i>wanting to bale water before it rises above the ankle (uk..129)</i>	<i>Kuyaondoa maji kabla hayakupita juu ya magoti. (uk .113).</i>

Jiwe pia, kama sehemu ya maumbile, linajitokeza katika methali *our eye sees something; we take a **stone** and aim at it. But the **stone** rarely succeeds like the eye in hitting the mark (AOG uk.174)* ambayo imetafsiriwa kuwa *Macho yanaona kitu, tunachukua **jiwe** na kukitunga kile kitu. Lakini lile **jiwe** si aghalabu kufaulu kama jicho kupiga ile alama (MWM uk. 52).* Methali hii imetumiwa na Akuebue, akimfariji, John Nwodika, kijana kutoka Okperi, aliyemtunza Ezeulu alipokuwa Okperi kwa mzungu. John, alikuwa anajilaumu kwa kuhusika katika Winterbottom kumuita Ezeulu Okperi na kumsababishia kukaa huko kama mfungwa kwa muda mrefu. Hata hivyo, John anaeleza kuwa alitarajia kuwa kwa kuja kwa Ezeulu Okperi, Waafrika wangepata sehemu katika mamlaka. Akuebue, anasema msemu huu akikusudia kusema kuwa binadamu huwa na matamano mengi, lakini hutimiza kidogo. Ili kudumisha mtindo, mtafsiri angeitafsiri methali hii kwa njia kwamba ichukue umbo la methali za kiswahili, kwa mfano *jiwe litupwalo kulenga kitu, aghalabu halifaulu kama macho yaliyokiona kitu hicho.*

Maji kama sehemu ya maumbile pia, yamejitokeza katika msemu uliorejelewa kama *wanting to bale water before it rises above the ankle (uk.129)* ambayo imetafsiriwa kuwa *kutaka kuyaondoa maji kabla hayakupita juu ya magoti (uk. 113).* Methali hii inatumiwa na Akuebue akimwambia Edogo kwamba alikuwa amefanya vizuri kwenda kwake. Edogo alikuwa anamtaka Akuebue kumshauri babake-Ezeulu kuhusu kosa la kumfanya mdogo wake Nwafo (kakake Edogo wa kambo) kuhisi kuwa ndiye atarithi ukasisi wa baba yao kwa kuwa ingewezekana asichaguliwe na hivyo kuzua tatizo kubwa. Msemu huu umebuniwa kutokana na hali ambapo maji huweza kuzua mafuriko na kuangamiza watu, ikiwa hayatazuiwa mapema. Unatumiwa kuonyesha umuhimu wa



kusuluhisha tatizo kabla halijawa kubwa kupita kiasi. Shamte anatafsiri msemu huu kwa njia ya moja kwa moja na kuupoteza sio tu msemu bali ujumbe kwa jumla. Shamte anataja kuwa *maji... hayakupita kwenye magoti*, kisarufi maneno haya hayaeleweki katika muktadha wa matumizi yake. Kisha ametafsiri neno ‘ankle’ ambalo ni kifundo cha mguu kwa Kiswahili, kuwa magoti ambayo yapo juu sana ya na kifundo cha mguu na kwa njia hiyo kutia chuku isiyokuwepo. Njia ya rahisi ambayo mtafsiri angetumia ni kutafsiri ujumbe kwa methali linganifu ya kiswahili kwa mfano, *usipoziba ufa utajenga ukuta*. Ila kwa kufanya hivyo mtafsiri atazua hali ambapo utamaduni uliobebwa kwenye methali hiyo katika LC utapotea hivyo basi mtafsiri anaweza kutafsiri methali hii kuwa *kutaka kuyaondoa maji kabla yafike kwenye kifundo cha mguu*, katika jaribio la kudumisha lengo la mwandishi wa MC.

### **3.2 Maswala Ibuka Kutokana na Tafsiri za Methali na Misemo Yenye Ushawishi wa Kiiojia**

Shamte ametafsiri methali na misemo inayohusiana na mazingira ya kiiojia katika riwaya ya AOG akitumia mbinu mbali mbali. Mbinu zinazodhihirika kutawala tafsiri ya methali na misemo hii ni pamoja na: mbinu ya kiufafanuzi, kimaelezo, vijalizo visivyo vya lazima, tafsiri sisisi na za moja kwa moja. Mbinu hizi alizozitumia Shamte katika kutafsiri methali na misemo inayohusiana na mazingira ya kiiojia japo kwa kiwango fulani imefikisha ujumbe wa Achebe, ujumbe huo hata hivyo haujajitokeza katika MWM alivyokusudia Achebe. Madai haya yanatokana na ukweli kuwa mfumo wa methali na misemo kama unavyojitokeza katika AOG unachukua nafasi ya katikati katika wingimifumo ya riwaya hii. Shamte anapotafsiri riwaya ya AOG, inaelekea kuwa anaitafsiri kwa ujumla wake bila kuzingatia upekee unaofaa kupewa tafsiri ya methali na misemo hasa katika AOG. Kwa hakika umuhimu wa methali na misemo katika AOG ni mkubwa sana na wa kipekee kwa kuwa ni sehemu ya kimsingi ya kimuundo na kimaudhui katika AOG. Kwa mujibu wa Dutta (2010), methali katika AOG, zimetumiwa kubainisha ujuzi wa usemaji wa Wa-Igbo. Kwa kuwa zenyewe ni ngano ndogo, methali zinawasilisha maswala changamano kwa urahisi. Dutta anaendelea kusema kuwa, methali pia zinatumiwa kutaja kwa muhtasari maswala makuu katika riwaya ya AOG; kwa mfano ulumbi wa pepo wa usiku *ogbazulobodo*, umesheheni methali kama hiyo kwa mfano methali *The fly that struts around on a mound of excrement wastes his time; the mound will always be greater than the fly* (AOG uk.230) ambayo imetafsiriwa *nzi ambaye hutambaa kwa maringo kwenye kishungu cha kinyesi anapoteza muda wake; kishungu siku zote kitakuwa kikubwa kuliko nzi* (MWM uk.202). Maana yake inaelekea kuwa na uhusiano na juhudi

za Ezeulu na watu wake kupinga dini mpya na utawala mgeni ambazo hazikufaulu. Kwa kutumia fani kama methali na misemo miongoni mwa mbinu nyingine, Achebe amefanya Lugha ya Kiingereza kuwa na “u-afrika.” Amefaulu kuibadilisha lugha ya mkoloni na kuifanya ibebe mzigo wa tajriba yake ya ki-afrika kwa kutumia ubunifu. Dutta anaendelea kusema kwamba yeyote anayesoma kazi za Achebe ambazo zimeandikwa kwa mandhari ya Nigeria anaweza kutambua kuwa kazi hizo zinaambatana na matukio yaliyotukia kiwakati.

Kulingana na Anigbogu na Ahizih (2016), Achebe anatumia lugha yake ya kipekee kuwasilisha hadithi ya mamlaka, migogoro na uongozi na uhusiano wao na historia ya jamii. Matumizi haya ya kipekee ya lugha ya Achebe yanadhihirisha nia yake ya mawasiliano. Lengo lake kuu katika kubadilisha lugha ya Kiingereza iwe na sifa za ki-afrika ni kumwezesha kuonyesha upekee katika jamii ya kitamaduni ya Ki-Igbo. Anaamua kutumia methali na ishara kufikia lengo hili la kufafanua mambo yanayoaminika kuwa kamilifu kwa Wa-Igbo, kaida zao na kuwasilisha mandhari ya kitamaduni ya Ki-Igbo. Anigbogu na Ahizih wanaendelea kueleza kuwa mbali na kuwasilisha utamaduni, matumizi ya Achebe ya methali yanaongeza uzuri wa kiafrika kwa lugha yake; yanaonyesha busara na hekima inayojitokeza wakati ambapo mwanamume wa Igbo anazungumza. Gogoi (2017) anasema kuwa kwa Achebe, methali za ki-afrika zina umuhimu mkubwa katika fasihi; matumizi yake yanadhihirisha uhalisia wa lugha asilia. Kwa mujibu wa kauli za wasomi hawa methali na misemo ina upekee wa matumizi katika AOG. Hivyo basi, ili lengo la Achebe katika AOG litimie, ni sharti methali na misemo hii itafsiriwe kwa makini. Hata hivyo kwa kuwa mbinu iliyotumika zaidi na Shamte kutafsiri methali na misemo ni mbinu ya ufafanuzi, methali imepotea. Kupotea kwa methali na misemo katika MWM kutokana na udhaifu wa mtafsiri kumeufanya ule mvuto wa lugha, unaotokana na ujumi wa utamaduni wa Afrika katika methali na misemo ya Ki-Afrika vile vile umepotea. Katika kiwango kingine maana imepotosha kutokana na viziada visivyohitajika na ambavyo vinampa msomaji ujumbe usio sahihi kulingana na MC.

### 3.3 Hitimisho

Kubuniwa kwa methali na misemo mbalimbali kumeshawishiwa na vipengee mbalimbali vya mazingira ya kiikolojia. Methali na misemo iliyomo katika AOG ina jukumu la kipekee katika kujenga maudhui na muundo wa riwaya ya AOG. Upekee huu wa matumizi ya methali na misemo unaweka fani hizi katika nafasi ya katikati katika wingimifumo ya riwaya ya AOG. Katika kutafsiri fani hizi kuna haja ya kudumisha nafasi yao kwenye ML kwa kutafsiri fani hizi kama mfumo uliojisimamia. Shamte ametafsiri methali na misemo inayohusiana na mazingira ya kiikolojia kwa mbinu mbalimbali. Zikiwemo mbinu ya kiufafanuzi, kimaelezo, vijalizo visivyo vya lazima, tafsiri sisisi na za moja kwa moja. Mbinu hizi zimefaulisha tafsiri ya Shamte kwa kiwango kidogo sana, na kwa kiwango kikubwa kupoteza ladha ya lugha ya usimulizi; Amepoteza methali na misemo kupitia kwa tafsiri ya ufafanuzi; na kupotosha maana kwa kutoa vijalizo visivyo vya lazima na udondoshaji wa dhana muhimu za mazingira ya kiikolojia. Zaidi maneno ya kitamaduni ya utamaduni wa kiikolojia wa Ki-Igbo yana ulinganifu kwa kiwango kikubwa katika Kiswahili na kufanya tafsiri ionekane rahisi. Hata hivyo kutafsiri maneno hayo kwa njia ya moja kwa moja, alivyofanya Shamte, hudumisha utamaduni wa LC ambao huenda haueleweki kwa msomaji wa LL. Ipo haja ya kutumia mbinu zinazoweza kudumisha ujumbe na vile vile mtindo wa mwandishi na zaidi kutimiza dhamira ya kuwasilisha utamaduni wa Ki-Igbo kupitia kwa methali na misemo katika AOG. Mbinu hizi ni kama vile: kutumia methali na misemo yenye ulinganifu wa maana au ujumbe na muundo, au kutoa maelezo kwa kuyafinyanga hivi kwamba yanachukua umbo la methali za Kiswahili na hivyo kujitokeza kama methali na misemo.

## SURA YA NNE

### TAFSIRI ZA METHALI NA MISEMO ILIYOSHAWISHIWA NA UTAMADUNI WA KIJAMII NA UTAMADUNI WA NYENZO KAMA ZINAVYOJITOKEZA KATIKA *MSHALE WA MUNGU*

#### **4.0 Utangulizi**

Katika sura hii kategoria mbili za utamaduni zimejadiliwa; kategoria hizi ni pamoja na: methali na misemo inayohusiana na utamaduni wa nyenzo na vilevile methali na misemo inayohusiana na utamaduni wa kijamii usio wa nyenzo. Kama anavyodai Mgbemere (2014) Utamaduni wa nyenzo hurejelea vitu vinavyoonekana, raslimali na nafasi ambazo watu hutumia kufafanua utamaduni wao. Hivi ni pamoja na makazi (maskani na mastakimu), ujirani, miji, shule, makanisa, masinagogi, mahekalu, misikiti, maafisi, viwanda, vifaa, mbinu za uzalishaji bidhaa na mazao, maghala na kadhalika. Utamaduni usio wa nyenzo kwa upande mwingine unarejelea mawazo yasiyo dhahiri waliyo nayo watu kuhusu utamaduni wao yakiwemo; imani, amali, sheria, kanuni, lugha na kadhalika. Mbali na kutumia lugha yenye methali na misemo kudhihirisha utamaduni wa kimazingira, fani hizi pia zimetumika kwa njia ya kipekee, kudhihirisha mawazo ya watu wa Igbo, hasa wazee. Kupitia kwa mazungumzo na majibizano yao. Mgogoro mkuu kwenye riwaya unadhihirika, mgogoro huu umejikita katika imani, falsafa, desturi na vifaa vya Wa-Igbo na unajitokeza katika methali ma misemo kadri unavyokuzwa na Achebe katika AOG. Anavyodai Gogoi (2017), Achebe, anatumia lugha yenye ya methali na misemo kwa wingi ili kuibadilisha lugha ya Kiingereza iseme hadithi ya Ki-Afrika kutoka kwa muonoulimwengu wa wa-afrika. Kauli hizi zinapelekea maoni kuwa, riwaya ya AOG ina upekee fulani ambao hauwezi kupuuzwa. Upekee huu unatokana na hali kuwa hadithi kuhusu Afrika, hususan kuhusu ulimwengu wa Wa-Igbo, ambayo inasimuliwa kwa njia ya kipekee hivi kwamba, ingawa inasimuliwa kwa Kiingereza; inawasilisha uafrika kama unavyochukuliwa na mwafrika. Hali hii ni kinyume na jinsi uafrika unavyochukuliwa na mtumizi asilia wa Kiingereza. Kama wanavyodai wataalamu mbalimbali ambao wamejadiliwa katika sura tangulizi, Achebe anafaulu kuwasilisha hali ya Afrika kihalisia kwa kutumia fani mbalimbali za fasihi simulizi, na kwa kiwango kikubwa, methali na misemo.

Kwa hakika, methali na misemo, anavyodai Gogoi (2017), haijanyunyiziwa tu kwenye, riwaya hii ya AOG, bali kwa ubunifu mkubwa imefinyangwa na kushirikishwa katika usimulizi kwa kiasi kuwa inaishia kuwa sehemu ya usimulizi. Methali na misemo inatumika na wahusika hasa wazee kuonyesha busara yao na kukuza migogoro mikuu katika hadithi. Migogoro hii inadhihirika kwa uwazi zaidi katika methali na misemo kwa kuwa ni kupitia kwa fani hizi', ambapo imani za kishirikina, imani za kidini, itikadi za jamii, maadili, busara, desturi na shughuli mbalimbali za jamii ya Wa-Igbo hujitokeza. Mbali na maswala haya ya kijamii, methali na misemo vile vile hushirikisha nyenzo mbali mbali za jamii zinazotumika katika shughuli anuwai na maisha ya kila siku ya Wa-Igbo. Hadithi ya Waigbo inakamilika kwa kusimuliwa katika miktadha ya kiikolojia, nyenzo na maswala ya kijamii ya Ki-Igbo ambayo inajenga taswira muhimu zinazodhihirisha utamaduni wa ki-afrika.

Inadhihirika kuwa methali na misemo imetumiwa kuwasilisha mambo ya kimsingi katika usimulizi wa Achebe, mambo haya yamekutanishwa kwa mfinyango changamano na wa kibunifu wa mifumo mbalimbali ambayo inaingiliana sana. Sawa na tulivyotaja awali, mtafsiri wa methali na misemo hii anapokuwa katika mchakato mzima wa kazi yake anapaswa kutambua kila mfumo ulio kwenye riwaya anayotafsiri. Mifumo hii ni pamoja na lugha, fani za lugha, utamaduni ambao pia ni muungano wa mifumo ya vipengee vya utamaduni vinavyowakilishwa na methali hizi. Baada ya kutambua mifumo hii mbali mbali, mtafsiri anapaswa kuzingatia nafasi ya kila mfumo katika wingimifumo anayotafsiri kisha ahakikishe kuwa mifumo hiyo imefikishwa katika LL kwa ulinganifu. Kama anavyodai Toury (1980), nafasi ya mifumo katika wingimifumo inafaa kumwongoza mtafsiri katika kutafsiri mifumo hiyo kulingana na kanuni mwafaka kwa wakati huo.

#### **4.1. Utamaduni wa Nyenzo.**

Kategoria hii ya utamaduni inajumlisha zana zote za jamii pamoja na vitu au vifaa vya utenda kazi, mapambo, nakshi na kadhalika vilivyoundwa na mwanadamu kama vifaa vya kazi, ujenzi wa maskani na mipangilio yao kimuundo na kiuamilifu, vyakula—kukijumuishwa majina ya vyakula, taratibu zao za maandalizi, sababu, mbeko na miiko ya chakula, miongoni mwa nyenzo nyingine. Utamaduni huu unajibainisha katika baadhi ya methali na misemo ya Ki-Igbo katika AOG na ni mfumo muhimu katika kujenga mgogoro mkuu, ambao ni ushindani baina ya utamaduni wa Ki-Igbo na ule wa kikoloni. Kwa mfano methali *When suffering knocks at your door and you say*

*there is no seat left for him, he tells you not to worry because he has brought his own stool* (AOG uk.87) inatimiza jukumu hili. Methali hii imetafsiriwa kuwa *Mateso yakija na kugonga mlango wako na wewe ukisema huna pa kukaa, anakwambia kuwa usijali maana mekuja na kiti chake mwenyewe* (MWM uk.75). Kupitia kwa methali hii, Achebe anadhihirisha hisia za baadhi ya wazee wa Umuaro kuhusu wazungu waliokuwa wamewakera baadhi ya vijana wa Umuaro. Methali hii inatumiwa na mhusika Moses Unachukwu aliyekuwa tayari ameshakuwa mfuasi wa dini ya mzungu na kujifunza lugha yake. Unachwuku anawashauri vijana kukubali kuwa mzungu alikuwa tayari miongoni mwao na hangeondoka karibuni bali badala ya kuondoka angeuharibu utamaduni wa Umuaro kabisa. Methali hii inawasilisha hali hii ya mgogoro kwa njia inayochora taswira mawazoni mwa msomaji na kubainisha kiwango cha kutoelewana kwa kutumia maneno machache. Vile vile methali na misemo katika AOG, inasadia katika kujenga migogoro mingine midogo kama vile kutoelewana baina ya Ezeulu kasisi wa Ulu na baadhi ya wanajamii, hasa Nwaka, kasisi wa Idemili ambao muda wote walikuwa katika ushindani miongoni mwa migogoro mingine. Vifaa mbalimbali vinavyojitokeza ni ishara za shughuli, busara amali, itikadi na imani mbalimbali kwa jumla za Wa-Igbo na vinachangia kwa kiwango kikubwa katika kuchora taswira ya utamaduni wa Ki-Igbo na jamii kwa jumla.

#### 4.1.1 Methali na misemo inayohusiana na Vifaa vya kazi.

<i>Methali/Misemo kama inavyojitokeza katika AOG</i>		<i>Tafsiri ya Methali / Misemo kama inavyojitokeza katika MWM.</i>
<b>1</b>	<i>Wisdom is like a goatskin bag; every man carries his own. (uk.16)</i>	<i>Busara ni kama mkoba wa ngozi ya mbuzi; kila mmoja huchukua wake (uk.14)</i>
<b>2</b>	<i>What man would send his son with a potsherd to bring fire from a neighbour's hut and then unleash rain on him? ( uk.233)</i>	<i>Mtu gani angeweza kumtuma mwanawe akachukue moto kwa jirani na halafu akamnyeshea mvua? (uk.205)</i>
<b>3</b>	<i>When suffering knocks at your door and you say there is no seat left for him, he tells you not to worry because he has brought his own stool (uk.87)</i>	<i>Mateso yakija na kugonga mlango wako na wewe ukisema huna pa kukaa, anakwambia kuwa usijali maana amekuja na kiti chake mwenyewe (uk.75)</i>
<b>4</b>	<i>Whoever sent his son up the palm to gather nuts and then took an axe and felled the tree? (uk. 233)</i>	<i>Nani anaweza kumtuma mwanawe akaangue nazi kisha akachukua shoka na kuukata ule mti? (uk.205)</i>
<b>5</b>	<i>The man who has never submitted to anything will soon submit to the burial mat. (uk.11)</i>	<i>Mtu ambaye hajapata kuitikia chochote, ghafla hutikia mkeka wa kuzikiwa (uk.10)</i>

Katika utamaduni wa Igbo sawa na ilivyo katika tamaduni nyingine, watu hushiriki katika shughuli mbalimbali. Shughuli hizi za wanajamii zinaweza kuwa za kiuchumi au shughuli za kijamii wanazoshiriki kwa raha zao. Mara kwa mara shughuli hizi huhitaji vifaa mbalimbali ili kufanya kazi zao, baadhi ya vifaa vya kazi miongoni mwa Wa-Igbo, vimejitokeza katika methali na misemo katika Arrow of God. Vifaa hivi ni pamoja na vifuatavyo; *mkoba wa ngozi ya mbuzi, kigae, shoka, Mkeka wa kuzikiwa, kiti* miongoni mwa vifaa vingine.

Methali *Wisdom is like a goatskin bag; every man carries his own.* (AOG uk. 16) inalinganisha busara na kifaa kimoja maarufu sana miongoni mwa Wa-Igbo ambacho huchukuliwa kama sehemu ya mavazi ya wanaume wa Igbo. Kifaa hiki kinachorejelewa ni *goatskin bag* (*mkoba uliotengenezwa kwa ngozi ya mbuzi*). Methali hii imetafsiriwa na Shamte kuwa *Busara ni kama mkoba wa ngozi ya mbuzi; kila mmoja huchukua wake* (MWM Uk. 14). Katika utamaduni wa Ki-Igbo kila mwanamume hubeba mkoba ulioundwa kwa ngozi ya mbuzi na ni desturi ambayo imekuwepo kwa muda mrefu. Methali hii imetumiwa na Nwaka kasisi wa Idemili ambaye alikuwa adui mkubwa wa Ezeulu. Katika kutumia methali hii, Nwaka anapinga ushahidi wa Ezeulu kuwa ardhi yenye mzozo ilikuwa ya Okperi kihalali na madai haya ni kulingana na Ezeulu alivyosimuliwa na babake. Kwa usemi huu Nwaka anasema kuwa babake Ezeulu hakujua alichokuwa anakisema kwa hivyo wasikitilie maanani. Methali hii imetafsiriwa kwa njia ya moja kwa moja na Shamte. Msomaji wa MWM huenda akapata changamoto kubwa katika kuelewa usemi huu kwa sababu mbili; Kwanza kutafsiri kwa njia ya moja kwa moja, kunaweza kumkanganya msomaji asiyelewa mkoba wa ngozi ya mbuzi vizuri na hasa unavyotumiwa kitamaduni. Methali hii imeshawishiwa na hali kuwa miongoni mwa Wa-Igbo, kila mwanamume hubeba mkoba wa ngozi ya mbuzi na kwa kulinganisha busara na mkoba huu, basi Nwaka anajaribu kusema kuwa kila mmoja anafaa kutumia busara aliyo nayo bila kutegemea busara ya mwingine. Anajaribu kusisitiza kuwa, watu tofauti wana haki ya kuwa na mielekeo tofauti kuhusu jambo moja. Msomaji wa tafsiri ya usemi huu katika Kiswahili huenda asiuelewe ulinganishi huu kwa urahisi kwa sababu dhana hii ni ya kigeni mno kwake. Jambo la pili linalofanya iwe vigumu kwa msomaji wa MWM kuupata ujumbe wa methali hii ni makosa ambayo mtafsiri amefanya katika kutafsiri neno “*carries*”. Shamte ametafsiri neno hili kuwa “*huchukua*” neno lenye maana zaidi ya moja. Hali hii inafanya msomaji kutatizika katika kuamua maana iliyokusudiwa baina ya maana ya kutoa kitu kilipo na kubeba kitu kutoka sehemu moja hadi nyingine. Ujitokezaji huu wa

methali hii katika tafsiri unapoteza ladha ya kitamaduni iliyokusudiwa na Achebe alipoamua kutumia methali hii. Sio hivyo tu, bali muundo wa methali hii katika Kiwahili ni wa kauli ya kawaida, au maelezo ya kawaida. Mtafsiri angetumia mbinu ya kutafsiri methali ya methali linganifu iliyopendekezwa na Newmark (1988), angetafsiri methali hii kwa kutumia methali ya Kiswahili *Akili ni nywele kila mtu ana zake*. Kwa kufanya hivi, mtafsiri angedumisha muundo wa methali na kuufikisha ujumbe kwa ulinganifu kwa sababu ujumbe wa methali hii unalingana na ule aliokuwa anawasilisha Achebe. Ingawa mbinu hii hukubalika katika tafsiri za methali na misemo katika miktadha mingine, katika muktadh huu, haiwezi kutumika kwa kuwa kuna haja ya kudumisha vipengee vya kitamaduni vinavyojitokeza katika methali na misemo ilinayojitokeza kwenye MC. Hivyo basi tafsiri anabaki na mbinu moja ya kutafsiri ambayo ni kutumia tafsiri ya moja kwa moja kibunifu ili, kutimiza majukumu yote matatu ya tafsiri za methali na misemo.

Kigae ni kipande cha chungu kilichovunjika, nacho huwa na matumizi mbalimbali. Miongoni mwa matumizi haya huwemo kubeba moto miongoni mwa jamii nyingi za Afrika kutoka kwa majirani zao inavyojitokeza katika methali *What man would send his son with a potsherd to bring fire from a neighbour's hut and then unleash rain on him? (AOG uk.233)* ambayo imetafsiriwa, *Mtu gani angeweza kumtuma mwanawe akachukue moto kwa jirani na halafu akamnyeshea mvua? (MWM uk. 205)* Katika methali hii Ezeulu anadhihirisha mgogoro baina yake na Ulu. Ezeulu anaona kuwa Ulu anampa majukumu ya kuelekeza watu wa Umuaro kutenda anavyotaka yeye (Ulu) kisha kuifanya kazi hiyo kuwa ngumu kwake. Achebe anapamba mgogoro huu kwa methali mbali mbali ili pengine kusisitiza mgogoro huu kwa kuwa unaishia kuporomoka kwa imani ya kitamaduni ya Wa-Igbo wengi akiwemo Ezeulu mwenyewe na kupisha dini ya Kizungu. Kupitia kwa methali hizi vifaa vya aina aina vya Igbo vinajitokeza. Kwa hakika maana ya methali hii inajitokeza katika sifa ya kigae ya uwazi hivi kwamba moto ukibebwa kwa kigae kisha matone ya mvua yaanguke, moto huo utazima. Katika tafsiri ya methali hii mtafsiri ametafsiri kwa njia ya moja kwa moja na zaidi akadondoa neno “potsherd” linaloweza kutafsiriwa kama “kigae” na ambalo ni muhimu sana katika kuelewa ujumbe wa methali hii. Kwa kufanya hivi mtafsiri amepoteza taswira muhimu katika mgogoro mzima baina ya Ulu na kasisi wake Ezeulu. Pengine methali hii ingejitokeza vyema zaidi ingetafsiriwa kuwa *Mtu gani angeweza kumtuma mwanawe akachukue moto kwa kigae kutoka kwa jirani kisha akamnyeshea mvua?*



*When suffering knocks at your door and you say there is no seat left for him, he tells you not to worry because he has brought his own stool.* (uk.87), methali hii imetafsiriwa kuwa *Mateso yakija na kugonga mlango wako na wewe ukisema hakuna pa kukaa, anakwambia kuwa usijali maana amekuja na kiti chake mwenyewe* (MWM uk.74), ni methali inayotajwa na Moses Unachukwu ambaye alikuwa mzee mfuasi wa dini ya mzungu kwa vijana wa rika la Obika walipokuwa wanajadili kuhusu uwezo wa mzungu. Unachukwu anasema hivi kuwaambia vijana waliokuwa pale kuwa mzungu amekuja kwao (Umuaro) kuleta taabu na zaidi hataondoka karibuni. Kwa kutaja methali hii Unachukwu anaelekea kuwashauri vijana wale kujitayarisha kuishi na mzungu huko Umuaro, pamoja na matatizo yote atakayoyaleta akiishi huko. Katika AOG uk.87 mhusika Unachukwu anasema kuwa kabla yeyote kati ya vijana waliokuwa kwenye mkutano ule kuwa na umri wa kutosha kujua kufunga kitambaa katikati ya miguu yake, aliona kwa macho yake mwenyewe kile ambacho mtu mweupe alifanyia watu wa kijiji cha Abame. Unachukwu anaendelea kusema kuwa alipoona kile ambacho mzungu aliwafanyia watu Abame, alijua kuwa hakuna pa kutorokea na jinsi mwangaza wa mchana ufukuzavyo giza ndivyo mtu mweupe atakavyofukuza tamaduni na desturi zao. Kwa ufupi methali hii imetumiwa kuwashauri vijana wasitarajie kuwa mzungu angeondoka bali wajitayarishe kuishi naye huko huko miongoni mwao. Methali hii ingetafsiriwa kwa methali linganifu ingejitokeza kwa Kiswahili kwa njia ambayo ingedumisha methali. Ila kwa kutafsiri sisisi, kazi hii katika Kiswahili imepoteza methali. Pengine, njia mwafaka zaidi ya kutafsiri methali hii ingekuwa kwa kutumia methali ya Kiswahili *Likufikalo patana nalo*. Lakini njia hii haiwezi kudumisha taswira ya kitamaduni, hivyo kuna haja ya mtafsiri kuwa mbunifu na kutafsiri methali hii kwa namna kwaba atadumisha, ujumbe na zaidi utamaduni kama alivyofanya Shamte.

Kifaa kingine kinachojitokeza katika utamaduni wa Ki-Igbo, kama unavyowasilishwa na Achebe katika AOG, ni mkeka wa kuzikiwa. Katika methali *The man who has never submitted to anything will soon submit to the burial mat* (uk.11). Methali hii imetafsiriwa kuwa *mtu ambaye hajapata kuitikia chochote, ghafla huitikia mkeka wa kuzikiwa* (uk. 10) katika MWM. Miongoni mwa Wa-Igbo na baadhi ya jamii za ulimwenguni, mtu akifa huwekwa kwenye mkeka mzito na wa kipekee kabla ya kuzikwa kaburini tofauti na jamii ya Waswahili ambayo wakati wa mazishi maiti hufungwa katika kitambaa cha kipekee kiitwacho sanda kabla ya kuzikwa. Methali hii imetumiwa na Ezeulu kwa mwanawe Obika ambaye alikuwa jasiri sana. Ezeulu anamkumbusha Obika kuwa

ni vyema kuwa jasiri lakini watu wenye ujasiri mwingi hufa kabla ya waoga. Mtu jasiri anapokufa hawezi kukataa kulalia mkeka wa kuzikiwa kwa kuwa hana fahamu wakati huo. Methali hii inatokana na ukweli huu kuwa, hata mtu awe na nguvu kiasi gani kupinga kila jambo na kushinda kila mja, anapokufa uwezo wote alionao huisha akabaki kufanya yale wanayotaka wanaomzika. Ujumbe unaosisitizwa na methali hii ni kwamba mtu asiwe na ujasiri kupita kiasi maana ujasiri huo unaweza kumsababishia maangamizi kabla ya wakati wake kufika. Shamte ametafsiri methali hii na kutumia neno “ghafla” linaloleta dhana ya bila kutarajia badala ya “hatimaye” linaloleta dhana ya hakika. Shamte vilevile, ametafsiri “mat” kwa neno “mkeka” dhana ya kitamaduni ya Ki-Igbo. Neno hili lina kisawe cha kitamaduni katika utamaduni wa Kiswahili ambacho angetumia kulingana na mapendekezo ya Newmark (1988). Neno “sanda” lingewasilisha ujumbe kwa ulinganifu zaidi kuliko “mkeka” lililotumika na Shamte. Makosa katika tafsiri hii ni matumizi ya visawe katika Kiswahili ama visivyo sahihi au vinavyopanua tofauti za kitamaduni badala ya kuzipunguza. Tatizo hili lingetatuliwa kwa kutumia visawe mwafaka, kwa mfano angesema *Mtu ambaye hajapata kuitikia chochote hatimaye huitikia sanda ya kuzikiwa.*

#### 4.1.2 Methali na misemo inayohusiana na vyakula na vinywaji

<b>Methali /Misemo katika <i>Arrow of God</i></b>	<b>Methali /Misemo katika <i>Mshale wa Mungu.</i></b>
<i>When was it ever heard that a child was scalded by a <b>piece of yam</b> its own mother put in its palm(uk. 233)</i>	<i>Lini imepata kusikika kuwa mtoto ameunguzwa na kipande cha kile kiazi ambacho mama yake mwenyewe amekitia kiganjani mwake (uk.205)</i>
<i>A man who knows that his anus is small does not swallow an <b>udala seed</b> (uk.72)</i>	<i>Mtu anayejua kuwa mkundu wake ni mdogo hawezi kumeza <b>kokwa ya udala</b> (uk.62)</i>
<i>A man does not summon <i>Umuaro</i> and not set before them even a pot of palm wine(uk. 145)</i>	<b><i>Msemo umedondolewa</i></b>

Methali na misemo ya Ki-Igbo pia, inarejelea vyakula na vinywaji mbali mbali ambavyo bila shaka ni vyakula vya watu wa Igbo. Vyakula hivi ni vya aina mbalimbali yakiwemo kwa mfano matunda kama vile Udala, viazi kama vile viazi vikuu na hata pombe ya mnazi miongoni mwa vyakula vingine. Kubuniwa kwa methali na misemo katika kategoria hii, kumeshawishiwa na kuwepo kwa

vyakula na vinywaji hivi na sifa zake zinazopelekea matumizi ya kijazanda katika fani husika ili kutimiza lengo la Achebe la kuwapa wasomaji wake taswira ya utamaduni wa Ki-Igbo.

*When was it ever heard that a child was scalded by a piece of yam its own mother put in its palm? (AOG uk.233).* Ni msembo ambao, kubuniwa kwake kumechochewa na viazi vikuu. Msembo huu umetafsiriwa na Shamte kuwa, *Lini imepata kusikika kuwa mtoto ameunguzwa na kipande cha kile kiazi ambacho mama yake mwenyewe amekitia kiganjani mwake? MWM uk.205).* Viazi vikuu ni maarufu miongoni mwa jamii ya Igbo kama chakula chao cha kimsingi. Umaarufu huu ni wa kiwango kikubwa hivi kwamba msimu wa kupanda na kuvuna kwa Wa-Igbo, huwa ni wa kupanda viazi vikuu ama kuvivuna na shughuli hii hujumuisha takriban kila familia. Methali hii imerejelewa na Ezeulu, baada ya kifo cha Obika mwanawe mpendwa; anajiuliza maswali mengi kwa njia ya methali likiwemo hili. Ezeulu anashindwa kuelewa sababu iliyomfanya Ulu kumpa pigo kupitia kwa kifo cha mwanawe ilhali siku zote amejitolea kutenda, mapenzi ya Ulu. Kulingana na Awa na Ngele (2014), viazi vikuu ni ishara wakilishi ya jamii yenyewe, shughuli nzima ya uvunaji na sherehe ya viazi vikuu huunganisha jamii sawa na viazi vikuu vyenyewe vinavyowaunganisha kwa kuwa ni chakula kikuu cha jamii. Tafsiri ya methali hii jinsi ilivyofanywa na Shamte huenda isitoe athari sawa kwa msomaji wa Kiswahili kwa kuwa kwa mara nyingine, utamaduni unaorejelewa na Shamte, ni mgeni kwa msomaji wa Kiswahili. Badala ya tafsiri hii ya moja kwa moja, Shamte angetumia methali linganifu kiujumbe katika Kiswahili. Kwa kutumia methali kwa mfano *Teke la kuku halimumizi mwanawe*, ujumbe ungepitishwa kwa ulinganifu na methali kudumishwa. Hata hivyo kuna haja ya kudumisha vipengee vya kitamaduni na kwa sababu hii itahitajika tafsiri ambayo itavirejelea vipengee hivi vya kitamaduni na kwa sababu hii, tafsiri alioitoa Shamte inaweza kukubalika kuwa mwafaka katika muktadha huu.

*A man who knows that his anus is small does not swallow an udala seed (uk.72)* ni methali nyingine ambayo imerejelewa mara kwa mara riwayani. Katika AOG (uk.72), methali hii imetajwa na Ezeulu katika mafoko anayofoka wakati anakimbia huku akifoka kutekeleza wajibu wake kama kasisi wa Ulu wakati wa sherehe inayoitwa *sherehe ya majani ya malenge* (TY). Shamte ametafsiri methali hii kwenye MWM kuwa, *Mtu anayejua kuwa mkundu wake ni mdogo hawezi kumeza kokwa ya udala (uk.62).* Udala ni aina ya tunda linaloliwa na watu wa Igbo, tunda hili lina kokwa ambayo haiwezi kusagwa tumboni na hivyo ikimezwa hutoka ikiwa nzima kupitia kwa tupu ya nyuma ya mtu pamoja na choo. Mtu ambaye ana nafasi ndogo ya kutolea choo, bila shaka atapata

taabu kubwa sana msalani iwapo atameza kokwa ya udala, kwa sababu atakuwa analazimisha kokwa ile ya Udala kupitia kwenye nafasi ndogo sana na zaidi atapata maumivu makali. Busara iliyo kwenye methali hii ni kuwa kila wakati mtu apime jambo analokusudia kufanya kwa kukadiria uwezo alinao na kupima matokeo yake kabla ya kufanya jambo hilo. Tafsiri ya Shamte itaeleweka tu pale msomaji atakapoelewa udala ni nini, ila katika tafsiri yenyewe msomaji hawezi kuelewa dhana hii kwa kuwa imehawilishwa. Ili kumrahisishia msomaji wa tafsiri uelewa, mtafsiri pengine angeongeza maelezo kuhusu tunda hili la udala kwenye tanbihi baada ya tafsiri aliyoifanya ili msomaji aelewe. Kwa mfano, tanbini inaweza kuwa na maelezo haya; *-udala ni aina ya tunda linalopatikana Afrika MAagharibi lenye kokwa ngumu kusagika tumboni na hutoka na kinyeshi kadri lilivyoingia tumboni.*

Ezeulu anawaita wazee wa Umuaro ili kuwaomba wamshauri atakavyomjibu Winterbottom kwa kuwa Winterbottom alimtaka Ezeulu kwenda kumwona huko alikokaa, Okperi. Ezeulu anajua kuwa ni kinyume cha masharti ya ukasisi alioshikilia kwenda mbali na kwake. Kwa kuwa wito huu ulimjia ghafla hakupata nafasi ya kuandaa chochote cha kutia kinywani kwa ajili ya wageni hao aliowaita kama ilivyotakiwa kidesturi. Kwenye mkutano Ezeulu anawaomba radhi na kuisitiza makosa yake kwa msemu *A man does not summon Umuaro and not set before them even a pot of palm wine* (AOG uk.145). Katika MWM, msemu huu haujitokezi hata kwa maelezo, labda mtafsiri hakuliona jambo la muhimu kuutafsiri au labda kausahau. Kuuacha msemu huu nje kunapoteza sio tu ladha ya lugha inayotokana na msemu huu bali pia utamaduni uliowakilishwa. Muundo wa msemu huu unaweza kukubalika katika misemo ya Kiswahili hata ukatafsiriwa kwa njia ya moja kwa moja na zaidi kinywaji kinachorejelewa kina kisawe katika Kiswahili. Hivyo, tafsiri ya moja kwa moja ingefaa katika kutafsiri msemu huu zaidi ya kuudondosha. Pengine tafsiri mwafaka zaidi ingekuwa *Mtu haaliki Umuaro na kukosa kuwaandalia hata buyu la pombe ya mnazi.*

#### **4.2. Utamaduni wa kijamii**

Methali na misemo katika kategoria hii hudhihirisha dhana mbalimbali katika maumbo yao ambazo huwakilisha hali na shughuli mbalimbali katika jamii mahususi. Maswala yanayowasilishwa na methali na misemo hii ni pamoja na, busara ya jamii, asasi za kijamii ambazo hudhibiti mahusiano ya wanajamii wa viwango mbali mbali, shughuli za kikazi ambazo wanajamii

hujihusisha nazo, pia imani za kidini na za kishirikina za watu wa jamii husika. Katika AOG maswala haya yanajitokeza katika methali na misemo ifuatavyo;

#### 4.2.1 Methali na misemo inayohusiana na busara ya jamii

Methali/misemo Kiingereza	Tafsiri katika Kiswahili
1 <i>When a handshake passes the elbow, it becomes another thing (uk.230).</i>	<i>Kupeana mikono kukifika mpaka karibu ya bega huwa kitu kingine (uk. 203)</i>
2 <i>When a man of cunning dies, a man of cunning buries him. (20)</i>	<i>Mjanja akifa huzikwa na mjanja (18)</i>
3 <i>A man must dance the dance prevalent in his time. (uk.193)</i>	<i>Mtu lazima acheze ngoma iliyo sawa na wakati wake (uk.169)</i>
4 <i>The boy who persists in asking what happened to <b>his father</b> before he has enough strength to avenge him is asking for his father's fate. (uk.231)</i>	<i>Mtoto anayeshikilia kuuliza yaliyotokea kwa <b>baba yake</b> kabla hajakuwa na nguvu za kutosha za kumlipia kisasi anataka bahati mbaya ya babake (uk.203)</i>

Kulingana na Aderinto (2014), ili kuwezesha mawazo yao kuhusu kuwa makini katika maisha kuwa bayana, watu wa makabila mbali mbali ya Nigeria hutumia methali kuandika jambo hili mawazoni mwa wenzao. Kwa kufanya hivi wanaazimia kuwasaidia ili waishi maisha yasiyo na matatizo kwa kusisitiza umuhimu wa kuwa makini. Achebe, katika AOG, ametumia methali *When a handshake passes the elbow, it becomes another thing (AOG uk.230)*. Methali hii ambayo imetafsiriwa kuwa *Kupeana mikono kukifika mpaka karibu ya bega huwa kitu kingine (MWM uk. 203)* inamaanisha kuwa mtu anafaa kuwa mwangalifu hasa kunapotokea mtu ambaye anajipendekeza sana kwa mwingine kwa kuwa inawezekana mtu huyo hana nia nzuri. Achebe anatomia methali iliyotajwa hapo juu kurejelea ukweli kuwa ni jambo la busara kwa mtu kuwa makini anapotangamana na watu na kufanya shughuli mbalimbali nao. Tafsiri ya methali hii katika MWM inajitokeza kama maelezo tupu ambayo hayadhihirishi ufundi wowote unaojitokeza kwenye methali. Kwa kuwa pengine hakuna kisawe katika Kiswahili basi inaweza kutafsiriwa ili ijitokeze kama methali ya Kiswahili kwa mfano anaweza kusema, *Maamkuzi ya mkono yanapopita kiwiko cha mkono, yanakuwa kitu kingine*.

Kulingana na Awa & Ngele (2014), katika riwaya ya **Arrow of God**, Akuakalia anawaambia wenzake, *When a man of cunning dies, a man of cunning buries him*. Methali hii imetafsiriwa kuwa *Mjanja akifa huzikwa na mjanja (Uk.18)* Kwa kusema hivi anamaanisha, yeye ni mjanja kama watu wa Okperi, kwa hivyo anafaa kuachwa akabiliane nao. Katika AOG Uk.18, Akuakalia

anatanguliza usemi huu ili kuwafahamisha kuwa anajua kuwa watu wa Okperi ni wagumu sana kueleza chochote na hivyo anawashauri wenzake wanyamaze ili yeye azungumze nao kwa kuwa anawaelewa vizuri. Kwa kuwa methali ina sifa za kimuundo zinazolingana na sifa za methali za Kiswahili hata inapotafsiriwa sisisi, inajitokeza kama methali na hivyo muundo na mtindo unadumishwa.

Ezeulu anamkumbusha mwanawe Oduche kuwa amemtuma kwa mtu mweupe ili akajifunze anachokijua mtu mweupe. Anamwambia kuwa mtu akimuuliza mbona ameenda kujifunza kwa mzungu, Oduche awajibu kwa msemu huu *A man must dance the dance prevalent in his time. (uk.193).* Msemu huu umetafsiriwa katika MWM kuwa *Mtu lazima acheze ngoma iliyo sawa na wakati wake (uk.169).* Kwa kusema hivi Ezeulu anamshauri Oduche kuwa wakati wa jambo fulani ukifika, ni sharti jambo hilo lifanyike wala hakuna njia ya kulikwepa. Tafsiri ya Shamte inadhooifisha uzito wa ujumbe. Neno ‘prevalent’ lina maana ya kuwa na umaarufu katika kipindi au nyanja maalum na hivyo lina msukumo zaidi, lakini Shamte amelitafsiri kwa neno ‘sawa’ lenye maana ya iliyopo wakati huo. Kwa kuzingatia hali hii inadhihirika kuwa msemu asilia una dhana ya ushindani baina ya ngoma za kitamaduni, ujuzi na elimu ambayo haijitokezi katika tafsiri. Kwa kutafsiri neno ‘prevalent’ visivyo mgogoro baina ya tamaduni ambao ni ujumbe mkuu wa riwaya ya Achebe AOG. Ili kudumisha ujumbe na mtindo wa methali na misemo katika Kiswahili, mtafsiri angetumia methali ya Kiswahili yenye ulinganifu wa maana kwa mfano *Mwenye nguvu mpishe.* Ingawa tafsiri hii ni mwafaka, itakuwa bora zidi kutasfiri methali hii kwa njia itakayodumisha vipengee vya utamaduni kwa mfano tafsiri inaweza kuwa *mtu ni lazima acheze ngoma iliyo na nguvu zaidi kwa wakati wake.*

Methali nyingine inayodhihirisha busara ya jamii ni *The boy who persists in asking what happened to his father before he has enough strength to avenge him is asking for his father's fate. (AOG uk. 231)* Shamte anatafsiri methali hii kuwa *Mtoto anayeshikilia kuuliza yaliyotokea kwa baba yake kabla hajakuwa na nguvu za kutosha za kumlipia kisasi anataka bahati mbaya ya babake (uk.203).* Kulingana na Aderinto (2014) methali hii inapendekeza kuwa lazima tufanye mambo kwa wakati ufaao. Katika muktadha wa Igbo ni makosa kwa yeyote kufanya mambo kwa wakati usiofaa kwa jambo hilo kufanywa. Ni mojawapo ya methali inayokaririwa usiku na Ogbazulobodo ambayo kimsingi ni muhtasari wa utamaduni wa Ki-Igbo. Wa-Igbo wanaamini kuwa hatua zinafaa kuchukuliwa kwa wakati ufaao bila kupapia mambo hivi kwamba ikiwa wakati wa jambo

kufanywa haujafika, watu wanafaa kusubiri na kufanya mambo taratibu, kwa uangalifu, hatua baada ya nyingine. Katika utamaduni wa Kiswahili pia, kuna imani inayokaribiana sana na hii na inaelezwa kwa methali *haraka haraka haina baraka* methali hii inatahadharisha watu dhidi ya kufanya mambo kwa haraka bila umakinifu. Matokeo ya tafsiri kama hii ni kuwa mtindo unapotea. Methali inatokea kama maelezo tu. Pengine, angetumia methali ya Kiswahili yenye ulinganifu kimaana

#### 4.2.2 Methali na misemo inayohusiana na imani za kidini na za kishirikina

Methali na misemo katika Kiingereza inavyojitokeza katika AOG	Tafsiri ya methali na misemo katika MWM
1 <i>If a man says yes his <b>chi</b> says yes(uk. 29)</i>	<i>Mtu akisema ndiyo, <b>mungu</b> wake husema ndiyo vile (uk.25)</i>
2 <i>A man might have <b>Ngwu</b> and still be killed by <b>Ojukwu</b>. (uk.40)</i>	<i>Mwanamume anaweza kuwa na <b>Ngwu</b> na juu ya hivyo auwawe na <b>Ojukwu</b> (uk. 34)</i>
3 <i>When a man sees a snake all by himself, he may wonder whether it is an ordinary snake or the untouchable python (uk.145).</i>	<i>Mtu akimwona nyoka peke yake hustaajabu kama ni nyoka wa kawaida au chatu asiyeguswa (uk.127).</i>
4 <i>No matter how <b>many spirits plotted</b> a man's death, it would come to nothing unless his personal god took a hand on the deliberation. (uk.139)</i>	<i>Hata pepo wangapi <b>wakipanga kifo</b> cha mtu, haitakuwa kitu mpaka mungu wake asaidie katika jambo hilo(uk.122)</i>
5 <i>The <b>evil charm</b> brought in at the end of a pole is not too difficult to take outside again. (uk.147)</i>	<i><b>Hirizi</b> mbaya iliyoletwa mwisho wa upondo, haina taabu kuitoa tena nje(uk.129)</i>

Methali na misemo pia imetumika kuwasilisha imani za Ki-Igbo kuhusiana na masuala ya kidini. Kwa mfano, *If a man says yes, his **Chi** also says yes (29)*. *Chi* katika ulimwengu wa Ibo ni Mungu wa roho, mlinzi wa mtu binafsi ambaye kila mja hupokea anapozaliwa na ni sehemu ya maumbile ya mtu. Kulingana na imani ya Ki-Igbo, *chi* ndiye huamua yanayompata mtu na vilevile ndiye anayemkinga mtu dhidi ya mabaya. *Chi* wa mtu kulingana na Awa & Ngele (2014), imani ya Ki-Igbo hukubali au kukataa chochote mtu hukubali au kukataa. Kwa hivyo, mtu ana sehemu ya kuchangia katika yanayompata, kwamba ni lazima mtu achukue hatua kisha *Chi* wake pia afanye hivyo. Methali hii imetafsiriwa kuwa *Mtu akisema ndiyo, **mungu** wake husema ndiyo vile (MWM*

uk.25) *Katika kutafsiri hivi*, usemi huu unasomeka kwa Kiswahili kama methali, hata hivyo, ujumbe wake unakanganya. Sababu inayofanya ujumbe huu ukanganye ni kuwa, utamaduni wa Kiswahili unatofautiana sana na wa Ki-Igbo katika maswala ya kidini. Dhana hii ya *Chi* haipo katika Kiswahili, na hata maelezo ya mtafsiri hayatoshi kuemueleweshwa msomaji wa tafsiri hii, ujumbe wa Achebe. Hali kama hii huhitaji matumizi ya muungano wa mbinu kama vile mbinu ya uhawilishaji na viziada katika kutafsiri. Methali hii ingetafsiriwa kuwa *Mtu akisema ndio, Chi wake pia huitikia*, kisha katika tanbihi anaweza kufafanua kuwa Chi ni Mungu roho, mlinzi ambaye kulingana na Wa-Igbo huwa sehemu ya kila mja.

Hali kama hii inajirudia katika methali *A man might have Ngwu and still be killed by Ojukwu. (AOG UK.40)* Methali hii imetafsiriwa kwa njia ya moja kwa moja kuwa *Mwanamume anaweza kuwa na Ngwu na juu ya hivyo auwawe na Ojukwu* (uk.34). Ngwu na Ojukwu ni miungu katika jamii ya Igbo miongoni mwa miungu wengine. Metuh (1999) anataja majina ya miungu wa Ki-Igbo wakiwemo Eze Mewi, Ogwugwu, Idemili, Ulasi, Ubu, Ele, Ojiyi, Akpu, **Ojukwu**, na **Ngwu** miongoni mwa miungu wengine na anaendelea kutaja kuwa wengi wa miungu hawa ni uhaishaji wa maumbile au wa vitu ambavyo vinazalisha miungu hii ndio maana huitwa miungu ya kimaumbile. Bila shaka methali hii inatokana na kuwepo kwa miungu wengi na inaelekea kuwa kila mungu ana majukumu yake anayotimiza, ambyo ni tofauti na ya miungu wengine. Methali hii inaonyesha kwamba kuwa na mungu mmoja kati ya hao waliopo hakumzui mungu mwingine kumdhuru mtu. Sawa na Chi, Ojukwu na Ngwu, ni dhana ngeni kabisa katika Utamaduni wa Kiswahili. Shamte katika kutafsiri, amezihawilisha dhana hizi, jambo ambalo si makosa kulifanya ila hakuzifafanua na hivyo akaishia kumwacha msomaji wake katika giza la kutoelewa kwani anavyodai Landers (2001), watu huelewa mambo na kulingana na utamaduni wao. Mbali na uhawilishaji huu, tafsiri ya methali hii vile vile ina makosa kwa kuwa inapendekeza ujumbe usiolingana na ule unaojitokeza katika methali ya LC. Kwa kutafsiri maneno and still kuwa, na juu ya hivyo, Shamte anapotosha ujumbe. ‘And still’ ina maana ya ‘zaidi ya hivyo’ wala si ‘na juu ya hivyo’ kwa sababu, ‘juu ya hivyo’ huelekea kuleta dhana ya ‘sababu.’ Hivyo basi, ujumbe wa tafsiri ya methali hii ilivyofanywa na Shamte ni kuwa mtu kuwa na Ngwu kunamsababishia kuuwawa Ojukwu maana iliyo potovu. Pengine, tafsiri mwafaka zaidi ingekuwa *Mwanamume kuwa na Ngwu hakumzui kuuwawa na Ojukwu*. Baada ya kutafsiri hivi, mtafsiri angeeleza katika tanbihi kuwa Ngwu na Ojukwu, ni miungu wa kimaumbile katika utamaduni wa Wa-Igbo.



Methali nyingine iliyotumika katika *Arrow of God* ni *when a man sees a snake all by himself, he may wonder whether it is an ordinary snake or the untouchable python (uk.145)*. Methali hii imetafsiriwa kuwa *Mtu akimwona nyoka peke yake hustaajabu kama ni nyoka wa kawaida au chatu asiyeguswa (MWM uk.127)*. Inaelekea kuwa katika muktadha wa matumizi yake, methali hii imetumiwa kumaanisha kuwa mtu huhitaji maoni ya wenzake katika kufanya maamuzi. Ezeulu anawaeleza wazee wa Umuaro sababu ya wito wake kwao kupitia kwa methali hii. Anawaeleza kuwa amewaita wampe ushauri kabla ya kuamua atakalofanya kuhusu na mwaliko wake kwenda Okperi kutoka kwa mzungu Winterbottom. Baada ya kuwaeleza wazee wenzake haja yake, anaisisitiza kwa methali hii ambayo inataja aina fulani ya chatu ‘the untouchable python’ ambayo imetafsiriwa kuwa ‘chatu asiyeguswa’ na Shamte. Chatu anayerejelewa katika methali hii si chatu wa kawaida ila mnyama wa kipekee ambaye anawakilisha imani ya dini ya kitamaduni miongoni mwa watu wa Umuaro. Ni mnyama ambaye anachukua nafasi muhimu katika ibada ya Idemili, mungu mmojawapo wa watu wa vijiji sita vya Umuaro. Kulingana na Achebe, katika (*AOG uk. 50*) watu wa vijiji sita vya Umuaro waliambiwa kuwa chatu wa kifalme ni mtakatifu kwa Idemili. Shamte anapotafsiri methali hii, anatafsiri kipengee hiki cha kidini kwa ukawaida kiasi kwamba, upekee wake unatoweka katika tafsiri hii na pamoja na upekee huo utamaduni pia unapotea. Kwa kuwa dhana hii ya kitamaduni ya utamaduni wa kidini haina ulinganifu katika utamaduni wa Kiswahili, mtafsiri ana uhuru wa kuamua mkakati bora zaidi wa kutumia katika kutafsiri. Kwa mfano kutafsiri methali hii kwa maelezo yanayoweza kupitisha ujumbe wa mwandishi kwa ulinganifu kadri iwezekanavyo alivyofanya Shamte.

Methali *No matter how many spirits plotted a man’s death it would come to nothing unless his personal god took a hand on the deliberation (uk.139)*, ambayo imetafsiriwa kuwa *Hata pepo wangapi wakipanga kifo cha mtu, haitakuwa kitu mpaka mungu wake asaidie katika jambo hilo (uk.122)* ni dhihirisho la imani ya Wa-Igbo kuhusu mapepo, kuwa mapepo wanaweza kusababisha ugonjwa unaoua mtu. Katika *AOG uk.115*, Akuebue anapozungumzia ugonjwa wa bwana mmoja kutoka Umofia kwa jina Ogbuefi Amalu, anamwambia Ezeulu kuwa “Lakini kama ugonjwa ni wa mapepo...hakuna dawa inayoweza kuutibu...” (TY) Maneno haya ya Akuebue kuhusu ugonjwa wa Amalu, yanathibitisha imani kuwa mapepo yanaweza kusababisha kifo cha mtu. Hata hivyo, pia inadhihirika kuwa ni lazima mungu wa mtu binafsi ambaye tunaamini ni Chi asaidie katika kuamua kifo hiki. Kulingana na maelezo tuliyotangulia kutoa kuhusu Chi wa mtu, kwanza ni

lazima mtu mwenyewe akubali kuuwawa na mapepo ndipo mungu wake binafsi (*Chi*) vile vile akubali, ndipo mapepo wamuue. Kukubali kuuwawa na mapepo katika muktadha huu kuna maana ya kukata tamaa na kuacha kupigania uhai. Hali kama hii inajitokeza pale Amalu anapewa Ofo (fimbo ya kipekee katika utamaduni wa Ki-Igbo) ashikilie na kukemea mapepo lakini anaiachilia inaanguka, watu wanaotazama wanatazamana kwa mtazamo unaoonyesha kuelewana kuwa, si muda mrefu Amalu atakufa. Methali *no matter how many spirits plotted a man's death it would come to nothing unless his personal god took a hand on the deliberation (AOG uk.139)*, imerejelewa na Ezeulu katika nyumba yake baada ya kutembelewa na Mjumbe wa Winterbottom. Mjumbe huyu ni mzaliwa wa kijiji cha Umuru na hivyo anaonyeshwa njia na mtu kutoka Umuaro kwa kuwa yeye ni mgeni katika kijiji cha Umuaro. Hali hii inamchochea Ezeulu kutaja methali hii kuonyesha kuwa hakuna jambo linaloweza kufaulu dhidi ya mtu iwapo mtu aliye karibu naye sana hatasaidia wanaotaka kulitekeleza. Shamte ametafsiri methali hii kwa usahihi, kwa kuangazia maana za maneno ambazo zinadhihirisha utamaduni ambao A chebe anaokusudia kuupitisha.

*Methali the evil charm brought in at the end of a pole is not too difficult to take outside again (uk.147)* imetafsiriwa kuwa **Hirizi mbaya iliyoletwa mwisho wa upondo, haina taabu kuitoa tena nje (uk.129)**. Ni methali inayorejelea imani za kishirikina za Wa-Igbo. Methali hii inatumiwa na Nwaka katika mkutano wa kumshauri Ezeulu kuhusu jinsi ya kukabiliana na wito wa Winterbottom. Inaelekea kuwa Nwaka analiona tatizo la Ezeulu kuwa kama hirizi iliyoletwa ndani mwishoni mwa upondo kwa maana kuwa Ezeulu alifanya urafiki na Winterbottom jambo lililosababisha wito huu, hivyo basi ikiwa Ezeulu hakupendezwa na wito huo ilikuwa rahisi kuuvunja urafiki huo. Dhana 'charm' ambayo imetafsiriwa kisahihhi kuwa 'hirizi' ni dhana inayofahamika miongoni mwa jamii nyingi za Kiafrika, hivyo si vigumu kupata ulinganifu katika lugha nyingi, ikiwemo lugha ya Kiswahili. Kwa sababu hii, tafsiri ya moja kwa moja aliyoifanya mtafsiri, ingeeleweka bila tatizo kubwa kama hangedondosha, neno moja kwenye tafsiri yake. Kwa kutafsiri methali hii kuwa *Hirizi mbaya iliyoletwa mwisho wa upondo, haina taabu kuitoa tena nje* amedondosha neno 'in' ambalo linarejelea ndani ya nyumba, kulingana na muktadha wa methali hii. Udondoshaji huu wa neno katika tafsiri umefanya methali ipoteze ukamilifu wake kama methali na hivyo imekosa ukamilifu wa maana. Ingekuwa bora zaidi kutafsiri methali hii bila kudondosha neno hata moja, kwa mfano *Hirizi mbaya iliyoletwa ndani ikiwa katika mwisho wa upondo, haina taabu kuitoa tena nje*.

#### 4.2.3 Methali na misemo inayohusiana na shughuli za kazi

Methali/misemo Kiingereza		Tafsiri katika Kiswahili
1	<i>When hunting day comes, we shall <b>hunt</b> in the backyard of the grass-cutter. ( uk.146)</i>	<i>Siku ya kuwinda ikifika, tutawinda nyuma ya <b>kikata majani</b> (uk.127)</i>
2	<i>A man cannot be too busy to <b>break</b> the first <b>kolanut</b> of the day in his own house. (uk.114)</i>	<i>Mtu hawezi kuwa na shughuli nyingi hata akashindwa <b>kuvunja kola ya mwanzo</b> nyumbani kwake.(uk.99)</i>
3	<i>A man who visits <b>a craftsman at work</b> finds a sullen host. (uk.116)</i>	<i>Anayetembelea <b>fundi</b> akiwa kazini, atakuta mwenyeji aliyechukiwa.( uk.101)</i>

Watu wa Igbo hushiriki katika shughuli mbali mbali za kujiendeleza kimaisha, ziwe za starehe na burudani au harakati za kiuchumi. Baadhi ya shughuli hizi zimejibainisha katika methali na misemo, kwa mfano, katika msemu uliorejelewa *When hunting day comes, we shall **hunt** in the backyard of the grass-cutter (AOG uk. 146)*, shughuli ya ‘hunting’ ambayo imetafsiriwa ‘kuwinda’ imetajwa. Methali hii imetafsiriwa na Shamte kama *siku ya kuwinda ikifika, tutawinda nyuma ya **kikata majani** (uk.127)*. Methali hii imerejelewa na Ezeulu akiwaambia wazee wa Umuaro kuwa ingawa hakuwa amewatayarishia pombe ya mnazi siku hiyo, ipo siku watakunywa mpaka wasaze huko mbeleni. Shughuli ya kuwinda ni shughuli ambayo wanajamii wa tamaduni mbalimbali hushiriki na hivyo kuitafsiri huzua matatizo machache kwa mtafsiri kwa kuwa kuna ulinganifu kitamaduni na pia wa kileksika. Hata hivyo, tafsiri aliyioifanya Shamte kwa methali hii mbali na kujitokeza kama maelezo na kupoteza muundo wa methali pia inajitokeza kwa namna kwamba ujumbe wake umepotea. Zaidi Shamte anafanya makosa ya kutumia visawe visivyo sahihi katika tafsiri ya methali hii. Kulingana na kamusi ya Kiingereza ya Oxford (2010), neno ‘grass cutter’ ni mnyama mkubwa wa familia ya fuko ambaye hupatikana Afrika Maghribi na huliwa na binadamu. Neno ‘backyard’ hutumiwa kwa maana ya sehemu ya nyuma nje ya nyumba. Kutokana na maana hizi za maneno, ni dhahiri kuwa methali hii inatumiwa kuwaomba wawe na matumaini kwa sababu kuwa siku ya kuwinda itakapofika, itakuwa kazi rahisi kwao kupata windo lao maana watawinda nyumbani mwa windo lao. Tafsiri ya Shamte inaonyesha kuwa watakuwa nyuma ya kikata majani na wala si nyumbani kwake ambapo ni rahisi sana kumkamata. Maana hii ni tofauti na haiwasilishi maana ya methali kwa ukamilifu kwa vile inaelekea methali hii ina uamilifu wa kuwatia watu moyo kutarajia mema baadaye. Pengine ingekuwa bora kuitafsiri methali hii kuwa *siku ya kuwinda itakapofika tutawinda kiamboni mwa kikata majani*.

Miongoni mwa shughuli za Wa-Igbo, kuna desturi ya kuvunja kola hasa wakati wametembelewa na wageni. Desturi hii inajidhihirisha katika msemu *A man cannot be too busy to break the first kola nut of the day in his own house (uk.114)*, ambayo imetafsiriwa kuwa *Mtu hawezi kuwa na shughuli nyingi hata akashindwa kuvunja kola ya mwanzo nyumbani kwake (uk.99)*. Msemu huu unatumiwa na Ezeulu akimwambia Akuebue nyumbani mwa Akuebue. Ezeulu alikuwa amemtembelea rafikiye huyu ambaye alikuwa anatarisha mbegu za viazi kwa ajili ya kupanda siku iliyofuata. Akuebue anamuomba Ezeulu kuvunja kola kwa niaba yake na Ezeulu analikataa ombi hili kwa methali hii. Kwa mujibu wa Mgbemere (2014) njugu ya kola, ni njugu yenye wekundu itokanayo na tunda la mti wa kola na hupandwa sana sana katika eneo la Magharibi la Nigeria. Kola ni njugu maarufu kwa upekee wake miongoni mwa Wa-Igbo. Mgbemere (2014) anaendelea kusema kuwa njugu hii ina utaratibu unaoongoza kuvunjwa na kuliwa kwake. Inaaminika kuwa bahati inayohusishwa na kola, iwe nzuri au mbaya kulingana na idadi ya vipande vya njugu zinazopatikana ndani yake, huwa na uhusiano wa moja kwa moja na anayeivunja na huathiri watu wote. Labda hii ndiyo sababu Ezeulu anakataa kuvunja kola katika nyumba ya Akuebue. Maelezo haya kuhusu utamaduni wa Ki-Igbo yana sehemu ya kimsingi katika kuelewa msemu huu lakini tafsiri iliyofanywa haikutilia hili maanani. Matokeo yake ni kuwa msemu huu haueleweki kisawasawa katika Kiswahili. Ni muhimu kuwa mtafsiri angezingatia kutumia viziada katika tafsiri hii ili aeleweke.

*A man who visits a craftsman at work finds a sullen host (uk.116)* ni methali inayotumiwa kuisitiza umuhimu wa kazi na kushauri watu kuwatembelea wenzao baada ya kazi ili kuwaruhusu wamalize kazi zao bila kubughudhiwa na wageni. Kutokana na msemu huu iwapo mtu atalazimika kumtembelea mwenzake wakati wa kazi, anatahadharishwa kuwa huenda akakosa kukaribishwa anavyostahili. Ni methali anayotaja Ezeulu, kama jibu kwa Akuebue aliyekuwa anatarisha vyakula kwa kupanda na ambaye alikuwa amerudia kazi yake baada ya salamu. Akuebue anaomba Ezeulu amuelewe kwa kutumia msemu wa *salamu wakati wa msimu wa baridi ya harmattan, hupokewa kando ya moto (TY)*. Kisha Ezeulu anajibu kwa methali hii kuonyesha kuwa anampa ruhusa kuendelea na kazi yake huku wakizungumza. Tafsiri ya methali hii katika MWM imejitokeza kuwa *mtu anayetembelea fundi akiwa kazini, atakuta mwenyeji aliyechukiwa (uk.101)*. Tafsiri hii inapoteza maana kabisa kutokana na kutafsiri neno ‘sullen’ vibaya; neno hili lina maana ya ‘kununa’ wala sio kuchukiwa. Makosa haya ya tafsiri yanaweza kuepukwa kwa

kutafsiri kwa usahihi kama vile kwa kusema *atembeleaye fundi kazini hukuta mwenyeji aliyenuna*. Tafsiri hii iliyopendekezwa inatatua tatizo sio tu la kisawe kisichofaa, bali pia inaweza kutatua tatizo la mtindo kwa kuwa methali hii inajitokeza kwa njia kwamba inaweza kutambuliwa kama methali ya Kiswahili na wala sio maelezo.

#### 4.2.4 Methali na misemo inayohusiana na desturi za kijamii

Methali/misemo	Kiingereza	Tafsiri katika Kiswahili
1	<i>We see a <b>little bird dancing</b> in the middle of the pathway, we must know that its <b>drummer</b> is in the near-by bush (uk.40)</i>	<i>Tunapokiona kidege kidogo kikicheza katikati ya njia, ni lazima tujue kwamba mpigaji ngoma wake yuko katika kichaka cha karibu (uk.35)</i>
2	<i>The man who belittles the sickness which monkey has suffered should ask to see the eyes which his nurse got from blowing the <b>sick fire</b>. (uk.231)</i>	<i>Mtu anayeyaona maradhi yaliyomsumbua kima kuwa madogo aombe kuona macho ya muuguzi wake yalivyo kutokana na kuvungia moto wa <b>ugonjwa ule</b> (uk.2o3)</i>
3	<i>The lizard who threw confusion into his mother's funeral rite, did he expect outsiders to carry the burden of <b>honouring his dead</b>? (uk.128)</i>	<i>Mjusi aliyeleta kutoelewana kwenye mazishi ya mama yake alitaraji watu waje kuchukua jukumu la <b>kuwaheshimu jamaa zake waliokufa</b>?(uk.112)</i>

Miongoni mwa shughuli za kila siku, Wa-Igbo hushiriki katika burudani, hasa kucheza ngoma, baadhi ya methali zinaonyesha utamaduni huu, kwa mfano methali *We see a **little bird dancing** in the middle of the pathway, we must know that its **drummer** is in the near-by bush (uk.40)* Methali hii imetumiwa na Achebe katika kueleza mawazo ya watu wa Umuaro ambao hawakuelewa ilivyowezekana kwamba Nwaka alikejeli mungu wao mkuu Ulu bila kuadhibiwa. Walishangaa Nwaka alipotoa nguvu zake kwa kurejelea methali hii ambayo Shamte ameitafsiri kuwa *Tunapokiona kidege kidogo kikicheza katikati ya njia, ni lazima tujue kwamba mpigaji ngoma wake yuko katika kichaka cha karibu (uk.35)*. Tafsiri hii inafikisha ujumbe kwa ulinganifu, kuwa mambo au vitu vinavyoonekana huwa ni matokeo ya vitu visivyonekana; tatizo tu ni kuwa imejitokeza kama maelezo tu. Pengine tatizo hili lingetatuliwa kwa kutumia methali ya Kiswahili yenye ulinganifu wa maana na muundo wa kileksika, lakini kwa sababu ni vigumu kupata methali ya Kiswahili yenye sifa hizi maelezo yaliyotolewa yanatokea kuwa tafsiri faafu zaidi.

Methali, *The man who belittles the sickness which monkey has suffered should ask to see the eyes which his nurse got from blowing the **sick fire** (AOG uk.231)* ambayo imetafsiriwa kuwa *Mtu*

*anayeyaona maradhi yaliyomsumbua kima kuwa madogo aombe kuona macho ya muuguzi wake yalivyo kutokana na kuvungia moto wa ugonjwa huo (MWM uk.203)* inaonyesha desturi ya Wa-Igbo wakati wa ugonjwa ambapo mtu anapougua, wanawasha moto ambao unahitajika kuwaka hadi mtu huyo apone au afe. Muuguzi wa mgonjwa hufanya kazi ya kuhakikisha moto huo hauzimi na hivyo macho yake huingia moshi na kuyafanya mekundu na yaliyovimba. Desturi hii inayorejelewa inatumia kusuta watu wanaodharau matatizo ya wengine kwa kuwa hawajui ukubwa au uchungu unaosababishwa na matatizo hayo. Methali hii imekaririwa sawia na methali nyingine na pepo wa usiku anayorejelewa kama *Ogubazulobodo*. Badala ya tafsiri aliyofanya Shamte kwa methali hii, angetumia methali ya Kiswahili kutimiza jukumu la methali hiyo na kudumisha mtindo; mambo mawili ambayo tafsiri yake katika MWM imenyima methali hii. Kwa mfano, angetumia methali *kitanda usichokilalia hujui kunguni wake*. Sawa na methali ya ki-Igbo iliyotajwa, methali hii ya Kiswahili huwakumbusha watu kutodharau matatizo ya wenzao na ingetimiza mahitaji ya tafsiri. Hali hii kinyume na tafsiri aliyofanya Shamte inabana uelewa wa msomaji wa Kiswahili kwa kuwa inawezekana asielewe desturi ya kuvunga moto kama inavyotokea miongoni mwa Wa-Igbo. Hata hivyo, tafsiri ya aina hii itaondoa vipengee vya kitamaduni vya utamaduni wa Ki-Igbo na badala yake kutumia vipengee tofauti vya utamaduni wa Kiswahili; athari ambayo haikubaliki katika vipengee vya kipekee ilivyo methali na misemo katika AOG.

Mazishi pia ni shughuli nyingine muhimu miongoni mwa Wa-Igbo, inavyodhihirika katika methali *The lizard who threw confusion into his mother's funeral rite did he expect outsiders to carry the burden of honouring his dead?* (uk.128). Methali hii imetafsiriwa kuwa *Mjusi aliyeleta kutoelewana kwenye mazishi ya mama yake alitaraji watu waje kuchukua jukumu la kuwaheshimu jamaa zake waliokufa?* (uk.112). Methali hii inajitokeza mawazoni mwa Akuebue mzee mmoja rafikie Ezeulu. Akuebue anawazia jinsi maadui wa Ezeulu wanamlaumu Ezeulu kwa kumtuma mwanawe Oduche kushiriki katika dini ya Ki-Kristo. Maadui hawa walikuwa wanamcheka Ezeulu baada ya kusikia kwamba Oduche alikuwa amefungia chatu mtakatifu kwenye sanduku kwa nia ya kumuua. Kitendo hiki kilikuwa makosa makubwa miongoni mwa watu wa Umuaro. Mtu aliyefiwa anatarajiwa kuonyesha hesima kubwa katika mazishi ya hao watu wa ukoo wake waliokufa kwa sababu yeye ndiye ana uhusiano nao. Kutokana na methali hii, inadhihirika kuwa, mtu aliyefiwa akikosa kufanya ilivyotarajiwa huwafanya watu wengine kususia kumsaidia.

Inaelekea kuwa methali hii inatumiwa kusuta watu ambao hujiingiza katika matatizo na kutarajia msaada wa wenzao, sawa na methali ya Kiswahili *msiba wa kujitakia hauna kilio* au *Mwiba wa kujichoma hauambiwi pole*. Methali hizi zingetumiwa kutafsiri methali hii ya Ki-Igbo badala ya maelezo yaliyotolewa na Shamte ambayo yamepoteza mtindo na kubana uelewa wa msomaji kwa sababu yanataja maswala ya kigeni kwa msomaji wa Kiswahili. Ila methali hizi hazingetumika kwa sababu msisitizo upo kwenye tafsiri ya methali na misemo kama viwakilishi vya utamaduni, zaidi ya kuwa mapambo ya lugha.

#### 4.2.6 Asasi za Kijamii

	<i>Methali/misemo Kiingereza</i>	<i>Tafsiri katika Kiswahili</i>
1	<i>A woman who carries her <b>head on a rigid neck as if she is carrying a pot of water will never live for long with any husband.</b> (uk.175)</i>	<i>Mwanamke anayekwenda na kichwa chake <b>juu ya shingo kakamavu</b> kama aliyejitwika mtungi wa maji, <b>hataishi muda mrefu na mume yeyote</b> (uk.153)</i>
2	<i>He is a fool who <b>treats his brother worse than a stranger.</b> (uk.97)</i>	<i>Ni <b>mjinga mtu anayemtendea nduguye vibaya kuliko mgeni</b> (uk.83)</i>
3	<i>Msemu <b>A boy sent by his father to steal does not go stealthily but breaks the door with his feet</b> (uk.19)</i>	<i>Mtoto <b>atumwae na baba yake kuiba haendi kwa kunyemelea bali huuvunja mlango kwa miguu yake</b> (uk.16)</i>

Asasi za kijamii zinajitokeza katika viwango mbali mbali, zipo methali zinaonyesha asasi ya ndoa, kwa mfano *A woman who carries her **head on a rigid neck as if she is carrying a pot of water will never live for long with any husband*** (uk.175). Akuebue anamwambia rafikiye Ezeulu kwamba amemwambia bintiye Udenkwo msemu huu mara kwa mara ila hamsikii. Kulingana na Akuebue, Udenkwo ana utukutu kama wa mamake na kwa sababu hiyo alikuwa amegombana na mumewe na kurudi nyumbani kwa babake, Akuebue. Msemu huu umetafsiriwa kuwa *Mwanamke anayekwenda na kichwa chake **juu ya shingo kakamavu** kama aliyejitwika mtungi wa maji, **hataishi muda mrefu na mume yeyote*** (uk.153) katika MWM. Methali hii inasisitiza unyenyekevu wa mke kwa mume wake. Imani hii ina ulinganifu katika utamaduni wa Kiswahili. Hivyo maelezo yanayotolewa kama tafsiri kwa msemu huu yanaeleweka kwa msomaji wa Kiswahili, ila mtindo umepotea. Kwa sababu hii kuna haja ya kutumia tafsiri inayodumisha msemu ili kudumisha mvuto wa kazi ya fasihi. Mtafsiri anaweza kutafsiri msemu huu kwa kuufinyanga msemu wa Ki-Igbo na kuufanya uchukue muundo wa misemo ya Kiswahili kwa mfano *Mwanamke **shingo kakamavu kama aliyejitwika mtungi wa maji, haishi muda mrefu kwa mume yeyote.***

Udugu ni asasi nyingine muhimu katika jamii nyingi za Afrika ikiwemo jamii ya Wa-Igbo. Katika methali *He is a fool who treats his brother worse than a stranger* (uk.97) iliyotafsiriwa, *Ni mjinga mtu anayemtendea nduguye vibaya kuliko mgeni* (uk.83). Asasi hii inabainika na kuonyeshwa kuwa kuna umuhimu mkubwa katika kuwa na uhusiano mzuri baina ya ndugu. Msemu huu umetumiwa na Ezeulu akimjibu rafikiye Akuebue, kwa kumwambia Ezeulu kuwa yeye si mgeni kwa hivyo hakukuwa na haja ya kumkaribisha kwa kola nyumbani mwa Ezeulu. Msemu huu ulivyotafsiriwa unaonyesha ulinganifu katika ujumbe, utamaduni na hata muundo. Tafsiri hii inaweza kukubalika kwa kuwa hakuna msemu unaolingana na huu wa Ki-Igbo katika Kiswahili. Kwa hivyo maelezo haya ambayo yamechukua umbo la msemu ya Kiswahili ni tafsiri mwafaka.

Uhusiano baina ya mtu na mwanawe unatiliwa maanani sana miongoni mwa Wa-Igbo. Msemu *A boy sent by his father to steal does not go stealthily but breaks the door with his feet* (uk.19), ni methali inayoonyesha ujasiri ambao mtoto hupata akijua kuwa anaweza kutegemea babake. Hata kama ni jambo baya kama vile kuiba, mtoto hulifanya kwa ujasiri tena bila tahadhari. Methali hii imetumiwa na Ezeulu kuwaonya wazee waliokuwa wanawatuma Akuakalia na vijana wenzake kwenda Okperi kuuliza maoni ya watu wa Okperi kuhusu msimamo wao kuhusu ardhi yenye mzozo. Wazee wanawaambia waende kwa amani wala wasizue vita. Ezeulu anataja methali hii kuwaonya kuwa hilo ni jambo lisilowezezana. Kupitia kwa methali hii, jukumu la mwanamume katika kuathiri matendo ya mwanawe wa kiume, linajitokeza. Methali hii imetafsiriwa kuwa *Mtoto atumwae na baba yake kuiba haendi kwa kunyemelea bali huuvunja mlango kwa miguu yake* (uk.16). Kwa mara nyingine inadhihirika kuwa utamaduni wa asasi za jamii una ulinganifu hivi kwamba, kutafsiri kwa njia ya moja kwa moja huweza kutimiza mahitaji ya tafsiri. Tafsiri hii iliyofanywa na Shamte, japo ni ya moja kwa moja inaweza kukubalika ingawa inajitokeza kama maelezo.

### **4.3 Hitimisho**

Kulingana na nadharia ya wingimfumo, kuna haja ya kuzingatia mifumo midogo inayounga na kuunda mifumo mikubwa. Kauli hii inatokana na ukweli kuwa kwa kutafsiri kila mfumo katika wingimifumo kwa ufasaha, tokeo linakuwa na ukamilifu na ulinganifu wa kiwango kikubwa baina ya MC na ML baada ya tafsiri. Mtafsiri akitafsiri wingimifumo bila kuzingatia mifumo, anaweza kusababisha upotoshaji na kupotea kwa ujumbe wa mwandishi wa MC katika ML. Tafsiri ya viungo vya utamaduni wa nyenzo za jamii na ule wa jamii huzua maswala mbali mbali. Viungo



tofauti vya utamaduni vina viwango tofauti vya ulinganifu. Utamaduni wa asasi za kijamii ndio ulio na ulinganifu wa kiasi kikubwa, huku imani za kitamaduni na zile za kishirikina zikidhihirisha tofauti kubwa baina yao. Viungo vya utamaduni vyenye ulinganifu huweza kutafsiriwa kwa njia ya moja kwa moja bila kuzua matatizo mengi huku vile ambavyo vina tofauti kubwa zaidi huhitaji mbinu ya uhawilishaji kutumika pamoja na maelezo ya ziada ili kufanikisha jukumu la kuupitisha ujumbe, kudumisha utamaduni na vile vile kufanya jaribio katika kudumisha mvuto wa kazi kwa kudumisha mtindo wa mwandishi wa MC.

Mbinu inayoelekea kuwa mwafaka zaidi ni kutumia methali na misemo katika LL yenye ulinganifu wa maana na methali na misemo katika LC. Kwa mujibu wa Abbas (2015) akimnukuu Robinson (1977), vipengee kama utamaduni na desturi za kitamaduni ni ngumu sana kutafsiri hasa kama mtafsiri anataka kudumisha muundo na muonjo wa methali asilia. Kwa hakika kuangazia utamaduni wakati wote kutakuwa njia mwafaka zaidi kuliko kuangazia sifa za lugha nje ya muktadha. Zaidi, kwa sababu za imani za kidini, tabia na desturi, methali na misemo ya lugha tofauti husheheni maana mbalimbali; kuelewa utamaduni wa lugha chanzi kunaweza kutusaidia kutambua maana za kitamaduni zinazorejelewa ili kuzitafsiri kwa usahihi. Methali kama hizi haziwezi kutafsiriwa kwa njia ya moja kwa moja na sisizi kwa sababu, kwa kufanya hivyo maana ya kitamaduni huweza kupotea. Inabidi kutumia methali katika lugha lengwa yenye wazo sawa na linalotolewa na methali na misemo katika LC

## SURA YA TANO

### MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

#### 5.0 Utangulizi.

Azimio la kufanya utafiti huu lilikuwa kuchunguza tafsiri za methali na misemo katika kazi ya fasihi ambapo fani hizi zimetumiwa kama viungo vyenye mchango wa kipekee katika kazi nzima. Tulikiri tokea mwanzo kuwa Achebe, alitumia methali na misemo sio tu kama viungo vya kupamba riwaya ya AOG, bali pia kama msingi wa kuchimuza maudhui, na kusukuma hadithi. Jukumu kuu la methali na misemo katika AOG kama lilivyojitokeza katika mijadala iliyotangulia kufanywa katika utafiti huu, ni kubadilisha lugha ya Kiingereza aliyoiandikia Achebe ili kuipa uwezo wa kuwasilisha maswala ya Ki-afrika katika uhalisia wake. Jinsi Achebe anawasilisha uafrika ni tofauti na wanavyowasilisha waandishi wengi wa Ki-magharibi ambao hutoa taswira ya Afrika iliyo potovu na inayobana uwezekano wa kujitokeza kwa utamaduni halisi wa Mwafrika. Methali na misemo miongoni mwa viungo vingine vya fasihi simulizi, ni fani zilizoweza kubainisha utamaduni wa Afrika na hasa ule wa Ki-Igbo. Kwa kuwasilisha utamaduni wa Ki-afrika alivyofanya, Achebe anafanya jaribio katika kuinua hadhi ya Uafrika iliyodidimizwa na waandishi wengi wa Kiingereza akitumia lugha hiyo hiyo ya Kiingereza.

Majukumu ya methali basi ni makubwa sana katika AOG, kiasi kwamba ndiyo viungo vya kimsingi katika kazi hii ya Achebe. Katika kutafsiri AOG na riwaya nyingine zenye sifa sawa na za AOG, hatua za tahadhari zinahitaji kuchukuliwa ili kufanikisha majukumu haya makuu ya methali na misemo, la sivyoy, uamilifu huu mkubwa utapotea katika tafsiri. Utafiti huu ulichukua mkondo wa kiuchanganuzi na kuongozwa na nadharia ya wingimifumo. Kulingana na nadharia hii iliyoasisiwa na Even-Zohar na kuendelezwa na Gideon Toury, fasihi inaweza kuchukuliwa kama Wingimifumo. Wingimifumo ni mfumo mkuu uliungwa kwa mifumo mingi inayoingiliana na kuchukua nafasi ama za pembeni au za kati katika wingimifumo. Zaidi, utafiti huu ulitambua kuwa miongoni mwa mifumo mingi inayounga riwaya ya AOG, fani na hasa methali na misemo imechukua nafasi ya kipekee ambayo inaweza kuelezwa kuwa nafasi ya kati ambayo ni kuu. Hali hii inatokana na wingi wa methali na misemo kwenye riwaya na jukumu la kimsingi ambalo viungo hivi vinatimiza.

Katika kuchunguza mfumo huu muhimu wa misemo na methali, utafiti huu ulitambua kuwa methali na misemo pia inatokana na mifumo mbali mbali ya kitamaduni. Kubuniwa kwa methali na misemo huchochewa na utamaduni wa jamii husika na vichochezi hivi hujitokeza katika methali na misemo yote. Utamaduni kama ulivyofafanuliwa katika tasnifu hii, ni chochote kinachohusu kuzaliwa kuishi kufa na kuzikwa kwa binadamu. Utamaduni pia unajitokeza kama mfumo wenye vipengee kadhaa vinavyohusiana na maisha ya binadamu kwa njia moja au nyingine. Kwa hakika utamaduni umejibainisha katika kategoria mbalimbali na katika utafiti huu, kategoria hizi zilichunguzwa kwa kadri zilivyoshawishi kubuniwa kwa methali na misemo iliyojitokeza katika AOG. Kategoria za utamaduni zilizochunguzwa ni pamoja na; utamaduni wa mazingira ya kiikolojia, utamaduni wa nyenzo na utamaduni wa kijamii. Mtazamo kuwa fasihi ni mtandao wa mifumo inayohusiana kwa njia moja au nyingine, ulipelekea kuchunguza mfumo wa methali na misemo pamoja na mfumo wa utamaduni. Uchunguzi huu umejikita katika kuchanganua swala la jinsi utamaduni umeshawishi kubuniwa kwa methali na misemo mahususi, na ujitokezaji wa utamaduni huo katika LL baada ya tafsiri. Kufanya uchunguzi huu kwa kina, kuna manufaa kwa kuwa kunawezesha kutathmini tafsiri iliyofanywa kwa methali au misemo husika. Kimsingi utafiti huu unasisitiza haja ya kufanya uchunguzi wa kipengee kimoja kwa kina ili kuzuka na matokeo yanayoathiri kazi nzima kwa ujumla.

Utafiti huu vilevile umetalii swala la udhibiti wa tafsiri, kwamba ingawa mtafsiri yuko huru kutafsiri kazi yake kwa njia anayoamua yeye, yapo maswala ambayo humdhibiti asifanye tafsiri kwa njia moja au nyingine. Kwa mujibu wa Toury, maswala haya yapo nje ya lugha na hutegemea kiwango cha ukubalikaji wa tafsiri katika LL. Hii ina maana kuwa usahihi wa tafsiri unategemea kiwango cha ukubalikaji katika LL na wala sio kiwango cha ulinganifu baina ya tafsiri na LC. Kwa njia nyingine, ni kusema kuwa tafsiri inayofanywa ni lazima ikubalike katika LL. Kulingana na Toury katika nadharia ya wingimifumo, maswala haya yanayothibiti mkondo wa tafsiri yanaweza kuitwa kwa jumla kanuni za tafsiri. Kanuni hizi za tafsiri zimeainishwa katika makundi matatu; kanuni za matayarisho, kanuni za mwanzo na zile za utendaji ambazo humwongoza mtafsiri katika kufanya maamuzi muhimu katika kutafsiri kazi yoyote ya fasihi. Kanuni za matayarisho hudhibiti mikakati ya kutafsiri na maamuzi kuhusiana na uteuzi wa kazi zitakazotafsiriwa ili ziingie katika wingimifumo fulani. Toury anasema kuwa hizi kanuni zinahusiana na kuwepo kwa sheria zinazodhibiti tafsiri, na pia kiwango cha umoja wa tafsiri.

Sheria za matayarisho ni jumla ya maswala ambayo hudhibiti uteuzi wa aina za matini; au pia matini zitakazotafsiriwa na hivyo kuingizwa katika utamaduni fulani, au lugha fulani katika wakati kipindi fulani cha wakati. Hii ina maana kuwa maswala mengi yanahitaji kuzingatiwa kabla kazi itafsiriwe ili kuingia katika utamaduni fulani. Mwegemeo wa kifasihi wa lugha fulani au utamaduni fulani huwa na mchango mkubwa katika kuamua aina ya matini na matini hasa itakayotafsiriwa. Swala kuu huwa, ni aina gani za tafsiri ambazo utamaduni pokezi utakubali? Ni muhimu kuisitiza kuwa kanuni za matayarisho katika mchakato wa tafsiri huwa nje ya mapendeleo ya kibinafsi ya mtafsiri.

Kanuni za mwanzo ni maamuzi ya kibinafsi ambayo mtafsiri anapaswa kufanya kuhusiana na mikakati ya tafsiri, kwa mfano anaweza kufanya tafsiri itakayodumisha sifa za lugha chanzi au tafsiri itakayodumisha sifa za lugha lengwa. Maamuzi haya hudhibitiwa na mkondo wa tafsiri ambao mtafsiri anauchukua kulingana na mwongozo unaotolewa na kanuni za matayarisho. Aina ya tatu ya kanuni ni kanuni za utendaji, hizi hudhibiti tafsiri yenyewe na hujitokeza katika hatua ya mwisho kabisa ya maamuzi ya mtafsiri. Kanuni hizi hujitokeza katika shughuli ya kutafsiri hasa. Toury anazifafanua kama Maamuzi elekezi yanayofanywa wakati wa tendo la tafsiri lenyewe.

### **5.1 Matokeo**

Kutokana na utafiti huu imejitokeza kuwa, tafsiri nyingi za methali na misemo kutoka AOG hadi MWM zimetafsiriwa kwa kufafanuliwa. Ufafanuzi huu umesababisha methali na misemo kupoteza sifa zao kama methali au misemo. Sababu ya kufanya hivyo ilivyobainika katika utafiti ni kwamba Shamte alichukua mwelekeo wa tafsiri ambao haukupatia methali na misemo nafasi yao katika wingimifumo kama ilivyostahili. Shamte alivichukulia vipengee hivi vya fani kwa ukawaida sana na kwa sababu hiyo hakuvipa kipaumbele katika tafsiri yake alitoa tafsiri sisisi bila kuzingatia uamilifu wa vipengee hivi kama viwakilishi vya utamaduni.

Mbinu ya kutafsiri misemo na methali katika LC kwa kutumia methali na misemo kutoka kwa LL yenye uamilifu sawa, na kadri iwezekanavyo yenye miundo sawa ya kileksika, ndiyo imependekezwa zaidi na wataalamu wengi wa tafsiri. Tofauti na mapendekezo haya, Shamte ametumia mbinu hiyo kwa kiwango kidodo sana katika kutafsiri methali na misemo kutoka kwa AOG, hadi kwa, MWM. Zaidi, kutokana na utafiti huu imedhihirika kuwa si rahisi kupata methali na misemo katika LL ambayo ni linganifu na methali na misemo ya MWM. Kutokana na hali hii,

utafiti huu unaunga mkono pendekezo la kutumia maelezo ya methali na misemo katika LC, lakini maelezo hayo yabadilishwe kimuundo ili yajitokeze kama methali na misemo katika Kiswahili. Kwa kufanya hivi, ladha ya methali na misemo itadumishwa katika LL, na msomaji wa kazi iliyotafsiriwa atapokea ujumbe kwa usahihi na dhamira ya mwandishi itatimia.

Baadhi ya tafsiri za methali na misemo zinazojitokeza katika MWM si sahihi kwa sababu zinawasilisha maana zisizolingana na maana za methali na misemo iliyotumiwa na mwandishi wa MC ambayo ni AOG. Tokeo la makosa haya ni kwamba msomaji wa ML, hupotoshwa kutokana na udhaifu huu wa mtafsiri wa kutafsiri visivyo. Mbinu alizotumia Shamte kutafsiri methali na misemo kutoka AOG, hadi MWM, ni pamoja na: uhawilishaji, utohozi, ukopaji udondoshaji, viziada (wakati mwingine maelezo yasiyo ya lazima), miongoni mwa mbinu nyingine. Nyingi miongoni mwa mbinu hizi, japo ziliwasilisha ujumbe wa Achebe kwa Kiswahili, zilifanya tokeo la tafsiri hii, yaani MWM, kuwa riwaya ya Kiswahili ambayo ina sifa za Ki-Igbo ambazo ni ngumu kwa msomaji wa kawaida wa Kiswahili kung'amua. Jambo lingine ni kuwa mbinu ya ufafanuzi aliyoitumia pia ilipoteza methali na misemo mingi iliyo katika AOG, kwa MWM, hivi kwamba ule msambao mkubwa wa methali na misemo katika AOG, haujitokezi katika MWM. Kwa kuwa methali na misemo kwapamoja iliunga kitovu cha ujumbe na dhamira ya Achebe, kupotezwa kwao vile vile kumesababisha kudhoofika kwa uafikiaji wa dhamira ya Achebe ya kuandika riwaya AOG katika tafsiri yake kwa Kiswahili.

## **5.2 Mapendekezo**

Katika utafiti huu tafsiri za methali na misemo kama viwakilishi vya utamaduni zimeshughulikiwa.

Hata hivyo, methali na misemo ni baadhi tu ya vifani ambavyo huwa na uamilifu wa kipekee katika kazi za fasihi. Uamilifu huu ni pamoja na kupamba lugha na kuifanya iwe na mvuto wa kipekee katika mawasiliano ya kimazungumzo au kwenye maaandishi. Uamilifu mwingine ni kuchora taswira akilini mwa mpokeaji ujumbe unaotolewa kupitia kwa vifani hivi kwa njia ambayi itafanya, ujumbe huo kueleweka kwa njia mahususi, miongoni mwa majukumu mengine. Ingekuwa bora kama utafiti zaidi ungefanywa ili kushughulikia tafsiri za fani nyingine na vipengee vingine vya fasihi katika fasihi kwa mwelekeo huu wa uchanganuzi wa kiuteuzi ili kuzuka na matokeo na mapendekezo yatakayopelekea kufanywa kwa tafsiri amilifu katika viwango mbalimbali vya fasihi.

## MAREJELEO

- Abbas, F. (2015) *An Analysis of Translation Methods for English Proverbs: Literal, Literary or Substitution*. European Academic Research- Vol. II, Issue 11/February 2015 [www.euacademic.org](http://www.euacademic.org)
- Achebe, C. (1958). *Things Fall Apart*. Toronto:Anchor Canada (New York: Anchor Books, 1994).
- Achebe, C. (1964) *Arrow of God*. East Africa Education Publishers Ltd. Nairobi
- Aderinto, S.I.A (2014). *The Social Implications of Some Nigerian Yoruba and IBO Proverbs on Carefulness* *European Journal of English Language and Literature Studies* Vol.2, No.2, pp.49-55-June 2014 Published by European Centre for Research Training and Development UK([www.ea-journals.org](http://www.ea-journals.org))
- Al-Shawi, M., na Mahadi, T. (2012). Strategies for translating idioms from Arabic into English and vice versa. *Journal of American Arabic Academy for Sciences and Technology*, 3(6) 139- 147. Lloyd, W. B. (1972). Cultural Norms and Modes of Perception in Achebe's Fiction. *Research in African Literature*, 3 21-25
- Amadiume, S. (1995). *Ilu ndi Igbo*, Fourth Dimension Publishers, Enugu.
- Anigbogu, N.C.& Ahizih, F.C (2016). *Language use in Arrow of God: A socio-linguistic dimension* *European Journal of English Language and Literature Studies* Vol.4, No.1, pp.60-68, January 2016 European Centre for Research Training and Development UK ([www.eajournals.org](http://www.eajournals.org))
- Awa, S & Ngele, C. (2014). *Absence of Local Flavour: Presentation of Igbo Proverbs in English and French* AN AFRICAN JOURNAL OF NEW WRITING NUMBER 52, 01 NOVEMBER 2014 (333-347)
- Baker, M. (1992) *In Other Words: a course book on translation*. London and New York: Routledge. Dabaghi, A. et. Al (2010). *Proverbs from the Viewpoint of Translation*. *Journal of Language Teaching and Research*, Vol. 1, No. 6, pp. 807-814, November 2010 ACADEMY PUBLISHER .doi:10.4304/jltr.1.6.807-814

- Classe, O. ed (2000). *Encyclopedia of literary translation into English* 2<sup>nd</sup> edition. LONDON
- Conolly, J. "(C) (2008). Omissions of Perspective, Lens and Worldview: What Africa Can Learn from the 'Western Mind' about the Oral Tradition of (Indigenous) Knowledge?" *JNGS* 6(3) 22-34.
- Culture and Society in Nigeria. Concept Publications LTD, Lagos, Nigeria (11-27).
- Dabaghi, A. et. Al (2010) *Proverbs from the Viewpoint of Translation*. Journal of Language Teaching and Research, Vol. 1, No. 6, pp. 807-814, November 2010 ACADEMY PUBLISHER .doi:10.4304/jltr.1.6.807-814
- Dare, S.O. (2008). *Theatre and the Celebration of the Material Aspect of Culture in Contemporary Nigeria*.
- Dutta, D. (2010) *Bearing the Burden of Native Experience: A Stylistic Analysis of Chinua Achebe's Arrow of God*. DOI:<https://dx.doi.org/10.21659/rupkatha.v2n2.07>
- Emery, P.(1997). Omani proverbs: problems in translation.in smith, R & Pridham,R(vol.4), *New Arabian Studies*(pp.39-70). Great Britain: Short Run Press Limited,Exeter.
- Even-Zohar, I. (1978) .*The position of translated literature within the literary polysystem*.in *Papers in historical poetics*.Tel Aviv: porter institute.
- Fakih, A. (2018). *Changamoto Za Kutafsiri Riwaya: Mifano Kutoka Tafsiri ya Kiswahili ya Riwaya ya Robinson Crusoe*. Tasnifu ya Shahada ya Uzamili. Chuo Huria cha Tanzania.
- Farahani, A., & Ghasemi, M. (2012). The naturalness in the translation of idioms and proverbs: The case of a Persian translation of Pinocchio. *Journal of Language and Translation*, 3(1) 17-22.
- Firoozkoohi, S. (2010). *Culture-Specific Items in Literary Translation*. Translation journal Volume 14, No. 1January 2010.<http://translationjournal.net/journal/51culture.htm>
- Gaber, J. (2005). *A Textbook of Translation: Concept, Method and Practice*. Al Ain: University Book House.
- Gentzler, E. (2001). *Contemporary Translation Theories*. Multilingual matters
- Gikandi, S. (1991) *Reading Chinua Achebe: Language & Ideology in Fiction*. Oxford.

- Gogoi, G. "A Study on Chinua Achebe's Use of Proverbs in Things Fall Apart and no Longer at Ease." IOSR Journal of Humanities and Social Science (IOSR-JHSS). vol. 22 no. 12, 2017, pp. 52-56. [www.iosrjournals.org](http://www.iosrjournals.org)
- Gorjian, B. (2006). Translating English proverbs into Persian: A case of comparative linguistics.
- Landers, C. E. (2001) Literary Translation: A practical Guide, New Jersey University Press: Multilingual Maters.
- Larson, M.L. (1984). Meaning-Based Translation: A Guide to Cross-Language Equivalence. Lanham and New York: University Press of America, Inc.
- Lawal, N. (2017). July 13, <https://www.penprofile.com/profile/nurudeenlawal>.
- Litovikina, A (2014). Antiproverbs. In H.Gotthardt & M. Varga (Eds) Mgbemere, C. D. Cues in Igbo Cultural Matrix: Analysis of Achebe's *Arrow of God* Journal of Culture, Society and Development- an Open Access International Journal Vol.4 2014 Lloyd, W. B. Cultural Norms and Modes of Perception in Achebe's Fiction. *Research in African Literature*, 3 (1972):21-25
- Marais, J. "The Language Practitioner as Agent: The Implications of Recent Trends in Research for Language Practice in Africa." *JNGS* 6(3) (2008): 35-47.
- Mgbemere, C. D. Cues in Igbo Cultural Matrix: Analysis of Achebe's *Arrow of God* **Journal of Culture, Society and Development-** An Open Access International Journal Vol.4 2014
- Meider, W. (2004). *Proverbs: A handbook*. United States of America: Greenwood Press. <https://books.google.jo/books>.
- Metuh, I. (1999). *God and Man in African Traditional Religion*. Enugu: SNAAP
- Mollanazar, H. (2001). *Principles and methodology of translation*. Tehran: SAMT
- Mule, K. (2002). *Translation, Mistranslation, and Cultural Theory: African Inflections, Challenges, and Prospects*. *Metamorphoses*, spring 2002 .10.1 Academic Research



- Mutie, E. K. (1997). *Sanaa katika Tafsiri: Matatizo na Athari Zake*.Tasnifu ya Shahada ya Uzamili.Chuo Kikuu cha Nairobi.
- Naudé, M.C & Naudé, J .A. *The Translator as an Agent of Change andTransformation: The Case of Translating Biblical Proverbs*. Agent of Change OTE 23/2 (2010), 306-321
- Nel, P. J. (2008). “Indigenous Knowledge Systems and Language Practice: Interface of a Knowledge Discourse.” *JNGS* 6/3 94-108.
- Newmark, P. (1988). *A Textbook of Translation*, London: Prentice Hall. Newmark, P. (1998) *More Paragraphs on Translation*. New Jersey University Press: Multilingual Maters.
- Nida, E.A. and C. R. Taber (1969). *The Theory and Practice of Translation*. Leiden: E.J. Brill. Shuttlewort
- Nzyoka, S. (2014). *Tathmini Ya Tafsiri Na Mikakati Ya Kutafsiri Tamathali Za Usemi Katika Tamthilia Ya Antigoni*. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu Cha Kenyatta.
- Palmer, E. (1979). *The growth of the African Novel*. London: Heinemann Educational Books Ltd.
- Pedersen, J. (2005). “How is Culture Rendered in Subtitles?” In: *Challenges of Multidimensional Translation: Proceedings of the Marie Curie Euroconferences MuTra: Challenges of Multidimensional Translation*. Saarbrücken, 2nd – 6th May 2005. Stockholm: Stockholms universitet. 1–18.
- Petrulione, L. (2012). “Translation of Culture-Specific Items from English into Lithuanian: The Case of Joanne Harris’s Novels”. In: *Studies about languages*. No 21, 2012. ktu. 43–49. <http://www.kalbos.ktu.lt/index.php/KStud/article/view/2305> [2015, May 6]
- Robinson, D. (1997). *Becoming A Translator: An Accelerated Course*. London: Oxford.h, M. and M. Cowie, Eds. (1997) *Dictionary of Translation Studies*. Manchester: St Jerome.

- Samovar, L.A., Porter, R.E & McDaniel E.R. (2009). *Intercultural communication: a reader*. SouthMelbourne, Australia: Wadsworth Cengage Learning.
- Shamte, H. (1978) *Mshale wa Mungu* Heinne Educational Books
- Shastri, P. D. (2012). *Fundamental Aspects of Translation*. New Delhi PH/learning.
- Shuttleworth, M. and M. Cowie, Eds. (1997) *Dictionary of Translation Studies*. Manchester: St Jerome.
- Toury, G. (1980). "The Nature and Role of Norms in Translation", Lawrence Venuti, ed., *The Translation Studies Reader*. Abingdon: Routledge, 2004, 205-218.
- Venuti, L. (2000). *The Translation Studies Reader*. London
- Vinay, J. P., & Darbelnet, P. (1995). *Comparative stylistics of French and English: A methodology for translation*. Translated by J.C. Sager & M. J. Hamel. Amsterdam and Philadelphia: John Benjamins: Routledge.
- Xizhi ZHANG (2014) Application of Polysystem Theory in the Field of Translation, *Comparative Literature: East & West*, 20:1, 138-143, DOI: 10.1080/25723618.2014.12015480
- Zaja O. (1986). *Fasihi Tafsiiri katika Ukuzaji wa Fasihi ya Kiswahili*. Tasnifu ya M.A. (Haijachapishwa), University of Nairobi.